# MWONGOZO WA CHOZI LA HERI.

## 1. NAMNA YA KUUTUMIA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu unanuiwa kumwonqoza mwanafunzi ili kuilewa vyema pamoja no kuelewa uliopo kwenye Riwaya. Hata hivyo ni muhirnu mwanafuzi aisome Riwaya kwanza kabla ya kuutumia mwongozo huu.

Pia ni vizuri mwanafunzi kuisoma na kuielewa Riwaya hata kama ni mara tatu, kabla ya kuujjbu mtihani wake mwisho wa Sekondari(KCSE). Mwongozo huu ni maoni ya waandishi kulingana na jinsi walivyoifiki Riwaya hii, wenyewe. Mwanafunzi anahimizwa kuzua maoni ziada kuhusu masuala waliyozungumzia waandishi huku jaribu kuyaoanisha na hali halisi katika eneo alirnotok, :,nchini, barani au kwingineko ulimwenguni ambapo maudhw yanayojadiliwa yanajitokeza. Kuna maelezo kuhusu uliotumika kwenye jalada, Ufaafu wa anwani, rnuhtasari wa sura(msukomtiririko) ,dhamira ya mwandishi, maudhui, sifa za wahusika, fani na Maswali ya marudio. Haya yote yanalenga kumhamasisha mwanafunzi kuielewa vyema Piwaya

Chozi la Heri. Ni muhimu kwa mwanafunzi kuelewa rntlririko wa Riwaya kwa undani ili kuweza kuelewa ujumbe wa mwandishi na mbinu anazotumia kuubainisha ujumbe huo. Fahamu kuwa iwapo mwanafunzi atauelewa mtiririko wa kazi hus ka hatatatizika wakati wa kuyajibu maswali, akakanganva matukio au 'kubuni' matukio ambayo hayamo Riwayant.

Katika sehemu ya mwisho, waandishi wametoa mifano ya maswali pamoja na mifano ya majibu mwafaka. Mwanafuntl ajibidiishe ili kuwa na uzoefu wa kuyajibu maswali atakayo ulizwa na mtahini katika mitihani ya karatasi ya 3 tatu

Shukrani

## Mwandishi

Assumpta K.Matei ni mwandishi wa kike. Ni mtafiti na mwalimu mwenye tajriba pana katika ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili katika shule za upili na vyuo vikuu. Kati ya taasisi alizowahi kufundisha ni Kenya High Schoolna

CUEA. Ameshiriki katika majopo mbalimbali ya ukuzaji, utekelezaji na tathmmi ya mitaala. Hivi sasa ni afisa katika

Wizara ya Elimu, kitengo kinachoshughulikia tathmini ya mitaala. Miongoni mwa kazi alizoziandika ni Fani ya Fasihi

Simulizi.

## JALADA

Jalada la Riwaya ya Chozi la Heri ni tokeo la usanii wake , Robert Kambo. Katika upande wa mbele sehemu ya juu, mna rangi ya kijani kibichi iliyokolea. Maana ya rangi hii ni uhai na rutuba. Riwayani yamo maeneo yaliyo na rutuba yanayotoa mazao mengi. Katika eneo la Msitu wa Heri alikoishi Ridhaa kwa miongo mitano, mwanzoni kulikuwa kama jangwa la

Kalahari lakini Ridhaa alihakikisha kuwa kijiji hiki kimepata maji ya mabomba hadi eneo zima likatwaa rangi ya chanikiwiti. Miti mingi kama Miambakofi, mivule na miti mingine kapandwa. Maeneo mengme yaliyokuwa na rutuba ni kama

Msitu wa Mamba. Watu waliogura makwao walipohamia hapa walikata miti na kupanda vyakula kama mahindi ambayo yalifanya vizuri mno.

Ndam ya rangi hii mna anwani ya kazi iliyoandikwa kwa rangi nyeupe. Kawaida rangi hii huashiria amani. Licha ya mambo kuwaendea vibaya wahusika wengi riwayani, hatimaye mna

amani ya kudumu.

Jina lake mwandishi liko maeneo yayo hayo na limeandikwa kwa rangi ya manjano. Rangi hii huashira ukomavu. Mwandishi wa riwaya hii ni mwenye tajriba pana. Amekomaa katika uandishi wa kazi za fasihi. Masuala anayoyaangazia ni yale yanayoiathiri jamii yake. Ametumia mtindo unaoashiria upeo wa ukomavu wake.

Upande wa chini wa jalada la riwaya hii mna mchoro wa jicho. Jicho hili linadondokwa na chozi. Ndani ya chozi mna watu watatu(mmoja wa kike na wawili wa kiume). Inahalisi kuwa watu hawa watatu ni Umu, Dick na Mwaliko. Walifurahl mno walipokutana wote katika hoteli ya Majaliwa. Riwayani, Umu na Dick walikimbia wote kwa pamoja na wakamkumbatia ndugu yao Mwaliko na huku wakaanza kulia na kutokwa na machozi ya farajaheri.

## *4.UFAAFU WA ANWANI*

Anwani ya Riwaya hii ni Chozi la Heri.

Kwa mujibu wa kamusi ya karne ya 21, CHOZI ni tone la maji au uowevu linalotoka machoni ambalo aghalabu hutokea mtu anapolia, kufurahi au moshi unapoingia machoni. Nalo jina

HERI lina maana tatu 1 Ni kuwepo kwa amani, utulivu na usalama 2Ni hali ya kupata Baraka na mafanikio 3 Ni afadhali. Maneno haya yanapotumika pamoja tunapata maana iliyo na undani zaidi kuliko jina likitumika peke yake.

Kwa hivyo, chozi la heri ni chozi ambalo linatoka wakati mhusika fulani amepata amani, utulivu na usalama. Chozi

kwisha kupata baraka na mafanikio. Maana nyingine ni kuwa chozi hili linaonekana ni chozi (la) afadhaliboranafuu.

Kwa kujikita katika maana mbalimbali yanayojitokeza wakati maneno hayo mawili yamewekwa pamoja, matukio yafuatayo yanaafiki ufaafu wa CHOZI LA HERI.

i) Mwandishi anatuleza kuwa Ridhaa alipokwenda shuleni siku ya kwanza alitengwa na wenzake kwani hawakuta ashiriki michezo yao. Kijana mmoja mchokozi alimwita 'mfuata mvua' aliyekuja kuwashinda katika mitihani yote. Ridhaa alifululiza nyumbani na kujitupa mchangani na kulia kwa kite na shake. Mamake alimliwaza na kumhakikishia kumwona mwalimu keshoye. Tangu siku hii, huu ukawa ndio mwanzo wa maisha ya heri kwa Ridhaa kwani baada ya mwalimu kuzungumza na wanafunzi umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano, Ridhaa alipea kwenye anga ya elimu hadi kufikia kilele cha elimu na kuhitimu kama daktari.

ii) Ridhaa alipotoka kwenye Msitu wa Mamba alijiona nafuu kwani wapwa zake- Lime na Mwanaheri walikuwa wamepata matibabu. Dadake Subira alitibiwa akapona. Mwamu wake

Kaizari amepona donda lililosababishwa na kuwatazama mabinti zake wakitendewa ukaini(kubakwa) na Vijana wenzao.

Ridhaa anajua kuwa Kaizari ni afadhali kwa sababu hakuna aliyemtenga na mmoja kati ya jamaa zake. Ridhaa anapomfikiria Kaizari anajiambia heri nusu Shari kuliko Shari kamili.

iii) Ridhaa aliposikia sauti ya kike ikitangaza, tangazo lile lilimrudiSha katika mandhari yake ya sasa. Alijaribu kuangaza macho yake aone anakoenda lakini macho yalijaa uzito wa machozi ambayo alikuwa ameyaacha yamchome na kutiririka

yatakavyo.

iv) Wakati Ridhaa alimkazia macho Mwangeka-waka

Mwangeka alikuwa akijiuliza iwapo babake amekuwa mweh kwa kukosa kushirikiana na majirani kuchimba kaburi kuyazl ka majivu- matone mazito ya machozi yalitunga machor mwake Mwangeka. Akayaacha yamdondoke na kumcharaz, yatakavyo. Uvuguvugu uliotokana na mwanguko wa macho:

haya uliulainisha moyo wake, ukampa amani kidogo. Moy wake ukajaa utulivu sasa kwa kujua kuwa wino wa Mung haufutiki.

v) Wakati Ridhaa alikuwa akimsimulia Mwangeka misib(

iliyomwandama tangu siku alipoondoka kwenda kuwel"amani Mashariki ya Kati, Ridhaa alisita akajipagusa kijash(

kilichokuwa kimetunga kipajini mwake kisha akatoa kitambm mfukoni na kuyafuta machozi yaliyokuwa yameanza kumpo fusha. Uk 48

vi) Mwangeka alipokuwa ameketi mkabala na kidimbwi che kuogelea, mawazo yake yalikuwa kule mbali alikoanzia

Akawa anakumbuka changamoto za ukauji wake. Akawa kumbuka wanuna wake. Alipomkumbuka Annatila(Tila) mwili ulimzizima kidogo akatabasamu kisha tone moto la choz:

likamdondoka.

vii) Katika Msitu wa Simba kulikuwa na maelfu watu waliogura makwao. Kati ya familia zilizoguria humu ni familia ya Bwana

Kangata. Kwa Kangata na mkewe Ndarine, hapa palikuwa afadhali kwani hawakuwa na pa kwenda kwa kuwa hata kule walikokuwa wakiishi awali hakukuwa kwao. Uk57

wongo: o wa chozi la Heri viii)Wakati Dick walikutana kisadfa na Umu katika uwanja wa ndege, walikumbatiana kwa furaha. Machozi yaliwadondoka wote wawili na wakawa wanalia kimyakimya. Walijua fika kuwa jaala ilikuwa imewakutanisha na kwamba hawatawahi kutengana tena. Maisha sasa yalianza kuwa ya heri kwao.

ix)Baada ya miaka kumi ya kuuza dawa za kulevya, Dick alifaulu hatimaye kujinasua kutoka kwa kucha za mwajiri wake. Alianza biashara yake mwenyewe ya kuuza vifaa wa umeme. Sasa akaanza kujitegemea kwa kuwa amejiajiri.

Alikuwa ameufungua ukurasa mpya katika maisha yake.

Maisha yake sasa ni ya heri.

X)Wakati Neema na Mwangemi walikabidhiwa mtoto wao wa kupanga na Mtawa Annastacia, Mwaliko alimkumbatia Neema na kumwita mama na kumwahidi kuwa ataenda naye. Neema alidondokwa na chozi la furaha na kumkumbatia Mwaliko kwa mapenzi ya mama mzazi. Hili lilikuwa ni chozi la heri kwa

Neema.

xi)Dick alimweleza Umu kuwa siku waliokutana katika uwanja wa ndege na wakasafiri pamoja, hiyo ndiyo ilikuwa siku ya heri Zaidi kwake. Nasaha alizopewa na IJmu zilimfunza thamani ya maisha. Kisadfa, huu ndio wakati Dick alikuwa ameamua kubadilisha maisha na kuishi maisha mapya yasiyokuwa ya kuvunja sheria.

Xii)Dick aliposimulia namna wazazi wake wapya pamoja na

Umu walivyomfaa maishani, kila mmoja katika familia hii alijil. Bila shaka yalikuwa machozi y

xiii) Baada ya Mwaliko kujitambulisha kwa Umu na Dick, umu na Dick hawakungojea amalize. Walikimbia wote wakamkUmbatia ndugu yao, wakaanza kulia huku wakiliwazana. Haya yalikuwa machozi ya furaha kwao kwa kupatana tena wote wakiwa hai. Kwa kweli kila mmoja alitokwa na chozi la heri.

xiv) Mwaliko alimwambia babake kuwa kuja katika hoteli ya

Majaliwa kuliwaletea heri kwa kuwa familia yao sasa imepanuka. Sasa amekutana na watu aliokuwa tu anasikia wakitajwa. Maisha sasa ni afadhali.

xv) Dick alitoa shukrani tele kwa Umu kwa kuwa alimpa matumaini kuwa siku moja watampata ndugu yao Mwaliko. Mwaliko hata anapomtazama Umu, macho yake yakiwa yamefunikwa na vidimbwi vya machozi, anajua kuwa familia yao imerudiana japo katika mazingira tofauti.

xvi) Siku ambayo Mwangeka alimwoa Apondi ilikuwa siku ya heri kwake kwani alimwaga chozi la heri. Tunaelezwa kuwa, Ridhaa alijua kuwa wakati ndio mwamuzi, ipo siku atakapotokeza hurulaini wake Mwangeka. Ataifungua kufuli kubwa iliyoufunga moyo wake na hiyo itakuwa siku ya kumwaga chozi la heri.

Mbunda Msokile(1992:206) anasema kuwa msuko ni mtiririk0

au mfuatano wa matukio yanayosimuliwa kutoka mwanz0

hadi mwisho. Hapa tutaangazia matukio katika kila sura

## SURA YA KWANZA

Sura hii inapoanza, Ridhaa alikuwa amesimama kwa maumi-vu makali huku mikono kairudisha nyuma ya mgongo wake uliopinda kwa uchungu. Amelitazama wingu la moshi ambalo linamkumbusha ukiwa aliozaliwa nao na ambao anahofia kuwa angeishi na kuzikwa nao. Alipogeuka alitazamana ana kwa ana na moto ambao uliteketeza jumba lake la kifahari. Walioangamia mie ndani ni Terry (mkewe Ridhaa),bintiye Tila, Mkewe Mwangeka(Lily) na mjukuu wake Becky. Tukio hill linamkumbusha mambo kadha yaliyotokea hapo awali yakiwemo mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama. Milio hii ilimtia kiwewe zaidi kwani bundi hawakuwa wageni wa kawaida katika janibu hizi. Alikumbuka akimwambia Terry kuwa milio hii ni kama mbiu ya mgambo ambayo ikilia huenda kukawa na jambo. Terry ambaye kawaida yake ni mcheshi hakunyamaza ball alimwambia Ridhaa kuwa kwake lazima kila jambo liwe na kiini. Terry alis-hangaa ni vipi daktari mzima alikuja kujishughulisha na mambo ya ushirikina. Terry anamkumbusha mmewe kuwa aliwahi kumwambia kuwa ni vizuri kuiacha mielekeo ya kijadi ambayo huyafifilisha maendeleo. Anazidi kumuuliza hata iwapo jambo likawa atafanya nini? Ndipo Terry anamjuvya kuwa la muhimu ni kumlaani shetani kwani Iiandikwalo ndilo liwalo. Mazungumzo haya baina ya Terry na mmewe Ridhaa yalikuwa ya mwisho kabisa kutokea Terry akiwa hai. Ridhaa sasa anajutia kuwa angelijua angelitumia kila sekunde za uhai zilizokuwa zimesalia kumuuliza mkewe maswali ambayo sasa yameivamia akili yake. Machozi yalifulika machoni mwake na kuulemaza uwezo wake wa kuona na ndipo moyo wake ukamwonya dhidi ya II

tabia yake ya kike ya kulia pindi tu akumbwapo na vizingiti ambavyo ni kawaida ya maisha. Aliyakumbuka maneno ya marehemu mamake kuwa machozi ya mwanamme hayapaswi kuonekana mbele ya majabali ya maisha. Siku hii Ridha hakujali la mama wala la baba; alijiskia kama mpigana masumbwi aliyebwagwa na kufululiziwa makonde bila mwombezi. Alisalimu amri na kuyaacha machozi yamvamie yatakavyo. Katika mito ya machozi ndipo alileta kumbukumbu ya mambo yalivyokuwa usiku ambao uliyatia giza maisha yake. Anakumbuka mayowe ambapo mwenye kuyapiga alimsihi

Mzee Kedi asiwauwe kwani wao ni majirani wake. Akamsihi asiwadhuru wanawe wala mume wake. Baada ya mayowe haya ndipo alisikia mlipuko mkubwa kisha akashikwa na uziwi wa muda uliofuatwa na sauti nyingine ya Mkewe "Yamekwisha". Kumbukumbu hii ilimpa kuzimia na alipozinduka alijipata kalala kando ya gofu la jumba lake lililokuwa linafuka moshi. Alijikongoja hadi kwenye kwenye shamba lililokuwa kando ya nyumba yake alipopaaza sauti na kusema " Familia yangu na mali yote hii kuteketea kwa siku moja?

Aliporudi kulikokuwa sebule ndipo alikumbuka kuwa

Mwangeka (kifungua mimba) wake alizaliwa kwenye chumba hiki miaka thelathinl iliyopita. Alishangaa ni vipi Mwangeka aliweza kunusirika mkasa huu na ndipo akawaza kuwa wadhifa aliyopewa kwenda Mashariki ya Kati kudumisha amani ulitokea kuwa wongofu wake. Katika kumbukumbu zake anaukumbuka mjadala mkali baina yake na bintiye Tila kuhusu mafanikio ya baada ya uhuru. Hakuna aliyethubu kuuchangia kwani masuala ya sheria Tila alikuwa ameyamu

d e i kweli. Tila anamuuliza babake maswali magumt ambayo yanamsawiri Mwafrika alivyonyanyaswa na tabaka le juu lililojilimbikizia mali baada ya mzungu kuondoka, likabaki likiukomaza ukoloni mambo leo. Mwafrika alibaki pasi na cho-

Chote cha kumiliki. Tila anasisitiza kuwa wao ni wategemezi si kwa lishe tu, bali pia kwa ajira. Na kazi zenyewe ni vibarua vya kijungu jiko. Tila alishangaa ni kwa nini wao hawajaanza kujisagia kahawa au chai yao. Haihalisi mbegu ziwe zetu, tulikuze zao lenyewe kisha kumpelekea mwingine kwenye viwanda vyake alisage kisha kuja kutuuzia hiyo kahawa au chai kwa bei ya kukatisha tamaa alisisitiza Tila. Ridhaa alikubaliana na mtazamo wa Tila kwani mstakabali wao wa ukuaji kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilimpa mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zinazotoa mazao mengi. Mwafrika akabaki aidha kuwa kibarua au skwota ambaye maisha yake yalitegemea utashj wa mzungu. Wafrika ambao walibahatika kupata makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao mengi, wakawa wakulima wadogo wadogo, maskini wasio na ardhi. Ridhaa anamkumbuka baba Msubili alivyokuwa akisema kuwa jamii yao iligeuka kuwa hazina ya wafanyakazi ambamo Wazungu wangeamua kuchukua vibarua kupalilia mazao yao.

Ridhaa hakuwa mkaazi asilia wa Msitu wa Heri. Alikuwa

Tuata mvua kama walivoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki. Ridhaa anasema kuwa hakupachagua mahali hapa ila majaliwa yalitaka awe hapo. Babake alikuwa na wake kumi na wawili. Wake hawa walijaliwa na wana wa kiume ishirini na ndipo ardhi ya mzee Mwimo Msubili ikawa haitoshi kuwalea madume hawa lligawanywa m na

ikamwia vigumu Mzee Mwimo kuwalisha wana hawa kwani ardhi yake ilitoa zao dogo. Katika ardhi ya Mzee Mwimo mlizuka uhasama, migogoro na uhitaji mkubwa. Jambo hili limfanya mzee mwimo kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu via Heri au Ughaishu kama walivyopaita wenyeji. Siku hizo ilikuwa rahisi mtu kuwa na shamba mahali kokote katika eneo lililomilikivia na kabila lake kwani umiliki wa mashamba ulitegemea bidii ya mtu. Mamake Ridhaa alikuwa mke wa mwisho wa Mzee Mwimo. Ridhaa alikuwa mwenye umri wa miaka kumi walipohamia Mlima via Heri na alikuwa bado

hajaanza shule. Walipowasili humu hamkuwa na wakaazi wengi na ilimchukua muda kuzoeana na watoto wa majirani ambao waliwaona Ridhaa na nduguze kama waliokuja kuuvuruga utulivu wao. Ridhaa alipowazia kuhusu jambo hill alielewa fika kuwa hali hii ilizuliwa na wakoloni na kuwarithisha Waafrika. Baba yake, Mwimo Msubili alikwisha kumwambia kabla ya miaka ya Hamsini umiliki wa kibinafsi wa ardhi haukusisitizwa katika jamii yao. Watu walitangama-na vyema. Familia zilizotoka kwengine ziliishi miongoni mwao pasi uhasama. Sera mpya ya mkoloni kujumuisha pamoja ardhi iiiyomilikiwa na mtu binafsi na kuuidhinisha umiliki huu kwa hatimiliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii. Sera hii mpya ya umilikaji wa ardhi ilimaanisha kwamba wale walio-kosa pesa za kununulia mashamba wangekosa mahali pa kuishi. Wale waliobahatika kuwa na pesa za kununulia mashamba daima walichukuliwa kama wageni wasiopasa kuaminiwa. Ridhaa alikuwa kati ya waathiriwa wa hali hii kwani alitengwa na wenzake siku ya kwanza shuleni katika michezo mbalimbali. Alichokozwa na mwanafunzi mmoja aliyemwita 'mfuata mvua' na kumwambia hakutaka kucheza naye kwani alikuja kuwashinda katika mitihani yote. Jambo 14

hili lilimfanya Ridhaa kulia kwa kite na kumwambia mamake kuwa hangerudi shuleni tena. Mamake alimwambia ni vyema kujifunza kuishi na wenzake bila kujali tofauti za kiukoo na nasaba. Mamake Ridhaa alizungumza na mwalimu naye mwalimu akazungumza na wanafunzi na kuwasisitizia umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano. Huu ukawa ndio mwanzo wa maisha ya heri kwa Ridhaa. Ridhaa alifanya vyema masomoni na kufikia kilelecha cha ufanisi alipohitimu kama daktari. Baadaye aliasi ukapera na akafunga ndoa naye

Terry. Alijaliwa na wana ambao waliangamia isipokuwa

Mwangeka. Ridhaa anashangaa ni kwa nini Mzee Kedi alimgeuka kwani ndiye aliyemsaidia kupata shamba hilo lake.

Familia zote mbili zilikuwa na mlahaka mwema. Ridhaa ameyafanya mengi mazuri kikijini hadi kikaacha kuitwa Kalahari. Ikawaje aliowatendea hisani wamelipa kwa madhila?

lweje watu waliokula na kunywa pamoja ndio waliomlipulia aila na kuyasambaratisha maisha yake? Haya maswali yasiyo na majibu yalimsumbua akilini mwake. Alipowaza alianza kuelewa sababu ya vikaratasi kuenezwa kila mahali vikiwatahadharisha kuwa mna gharika baada ya kutawazwa kwa

Musumbi- kiongozi mpya. Anaelewa sababu ya jirani kuacha kumtembelea kwake kwa ghafla. Anaelewa sababu ya mke wa jirani kulalamika kuhusu kuuzwa kwa mashamba ya wenyeji kwa wageni. Alielewa kuwa alikuwa mgeni wala si mwenyeji hata baada ya kuishi pale miongo mitano. Katika usingizi alikumbuka habari iliyosomwa katika runinga miaka miinne iliyopita. Habari ilisema kuwa matrekta ya Baraza ya jiji yalitekeleza amri ya Bwana Mkubwa ambayo ilikuwa ni kwabomoa majumba ishirini katika mtaa wa kifari wa Tonon-

Okeni. Ridhaa alitazama picha za majumba yake matatu

kwenye mulishi wa runinga yakibomolewa. Majumba haya sasa yamegeuka udongo. Pigo hili la pili aliliona kali zaidi.

Alibaki akijiuliza maswali akishangaa ni upi utakuwa mstakabali wake, wa mwanawe Mwangeka na Subira, dada yake

Ridhaa aliyeishi maili kumi kutoka pale.

**<u>Maswali</u>**:

***i)Eleza kwa kifupi hasara ya ukabila.***

***ii) Ni mambo gani yalifuatia kutawazwa kwa Musumbi ?***

***iii) Ni mambo gani yalimpata Ridhaa tangu walipohamia Msitu wa***

***Heri?***

***iv) Wataje, kisha utoe sifa za wahusika waliotajwa katika sura hii.***

***v) Onyesha namna mbinu rejeshi ilivyotumiwa katika sura hi*i.**

**SURA YA PILI**

Ni siku kumi tangu kuondoka kwa Kaizari na wenzake na kujipata katika mazingira haya mageni. Si mageni kwani ni mumo humo kwao kwani si ughaibuni wala nchi jirani. Pahali hapa ni kambi au mabanda yaliyosongamana. Waliokuwa nacho na wachochole wote wako pamoja katika kambi hii.

Kuna kiasi fulani cha usawa. Japo wanasema kuwa wanadamu huwa sawa kifoni, kuna tofauti katika mandhari wanamofia. Kuna wanaofia zahanati za kijijini na wapo wanaolala maumivu yao yakiwa yamefishwa ganzi katika hospitali za kifahari huku wakiliwazwa na mashine. Kuna wengine ambao hufia kwenye vitanda vya mwakisu vitongojini baada ya kupiga maji haramu(pombe haramu) kama nzi ambao kufia dondani si hasara. Kuna tofauti pia mitindo ya mazishi na

hata mavazi ya mwenda zake na wafiwa. Hata majenez yenyewe huhitilafiana.

Katika kambi la kina Kaizari mipaka ya kitabaka imebanwa.

Kwani, hata waliokuwa navyo sasa hivi wanang'ang'ania chakula haswa uji. Hata aliyekuwa waziri wa Fedha miaka mitano iliyopita yumo katika kambi hii aking'ang'ania chakula na wenzake. Mvua kubwa inanyesha na matone mazito kuwaangukia wanawe wakembe wa Ndugu Kaizari-Lime na

Mwanaheri. Hana hata tambara duni la kuwafunikia. Ubavuni amelala mke wake Subira. Anaonekana kuwa siye yule Subira wa awali kwani mwonekano wake ni wa kukatisha tamaa amevimba sana baada ya kutendewa unyama na binadamu wengine.

Kwa mbali anaonekana Ridhaa, akitafuna kitu fulani kinachofanana na mzizi-mwitu. Ni kina ya Daktari mzima, Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini kula mzizi!

Kaizari anaanza kusimulia yaliyojiri siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya. Anasema kuwa baada ya kutawazwa kwa kiongozi mwanamke(wengine waliamini hafai kuongoza) mambo yaliharibika. Watu wakashika silaha kUPigania uhuru wao, uhuru ambao walidai hawakupewa-

Wakaupigania. Wakatoa kauli kuwa wanaume watatumikishwa kwa walivyofanywa enzi hizo katika visakale vya jirani

GO. Waliona kuwa kiongozi mwanamke atawarudisha pale-

Walikotoka. Walikemea kusumbuliwa walikosumbuliwa kwa miongo mitatu sasa na Affirmative action na a third should be

Women. Walikerwa mno na suala la jinsia ya ki kuchipuza kila mara katika vikao vyao wakalamik' Y mwa mke

kutetewa na vyombo vya habari na wapigania haki. Mwanaharakati mmoja kwa jina la Teitei akazidi kusema kuwa mwanamke kuiongoza jamii nzima itakuwa kukivika kichwa cha kuku kilemba.

Bi. Shali alikanusha kauli ya Teitei na kusema kuwa, Mwekevu(kiongozi mwanamke) alijitosa katika siasa na kuomba kura kama wanaume hao wapinzani wake, akastahimili vitisho na matusi kutoka kwa wanaume na kwa hivyo ushindi wake ni zao la bidii yake. Mradi wake wa kuchimba visima umewafaidi raia kwenye maeneo kame.

Kaizari aliendelea kumweleza Ridhaa kuwa vita vilianza kati ya kundi lililokuwa linaunga mkono

Mwekevu na lililokuwa likiunga mkono mpinzani wake mwanamume. Vita vikacha-

Cha baina ya pande zote mbili. Kundi pinzani likidai kuwa haiwezekani mwanamke kushinda uchaguzi huenda aliiba kura na wafuasi wake kuwanunua wanawake ambao ndio wapiga kura wengi. Kundi la mwekevu lilisikika likisema kuwa wakati wa mabadiliko ni sasa na kuwa wanastahili kumpa Mwekevu nafasi. Mijadala iliyozuka ilizidisha migogoro na hali ya taharuki ikatamalaki. Askari wakatumiwa kudumisha usalama katika vijiji na mitaa. Muda si muda raia walianza kukimbizana na polisi. Katika mchezo huu, watu wengi walipoteza maisha yao.

Wengine walipoona kuwa mambo yameharibika waliacha makwao na kukimbia. Mali walioacha nyuma yaliteketezwa.

Wakapoteza kila kitu. Wengine waliokuwa jasiri walipora maduka ya Kihindi, kiarabu na hata Waafrika wenzao wakapora walichoweza kubeba kabla ya kupatana na mkono wa utawala.

Sura ya nchi ya Wahafidhina ikawa mpya. Misafara ya wakimbizi ikawa kwenye barabara na vichochoro vya Wahafidhina.

Mizoga ya watu na wanyama, magofu ya majumba yaliyoteketezwa kwa moto na uharibifu wa mali na mazingira ukashamiri.

Kaizari anakumbuka siku ya pili akiwa sebuleni na wanawe wakitazama runinga mara alisikia kuwa hakuna amani bila kuheshimu mwanamume. Kilichofuatia ni mabarobaro waliobeba picha za mpinzani aliyeshindwa na Mwekevu na wakaanza kughani mkarara uliokuwa ukisema Tawala Wahafidhina tawala, Mwanzi wetu tawala Wahafidhina tawala.

Mara hali ilibadilika na wakayazingira magari barabarani na kuanza kuyawasha moto kana kwamba wanayachoma mabiwi ya taka! Vikasikika vilio vya binadamu akiomba kuhurumiwa na binadamu kaini, lakini vilio havikusikika.

Magari yakawa yanawaka moto bila kujali binadamu waliokuwamo ndani.

Mmoja wa waliokuwa wakitekeleza unyama alisikika akiwaambia wapinzani wao wanyamaze kwani wao ndio wamekuwa wakiwarudisha nyuma miaka yote hiyo kwa kuhadaiwa na Vishahada hivyo wanavyopewa vyuoni. Alilalama kuwa wanafunzwa kukariri nadharia bila kuwazia umilisi na stadi za kuwawezesha kujitegemea. Mtu ana digrii tatu na hata baada ya miaka kumi kazi hana.

Vijana waliendelea kulamikia kupuuzwa kwao. Mate yame-

Wakauka vinywani wakifunga barua za kutumia maombi ya

Baadaye ving'ora vilisikika na askari wanaojulikana kama fanya fujo uone wakawa wanawinda vijana hawa. Walimiminiwa risasi vifuani mwao na wote wakaiaga dunia kifo cha kishujaa kwani walijitolea mhanga kupigania uhuru wa tatu. Kaizari alitokwa na machozi na kuwahurumia vijana hawa waliokufa kifo walichoweza kukiepuka. Akaihurumia nchi yake ambayo ilielekea kushindwa kuwahakikishia usalama watu wake. Baada ya siku nne kwa kina Kaizari kulibishwa hodi, mke wake Kaizari, Subira ndiye alikwenda kuufungua, alisalimiwa kwa kofi kubwa kisha akaulizwa alikokuwa kidume chake kijoga. Walisemekana kuwa wao ndio vikaragosi waliotumiwa na wasaliti wao kuendelea kuwafukarisha.

Alikatwa mikato miwili ya Sime hata kabla hajajibu lolote, akazirai kwa uchungu. Kisha genge la mabarobaro watano likawabaka mabinti wake Kaizari, Lime na Mwanaheri. Alijaribu kuwaokoa lakini hakufaulu. Mahasimu hao wakaondoka baada ya kuutekeleza unyama huo bila kumgusa Kaizari, auguze majeraha ya moyo. Alijizatiti na kuwapa wanawe na mke wake huduma ya kwanza. Punde si punde, sauti ya

Jirani yao Tulia iliita ikiwataka kutoka iwapo walitaka kuishi.

Tofauti na majirani wengine, Tulia alimsaidia Kaizari kufunganya na kumsindikiza hadi njia panda. Alimkumbatia na kumwambia kuwa mwenyezi mungu ndiye hupanga na nguvu na mamlaka pia hutoka kwake. Akamjuvya kuwa uongozi mpya umezua uhasama kati ya koo ambazo Zimeishi kwa amani kwa karibu karne moja. Akamshauri aihamishe aila yake kwa muda kwa sababu ya usalama. Akamhakikishia kuwa huo sio mwisho wa kuonana. Huu utakuwa mwanzo wa uzao wa jamii mpya isiyojua mipaka ya kitabaka, jinsia na kikabila. Jirani alipompungia mkono, matwana ya abiria ilikuja nao wakaabiri. Ilikuwa ikiendeshwa kwa kasi kana kwa

inakimbizwa. Waliyashuhudia mengi katika safari hii ya shaka kama vile mabasi kuchomwa pamoja na shehena zayo na hata mifyatuko ya risasi. Hatimaye, gari lilikwisha petroli ikawa sasa ni mtu na malaika wake. Walijitoma msituni, kila mtu na aila yake. Walipata shida kwani chakula kilikuwa adimu.

Kulikuwa na changamoto ya maji safi ya kunywa. Walikata miti wakajenga vijumba ambavyo viliezekwa kwa nyasi na kukandikwa kwa udongo. Wengi walipata homa ya matumbo na wengine kuyapoteza maisha yao. Wakimbizi walizidi kuongezeka nayo hali ya maisha ikazidi kuwa ngumu. Idadi kubwa ya wakimbizi ilifanya kuwe na vyoo vya kupeperushwa- yaani sandarusi ambazo hutumiwa kama misalani. Siku za mwanzomwanzo Kaizari hakuweza kutumia misala hii, lakini alisalimu amri na kusema potelea mbali, lisilo budi hutendwa. Lakini kutokana na tishio Ia maenezi ya kipindupindu aliwasihi kuchimba misala kwa jina long drop. Tatizo la njaa pia lilishamiri kwani waliokuwa wamebahatika kubeba nafaka chache walizitoa zikatumiwa na wote, zikaisha. Njaa ikawa inatishia kuwaangamiza wote, lazima wafanye jambo.

Asubuhi ya siku ya kumi na tano Selume(mke wa jirani yao aliyekuwa mpinzani mkuu wa Mwekevu) alipitia kwenye kibanda cha Ndugu Kaizari. Selume alikuja kuwaeleza kuwa alikuwa amesikia fununu kuwa upo mradi wa kuwakwamua

Wakimbizi kutokana na hali hii. Shirika la Makazi Bora, lilikuwa limejitolea kuja kuwajengea wakimbizi nyumba bora.

Misikiti na makanisa yalikuwa yalikuwa yamekusanya vyakula ili kuwalisha wahasiliwa. Watu walijawa na matumaini. Siku ya ishirini lori kubwa liliingia na watu wakakimbilia chakula kama watoto wafanyavyo. Watu waligawiwa chakula na

akina mama( wa Mother's union, woman's Guild na waliokuwa wamepakiwa nyuma ya lori hilo. Msukumano ulianza hadi mlinda usalama mmoja alipojitokeza na kuwasihi kuweka usalama. Watu wengine kama Mzee Kaumu walishangaa walipokuwa hawa wangwana wakati madhila haya yalipowapata.

Kwa kuwa tabia ni ngozi, Bwana Waziri Mstaafu aliyekuwa na uzoefu wa kuwaelekeza watu huko wizarani, alisaidia kukigawa chakula. Pia Kaizari na Selume waliitwa kusaidia. Hata hivyo, wengine walitumia ulaghai ( kama familia ya Bwana

Kute- diwani wa hapo awali) kupata chakula kingi kuliko familia zingine.

**Maswaii**.

*i) Maisha kotika mitaa ya mabanda ni kukatisha tamaa. Tetea kauli hii.*

*ii) Fafanua matatizo wanayoyapitia wakimbizi wa ndani kwa ndani.*

*iii) Faha!i wawii wakipigana, nyasi huumia. Kwa kurejele sura hii, onyesho ukwei wa kauli hii.*

*iv) Siasa husababisha migogoro katika ndoa. Kwa kurejelea sura hii, tetea kauli hii kikamilifu.*

**SURA YA TATU**

Baada ya kuishi katika msitu wa Mamba kwa miezi sita, Ridhaa, Kaizari na familia yake walibahatika kurudi nyumbani kufuatia mradi wa Operesheni Rudi Kanaani. Asubuhi hii

Ridhaa ameketi katika chumba cha mapokezi katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Rubia. Ana hamu kuu ya kumwona Mwangeka akiwa mzima. Ridhaa anakumbuka kuwa siku ya kuhawilishwa kutoka Msitu wa Mamba hakuwa na matumaini ya maisha bora kwani hakuwa na mwenzi wala mtoto wa kuendea. Wengine kama Selume walikuwa wakilia kwa kuwa hawakujua waende wapi kwani mme wake amekwisha kuoa msichana wa kikwao na Babake alimkatalia katakata. Ridhaa alimfariji na kumwomba asilie kwani mwana wake yu hai tena ana kisomo na amehitimu kama mkunga, anaweza kujitegemea. Ndipo Ridhaa akamwahidi warudipo nyumbani, angemtambulisha Selume kwa mkuu wa Idara ya Afya ya Jamii katika Hospitali Kuu ya Tumaini. Leo hii, Ridhaa anapowaza haya, Selume amekwisha kuajiriwa kama muuguzi katika hospitali ndogo iliyojengwa karibu na kambi ya

WWHN.

Ridhaa anakumbuka mambo mengi kama vile kadhia iliyompoka familia yake ndiyo ilimkutanisha na watu kama Selume arnbao angewaita ndugu na kumfanya kusahau msiba wa kUipoteza akraba yake. Kutangamana na wakimbizi kukamfunza thamani ya binadamu. Sasa amejifunza mengi kama

Vile uzima ni upande mwengine wa mauti.

Kwenye Msitu wa Mamba, Ridhaa alipata huduma za ushauri na uelekezaji kutoka kwa wataalamu mbalimbali na akaweza ugonjwa wa shinikizo la darnu ambao ulitokanana

mshtuko wa kupoteza jamaa yake na mali yake dafrao moja.

Hapo alipotoka kwenye msitu alijihisi kiumbe kipya kwani wapwa zake- Lime na Mwanaheri walikuwa wamepata matibabu. Dada yake Subira alitibiwa akapona. Mwamu wake

Kaizari- amepona donda lilitokana na kuwaona binti zake wakibakwa. Ridhaa anamwona Kaizari ni afadhali kwani heri nusu Shari kuliko Shari kamili.

Asubuhi hii, Ridhaa akiendelea kumngojea Mwangeka hakuweza kusahau jinsi alivyohisi aliporudi tena kwenye ganjo lake siku ile. Anakumbuka kuwa alipozinduka(kutoka kuzirai), alijipata katikati mwa kiunzi cha sebule lililokuwa kasri lake. Eneo hili ndipo wanawe Tila na Mwangeka walipokuwa wadogo walipenda kumkimbilia kila mara alipotoka kwenye shughuli zake za kikazi. Hapo ndipo kijukuu chake kilipozoea kutembea tata na kumwita "bubu" naye alipenda kukirekebisha na kukiambia "sema babuu". Hayo yote hayapo sasa, hata zile pambaja za mkewe Terry na utani wake hamna.

Akiwa yu pale katika kumbukumbu zake, polepole kwenye jukwaa la akili yake kunaanza kuigizwa mchezo wa maisha yake kabla ya dhiki iliyomfika. Anamwona Tila akitoka shuleni na kuuweka mkoba wake juu ya meza. Katika mazung-

Umzo yao inabainika kuwa Tila ana upevu wa mawazo. Waliishi kujadiliana na Mwanawe Tila masuala nyeti kana kwamba walikuwa marika. Tila alijua kuwa Siku moja atakuwa jaji katika mahakama kuu na kuusafisha uozo uliotamalaki humo.

Alitamani kuwaonjesha washukiwa waliowekwa rumande kwa miaka mingi utamu wa haki. Lakini sasa Tila hayupo tena, kilichObaki ni kumbukumbu zake.

Ridhaa aliona kuwa utabiri wa mwalimu wa la mabadi

liko' ulikuja kutimia kwani viongozi wa awamu ya awali walibwagwa chini na vijana chipukizi. Kinaya ni kuwa wengi walishindwa kabisa kukubali kushindwa hasa yule aliyekuwa akigombea kilelecha cha uongozi. Kulingana naye nafasi hii iliumbiwa mwanamume na kumpa mwanamke ni maonevu yasiyovumilika. Kiongozi huyu alipita kila mahali akitoa kauli ambazo ziliwajaza hamasa wafuasi wake nao wakaanza fujo zilizoangamiza juhudi za miaka hamsini za raia za kuijenga jamii yao. Hatimaye ndege kwa jina PANAMA 79 iliyotarajiwa kufika saa tatu unusu sasa ndio inalikanyaga sakafu. Abiria waliposhuka, Ridhaa na Mwangeka walitazamana kimya.

Ridhaa alihisi kana kwamba anauona mzuka wa Mwangeka, hakuamini kuwa angerudi nyumbani akiwa hai. Hatimaye baada ya shaka kumwondokea, alimkumbatia mwanawe.

Mwangeka akajitupa kifuani mwa babake kwa furaha. Ridhaa alimkaribisha Mwangeka nyumbani na kumtaarifu kuwa hakujua kuwa watawahi kukutana akiwa hai. Ridhaa akamjuwa mwanawe yaliyoisibu familia yao. Mwangeka alipomtazama babake akaona kuwa amekonga zaidi na sasa ameshabihi mno babu Mwimo. Baada ya kumbukumbu zake kumkumbusha ya awali Mwangeka alimshukuru babake na kumweleza kuwa alipoipata habari ya machafuko ya baada ya kutawazwa kwa kiongozi, alijawa na kihoro kisicho kifani. Mwangeka amekuwa akifuatilia matukio kwa makini kwani hata kura zilipohesabiwa upya kiSha mpinzani wa Mwekevu kukubali kushindwa na kutoa wito kwa raia kusahau yaliyopita, alijua kuwa nchi imepiga hatua moja katika safari ndefu ya kupata afueni kutokana na tufani za baada ya kutawazwa. Mwangeka aliendelea kuwapa heko vijana wenzake kwa kugundua kuwa wanatumiwa vibaya na viongozi wenye tama. Mwangeka akawa sasa anakubaliana na usemi wa Tila kuwa "usi

cheze na vijana, wao ni kama nanga. Huweza kuizamisha marikebu " Japo Ridhaa aliyaitikia maneno ya Mwangeka kwa mgoto, alijua kuwa palikuwa na kazi ngumu ya kujenga upya ukuta ambao ufaa wake ulikuwa umepuuzwa. Akawa akawa anakubaliana na sera ya bintiye marehemu, Tila kuwa

Vijana wanafaa kuelimishwa zaidi kuhusu amani kwani ndio wengi na ndio mhimili wa jamii yoyote ile. Hatimaye, Ridhaa alishusha pumzi na kumkabidhi mkono mwanawe na kumtaka waende ili akajipumzishe kutokan na adha za anga.

Mengine watazungumza baadaye.

*i)Fafanua sifa na umuhimu wa Ridhaa.*

*ii)Mwandishi ametumia mbinu rejeshi katika kuuwasilisha ujumbe wake. Onyesha narnno alivyotumia mbinu hii, iii)Fafanua sifa nq umuhirnw wa tTiIa kama zinavyjitQkeza katika surg hit, tiv)Ni masaibu gani Wdhafidhing waliyapitia? Tajmmatan.*

*v)Ni nini umuhimu wa Mwangeka? Rejelea sura hii.*

**SURA YA NNE**

Mwangeka ameketi mkabala mwa kidimbwi cha kuogelea nje ya jumba lake la kifahari ambalo yeye aliliona kama makavazi ya kumtonesha donda lililosababishwa na kifo cha mke wake

Lily Nyamvula. Siku ile baada ya kutoka kwenye uwanja wa ndege walifulul iza moja kwa moja hadi kwenye gofu la baba yake Ridhaa. Majivu yaliyokuwa mabaki ya kilichokIJWa kwenye kasri lile yalibaki pale pale. Majivu hayo miili ya mama yake(Terry), wanuna wake, mkewe na mtoto wake.

Mwangeka hakuelewa ni kwa nini babake hakuyaondoa mabaki hayo na ni kwa nini hakushirikiana na majirani kuchimba kaburi (mass grave) kuyazika majivu hayo. Baba mtu alimkazia tu macho. Machozi mazito ya machozi yalitunga machoni mwa Mwangeka, akayaacha yamcharaze yatakavyo. Wakati huu hata nyanya yake angekuwapo kumwonya dhidi ya kulia kama msichana angempuuza. Alihitaji kulia ili kuliondoa komango ambalo lilikuwa limefunga mishipa ya

moyo wake. Alipolia, moyo wake ulilainika na moyo wake sasa ulijaa utulivu. Mwangeka akakumbuka methali isemayo wino wa Mungu haufutiki. Hata hivyo alizidi kujjuliza iwapo binadamu aliandikiwa kumpoka binadamu mwenzake uhai.

Siku ile baada ya wao kutoka kwenye uwanja wa ndege, Ridhaa alimwelezea Mwangeka mambo yalivyojiri. Alimweleza kuwa maisha yalibadilika Pindi tu Mwangeka alipoondoka. Waliandamwa na msiba baada ya mwingine. Mwanzo, Ridhaa akapoteza majumba yake mawili. Miezi mitatu baadaye ami yake Mwangeka aliyeitwa Makaa alichomeka asibakie chochote alipokuwa aakiwaokoa watu ambao walikuwa wakipora mafuta kutoka kwenye lori lililokuwa limebingiria. Makaa alizikwa pamoja na mabaki ya wahasiriwa wote katika kaburi moja kwani serikali iliwatayarishia mazishi ya umma. Baada ya Ridhaa kushusha pumzi, aliendelea kum-

Weleza Mwangeka kuwa mambo hayo yote aliyakabili kwa msaada wa wanuna wa Mwangeka, mamake Mwangeka na rnkaza mwanawe. Akaanza kuyajenga upya maisha yake hadi

Siku ile ambayo aliitazama familia nzima ikimponyoka. Daktari Ridhaa amewaokoa wagonjwa wengi kutokana na magonjwa sugu lakini alishindwa kuuzima moto uliokuwa ukiiteketeza nyumba yao. Lakini, hakushindwa kwani hakuwepo



tendo lenyewe likitendeka. Alikuwa ameenda kumfanyia ma jeruhi mmoja upasuaji. Ridhaa alipokuwa akirejea nyumban akasikia sauti ya kite ya mamake Mwangeka, kisha mlipukc mkali. Yote yakaisha. Hadi hapo, ameyaishi maisha ya kinyama kupigania chakula na wahitaji wenzake. Ameonja shubiri ya kuwa mtegemezi kihali na mali. Lakini katika hayo yote amejifunza thamani ya maisha, udugu na amani. Alimhurumia Mwangeka ambaye mkasa huo ulimfanya mjane hata kabla ya ubwabwa wa Shingo kumtoka.

Baada ya kurejea kwake Mwangeka hakuishi na babake kwa muda mrefu. Mwanzo, hakuweza kustahimili uchungu uliosababishwa na kuamka kila asubuhi kutazama mahali ilipoangamia aila yake. Alimrai babake kila siku akibomoe kiunzi kile cha nyumba lakini babake alikataa katakata. Lilikuwa kaburi la ukumbusho wa familia yake. Sababu ya pili ni kuwa lazima

Mwangeka angeyaanza maisha yake upya. Atafute ushauri kutoka kwa wataalamu, auguzie moyo wake mbali na babake.

Mwangeka aliporejelea shughuli zake za kawaida kazini alitafuta kiwaja cha kujengea nyumba. Babake akamtahadharisha kufanya uchunguzi kabla ya kuanza ujenzi wenyewe. Baada ya Mwangeka kuhakikisha uhalali wa stakabadhi hii na ite alipata kipande cha ardhi karibu na ufuo wa bahari. Kazi ya ujenzi ilianza na baada takriban mwaka mmoja na nusu akahamia kwake.

Hata anapokitazama kidimbwi hiki, mawazo yake yakO mbali alikoanza maisha. Anazikumbuka changamoto za ukLji wake. Anawakumbuka wanuna wake: Kombe, Mukeli na



Annatna(Tila). Anapomkumbuka Tila anatabasamu kisha tone moto la chozi linamdondoka. Kumbukumbu ya Annatila inavuta taswira ya mnuna wake mkembe aliyefariki dunia akiwa na umri wa miaka sita wakati ule Mwangeka akiwa na umri wa miaka kumi na miwili tanzia ile ilipowafika. Katika jamii ya Mwangeka, kifo kilifuatwa na viviga vya aina mbalimbali yakiwemo maombolezi. Basi baada ya kifo cha mtoto huyo majirani walikuja kuifariji familia ya Bwana Ridhaa. Wiki mbili baada ya mazishi ya ndugu yake, Jumamosi moja

Mwangeka alimpata Tila na wenzake nyuma ya nyumba wakimngojea. Tila alimvuta na kumnong'oneza kitu sikioni kisha akavuta boksi lililokuwa limetiwa mwanasesere wao kwa jina Dedan Kimathi lakabu waliokuwa wamempa

marehemu ndugu yao-Dede. Walianza kulia na kuomboleza kifo cha Dedan Kimathi. Wakaimba mbolezi. Katika hali ile ya kuomboleza, watoto hawa hawakujua kuwa baba yao alikwisha kuja dakika thelathini zilizokwisha. Akawa anawatazama watoto hawa wakiigiza mazishi ya ndugu yao Dede.

Alibanwa na hasira na kuutwa mshipi wake kutoka kiunoni, akamshika Mwangeka na kumwadhibu vikali. Akamkemea

Mwangeka kwa kuwa bendera inayofuata upepo badala ya kuwa kielelezo bora kwa mnuna wake Tila. Mwangeka anapokumbuka kisa hiki anajutia ni kwa nini hakukiomboleza kifo cha Tila.

Baada ya kipigo hiki, Mwangeka aliwajibika zaidi akayavalia masomo yake njuga hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. Hapo ndipo alipokutana na mke wake Lily Nyamvula. Nyamvula alikuwa akisomea uanasheria. Mwangeka alihitimu masomo yake na kujiunga na kikosi cha wanamaji, jambo hili liliwashangaza wengi.

**Zoezi**.

*i)Eleza kwa muhtasari mambo yalivyokuwa Mwangeka aliporudi nyumbani.*

*ii) Ni kwa nini Mwangeka alimwona Ridhaa(babake kama)*

*mwehu?*

*iii) Eleza misiba aliyomwandarna Ridha kama iivyoonyeshwa katika sura hii.*

*iv) Jadili maudhui ya koma yaivyoangaziwo katika sura hii.*

*v)Eeza sifa nne za Tila.*

*vi)'Kama ningeusikiliza ushauri wa Tausi wangu labda ningeweza kuiokoa aila hii '*

*a. Eleza muktadha wa dondoo hili.*

*b. Eleza kwa kifupi jambo ambalo aila ya msemaji ilikumbana nalo.*

*c. Eleza sifa na umuhimu wa anayeitwa 'Tausi wangu'*

*v)Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika sura hii*

**SURA YA TANO**

Msitu wa Mamba uligeuka kuwa nyumbani kwa maelfu ya watu waliogura makwao bila tumaini la kurudi. Walijipa moyo na kusema kuwa hata walikokuwa wakiishi hakukuwa kwao, walikuwa maskwota*. Wakaamua kula asali na kuyanywa maziwa ya Kanaani hii mpya isiyokuwa na mwenyewe. Matokeo ya maamuzi haya yalikuwa nWd

kukatwa kwa miti kwa ajili ya kupata mashamba ya kupandia vyakula na kwa ajili ya ujenzi. Kabla ya miaka miwili kuisha, pahali hapa palikuwa pamepata sura mpya- majumba yenye mapaa ya vigae, misitu ya mahindi na maharage, maduka ya jumla, viduka vya rejareja kila mmoja akijibidiisha kufidia kile alikuwa amepoteza.

Familia ya Bwana Kangata ilikuwa miongoni mwa zile zilizoselelea(zilizoishi) kwenye msitu huu. Kwa Kangata na mkewe Ndarine hapa palikuwa afadhali. Awali wakiwa wamelowea katika shamba Ia mwajiri wao aliyekuwa akiishi jijini. Waliishi pale kwa muda mrefu hata watu wakadhani kuwa ilikuwa milki yao. Wengine wakidhani Kangata na familia yake walikuwa akraba ya mwajiri wao. Hata wana wa Kangata walipokwenda shuleni walijisajilisha kwa jina Ia tajiri wa baba yao. Walikuwa wakiitwa Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na

Akelo Kiriri. Kiriri likiwa jina Ia Mwajiri wa Kangata. Kangata na mwajiri wake walikuwa wamesekuliwa kutoka mtaa wa

Matunda katika zile patashika za baada ya kutawazwa. Kiriri aliiaga dunia muda mfupi kutokana na kihoro cha kufilisika na ukiwa aliokuwa ameachiwa na mkewe Annette na wanawe.

Walipata Green Card na kuhamia ughaibuni. Hivyo basi, juhucii za Kiriri kumshawishi mkewe asimnyime ushirika wa

Wanawe ziljangukia rnoyo wa Firauni. Mkewe Kiriri alikuwa



ashaamua kuwa hapa hapamweki tena. Kazi aliyokuwa akiifanya katika afisi za umma kama mhazili mwandamizi kwa miaka mingi ilikuwa inamfanya kusinyaa, akawa hana hamau akahisi kinyaa. Wanawe walipoenda kusomea Ng'ambo - wafanyavyo wana wa viongozi kwa kuwa wanaiona elimu ya humu kama isiyowahakikishia mustakabali mwema raia wake, yeye alistaafu mapema na kuchukua kibunda cha mkupuo mmoja almaarufu Golden Handshake akachukua

Green Card na kuwafuata na kumwacha mume wake akiwa mpweke. Baada ya wana wa Kiriri kumaliza masomo yao walibakia huko huko Uzunguni kufanya kazi. Walipuuza rai baba mtu za kurudi nyumbani ili kuziendesha baadhi ya biashara zake. Kila mmoja akajishughulisha na mambo yake. Kifungua mimba wa Kiriri kwa jina Songoa alisema kuwa nchi yao haina chochote kumfaa kwa hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mshahara mdogo sana, akaona heri awekeze huko mbali aliko na imani nako. Kabla ya kifo chake, Kiriri alikuwa akiibua mijadala nafsi akilini mwake kuhusu Waafrika ambao ni kama waachao mbachao kwa mswala upitao. Akawa anajiuliza maswali mengi kama vile ni nini huwavutia raia kuhamia ughaibuni?

Je ni hiyo mishahara minono wanayolipwa? Je, ni hizo kazi za kujidhalilisha za kwenda kuwauguza maajuza waliotelekezwa na aila zao? Au ni zile ndoa kati ya vijana wakembe wa Kiafrika na vikongwe vilivyochungulia kaburi? Kiriri aliendelea kushangaa ikiwa mkewe amegeuka wale wake pindi wafikapo ng'ambo hufunga ndoa na waume wengine kwa kuwa ndio njia pekee ya kuufukuza upweke na kupata riziki au kwa

kuta kujikwamua kwenye tope la uhawinde?

Kutokana na uzoefu wake katika kilimo, Kangata alipofika katika Msitu wa Mamba aliweza kuendeleza kilimo chenye natija. Kwa sasa, miaka mitano imepita na Kangata na

Ndarine wameipa dunia kisogo. Lucia Kiriri-Kangata ameolewa katika ukoo wa Waombwe ambao awali walikuwa maadui sugu wa ukoo wa Anyamvua. Ndoa hii ilipata pingamizi sana kutoka kwa ukoo mzima lakini kutokana na Msimamo imara wa Kangata ndoa hii ilisimama. Watu wa ukoo wa kina Kangata walishangaa ni kwa nini mwana wao akaozwa kwa watu ambao huvaa nguo ndani nje na pia huzaa majoka ya mdimu ambayo ni machoyo kupindukia.

Kangata aliyatupilia maneno ya watu wa ukoo wao kwani

Kiriri aliyadhamini masomo ya mabinti zake hata ingawa walikuwa wa ukoo tofauti na wake. Watu wa ukoo wa Kangata walikuwa wakipinga elimu ya msichana na kutoa rai kama kumuelimisha msichana ni kufisidi raslimali. Kangata anashangaa wakati mwanawe ameneemeka na kuishi maisha ya heri ndio wakati jamaa zake wameona tofauti za kiukoo.

Hatimaye ukoo wa Kangata ulikubali muungano huu wa ndoa na ukawa umeyeyusha tofauti na chuki iliyokuwa baina yao.

Nasaba hizi mbili zikawa sasa zinapikia chungu kimoja.

Naye Akelo Kiriri-Kaango habari yake haijulikani. Baada ya kumaliza masomo yake ya kidato cha nne, alipata kuolewa na dereva wa malori yanayosafirisha bidhaa hadi Zambia. Jina la dereva huyo ni Kaango. Alipomwoa Akelo Kiriri, alimjengea nyurnba katika

gatuzi la Mbuyuni na tetesi zinasema kuwa walipata watoto wawili. Mmoja kwa jina Ngaire na mwingine

Mumbi. Hakuna ajuaye walikopelekwa na misukosuko ya miaka mitano iliyopita.

Lunga Kiriri — Kangata ndiye anaishi katika milki ya babake katika Msitu wa Mamba. Yeye amesomea kilimo. Awali alikuwa ameajiriwa kama afisa wa kilimo nyanjani. Alikuwa akiwaelimisha raia kuhusu mbinu bora za kilimo kama vile watu wasilime karibu na mito, watu wachimbe mitaro kuzuia mmonyoko wa udongo na watu wapande miti inayostahimili ukame. Alikuwa amirijeshi wa uhifadhi wa mazingira. Alipokuwa shuleni ndiye aliyekuwa mwasisi wa chama cha watunza mazingira wasio na mipaka. Kila ijumaa wakati wa gwaride ungemsikia akihutubia wanafunzi wenzake kwa mhemko.

KimondO (mwanafunzi mwenzake Lunga) alikuwa haishi kushangazwa na I-unga kwani mtu akimsikiliza Lunga hangedhani kuwa amekulia mazingira sawa na wale wanyonge ambao uwepo wao huamuliwa na matajiri. Ilishangaza kuwa Lunga hakuwazia kwamba alikolowelea baba mtu palikuwa msitu tu, tajiri wake akapabadilisha. Babake Lunga haswa ndiye aliyeliendeleza shamba lile. Aliendelea kumuuliza iwapo hajui kwamba umaskini unaweza kuupujua utu wa mtu akatenda hata asivyokusudia kutenda. I-unga hangewe za kujua kwani hajawahi kulala njaa akakosa usingizi kutOE-

na na mkato wa njaa ilhali baba mtu anavuna kahawa katika shamba kubwa la Mzungu. Mzungu huyu mwenye shamba akiwa anapata mamilioni ya pesa lakini anawapunja wafa nyakazi wake kwa kuwalipa kishahara duni kiasi cha wao kushindwa kuwanunulia wana wao sare mpya. KimondO anaendelea kumwambia mwenzake Lunga kuwa hajawahi

kilichoko ndani ya kijiji ambacho mwenye kahawa amewajengea wafanyakazi, Daktari mwafrika anakataa kukupa huduma kwa kuwa wazazi wako hawajawekewa bima kutokana na kijishahara duni wanacholipwa.

Sasa Lunga ni mkulima stadi. Ametononokea si haba katika msitu huu. Hakumbuki kuwa msitu huu unafaa kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye. Kabla ya shida kumleta hapa mstakabali wa maisha ya Lunga ulitishia kuporomoka. Alikuwa ameipoteza kazi yake ya Ukurugenzi katika kampuni ya Maghala ya Fanaka alikopinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ambayo yalikuwa yameagizwa kutoka ughaibuni. Mahindi ambayo licha ya kuwa na rangi ya njano, yalihofiwa kuwa yameharibika. Yalikotoiewa yalisemekana kuwa hatari kwa usalama hata wa panya. Lunga alipopinga uuzaji wa mahindi haya kwa raia vijisababu vilitolewa na vigogo wenye shehena za mahindi haya. Walidai kuyakataa mahindi haya ni kama kuidhinisha kifo cha mamilioni ya raia ambao hawamudu kujinunulia hata kibababa cha unga. Hata hivyo, rai za wakubwa ziliambulia patupu kwani Lunga alikataa katakata.

Lunga akawa amehiari kupoteza kazi yake ili kuyaokoa maisha ya wanyonge wasio na hatia. Baada ya mwezi mmoja

I-unga akiwa ofisini mwake alitumia barua ya kumstaafisha kwani shirika hili lilikubwa na changamoto ya kifedha na hivyo halmashauri ikachukua hatua ya kupunguza idadi ya wafanyakazi. Lunga alipoisoma barua hii mara mbili alishangazwa na ukosefu wa fadhila wa waajiri wake. Kweli asante ya punda ni mateke.

Lunga alipokuja katika Msitu wa Mamba alikuwa na azma ya



kuamka asubuhi huku anakeng'etwa na tumbo na homa ya matumbo inamwandama. Mwalimu anapokupa barua ili ukatibiwe kwenye kituo cha afya

kumhamisha babake na kuwachia wanyama Edeni pao lakini aliyoazimia siyo aliyotenda. Lunga alipokutana na ekari thelathini na tano za mahindi aliingiwa na tamaa na uchu akausaliti uadilifu wake.

Tamaa ya kulima maekari na maekari zaidi ikamkumbatia akakata miti zaidi. Alipoulizwa ilipofia jadhba ya kupigania uhifadhi wa misitu alisema mungu mwenyewe alitupa ulimwengu tuutawale, sio ututawale.

Siku zilivyosonga, mashamba ya Lunga na wenzake yakendelea kutoa mazao mengi nayo jamii ya Msitu wa Mamba ikazidi kupanuka nazo tofauti za kitabaka zikazidi kujionyesha. Kundi

Ia kwanza la wakimbizi Ridhaa, Kaizari na Kangata hamkuwa na tofauti kubwa. Mpito wa wakati ukazaa matajiri kama

Lunga ambaye alikuwa akiwakumbusha wenzake kuwa alitO-

kana na jadi ya kifahari ya Kiriri. Kulikuwa pia na maskini ambao kupata kwao kulitegemea utashi wa matajiri. Polepole uhasama ulianza kutishia kuisambaratisha jamii ya Msitu wa

Mamba.

Vlongozi nao kwa kuhofia mambo kuharibika, walianza kampeni za kuwaelimisha raia kuhusu umuhimu wa kuishi kwa amani licha ya tofauti zao za kiusuli. Hata hivyo juhudi hazikufua dafu kwani awamu ya kwanza ya vita vya wenyewe kwa wenyewe ilianza. Walinda usalama walipokuja kudumisha amani, walitumia bunduki zao na kuwaacha wengi wakiwa wafu nao watoto wakabaki wanawakiwa.

Kisa hiki kiliwafungua macho viongozi wakatambua kuwa wakazi hawa walikuwa wakiishi hapa kiharamu. Vyombo vya habari vikatoa wito kwa chama tawala kuwatafutia mahali kwingi, vidonda vya zamani vikanza kutoja damu. Juhudi zao za kuandama ya uamuzi wa kuhamiShwa kwao hazikufua

dafu. Wachache walifanikiwa kurudi kwao katika awamu ya pili ya Operesheni Rudi Kanaani. Wengine kama Lunga ambaye hakujua kitovu chake hasa walitimuliwa pamoja na familia zao. Baada ya miezi mitatu Lunga aligundua kuwa amerudishwa kwenye Mlima wa Simba ambako inaaminiwa mababu zake walikuwa wamehamia kutoka Kaoleni, siku za biashara ya watumwa. Msitu wa Mamba ulibaki tasa. Mto uliokuwa hapo karibu, ambao ulikuwa umeanza kukauka sasa ulianza kutiririsha maji. Jambo la kushangaza ni kwamba, hata baada ya tangazo kutolewa kuwa msitu huu ni marufuku kwa binadamu, usiku wa manane kulisikika milio ya malori na matrekta yakibeba shehena za mbao, makaa na mahindi.

Moshi pia hufuka mle mara kwa mara.

*Maswali i)Eleza sifa za wahusika hawa: (alama 10)*

*a. Lunga b. Kimondo c. Kangota kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika "*

*a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)*

*b. Eleza namna msemaji alivyoukata mkono aliostahili kuubusu (a!ama 6)*

*C. Fafanua mambo mawili yaliyotnfika msemaji (alama 2)*

*I d. Tajo tamathali mbili za usemi ziizotumika katika dondoo*

*37*

*Uj. TaTa7na e. Eleza kwa kifupi namna msemaji alivyobadilika baada ya "yali_*

*yomfika kumfika " (glama 6)*

*za kitabaka huzaa uhasama " Tetea kauli hii kwa*

*Kurejelea sura hii (alama 20)*

*iv) Fafanua matatizo wanayoyapitia vibarua na familia zao (ala.*

*ma 20)*

*v) Mashirika mengiya kiserikali huendeleza uozo. Tetea kauli hii kwa kurejelea matukio katika sura hii (olama 20)*

**SURA YA SITA**

Sura hii inapoanza tunampata Mwalimu Dhahabu akimtaka

Umulkheri kuyarudisha mawazo yake darasani. MwalifflU huyu kwa kawaida ni mcheshi. Umu(ufupi wa Umulkheri) aliyarudisha macho yake darasani yakatazamana na ya

Mwalimu Dhahabu bila yeye Umu kumwona mwalimU mwenyewe. Tangu Umu kujiunga na Shule hii katika kidato cha pili anajihisi kama samaki aliyetiwa kwenye dema. Haya mazingira ni mageni kwake na hakuja hapa kwa hiari. Baridi ya mahali hapa inamsinya kwani si kama kwao ambako kulikuwa na hari*. Ukweli ni kuwa Umu alikuwa na kwao ila sag hana. Amebaki kuishi kwa hisani ya mkuu wa Shule ya gamano aliyeshauriwa na Wizara ya Elimu kumsajili umu na wengine watano. Umu ni mwana wa pili wa Bwana Lunga

Kiriri —Kangata. Uongozi ulipoamua kuwahamisha hadi Mlirna



wa Simba, IJmu alikuwa ndio anajiunga na kidato cha kwanza. Kule kuhamia Mlima wa Simba hakukumkalia vyema

Lunga. Aliona kuwa alikuwa ameyapoteza maisha yake pamoja na ndugu na marafiki zake. Wanawe walikuwa wakisomea katika Shule za kifahari na sasa fidia aliyopewa na serikali haitoshi hata kuwapeleka wanawe katika Shule za watu wa kima wastani.

Lunga alipohamia Mlima wa Simba mke wake Naomi naye hakuwekwa na mazingira haya mapya. Asubuhi moja alimtumia Lunga ujumbe na kumtaarifu kuwa ameondoka ili akatambe na ulimwengu na huenda

akaambulia Cha kumsaidia Lunga kuikimu familia. Akawaacha Lunga na wanawe.

Pigo hili la tatu lilimuuma I-unga sana kwani alijisabilia kwa hali na mali kumpendeza mkewe. Naomi alilipa penzi lake na kumwachia Lunga adha za malezi jambo ambalo Lunga hakustahimili. Mwaka mmoja wa kwanza ulimwia Lunga mgumu mno kwani ilimlazimu Lunga kuwa mama na baba wa watoto wake. Katika hali hii I-unga aliingiwa na wahka na kihoro na hatimaye ugonjwa wa shinikizo Ia damu ukampata. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake na mikononi mwa kijakaziwao.

Asubuhi moja IJmu aliamka na kujipata yu pweke nyumbani mwao. Ndugu zake wawili, Dick na Mwaliko walikuwa wametoweka. IJmu alijaribu kumwita kijakazi Sauna kumjuza lakini alisalimiwa na cheko la mwangwi wa sauti yake katika sebule.

umu alimaka, hajui awafuate wapi ndugu zake wakembe.

Dick alikuwa darasa la saba naye mwaliko alikuwa katika darasa Ia kwanza. Picha ya watoto waliotekwa nyara ilimjia

Umu akilini mwake ikakifanya kichwa chake kumwanga kwa



maumivu. Mwishowe alipiga ripoti katika kituo cha polisi alikoulizwa maswali mengi kuhusiana na kukosekana kwa ndugU zake. Baada ya kuripoti habari hiyo IJmu alijizoaoa na kujiendea zake nyumbani. Maisha ya Umu sasa yalichukua mkond0

mpya. Siku ile baada ya kuwapigia polisi ripoti, ilibainika wanuna wake walikuwa wametekwa nyara na Sauna kwani hayo ndiyo yalikuwa mazoea ya Sauna. Sauna alikuwa akijifanya mwema kwa waajiri wake ili aaminiwe ili naye apate fursa ya kuwaiba watoto na kuwapeleka kwa bibi mmoja ambaye

aliwatumia katika biashara zake na katika ulanguzi wa dawa za kulevya.

Machozi ya uchungu yalimtiririka Umu na hakuamini kuwa nduguze wadogo walikuwa mali ya mtu atakayewatumia kama kitega uchumi. Baada ya kutia na kutoa, aliona kuwa hapo hapamweki tena akaamua kuondoka. Asubuhi moja

Umu alifika kwenye kituo cha garimoshi. Sasa yu katikati mwa jiji la Karaha. Woga mkubwa ukamkumbatia kwa kutojua alikokuwa kwani mji huu ni mpya kwake. Hajawahi kutembea hapa peke yake. Hata hivyo, IJmu yu tayari kuanza maisha upya katika jiji hili. Hajui vipi lakini penye nia ipo njia.

Baada ya kuwaza na kuwazua, IJmu alijikokota na kuchukua njia iliyoelekea kushoto. Alipofika Church Road mara moja aliikumbuka njia hii. Aliwahi kupitia pale zama za utukufu wa babake. Anakumbuka akiwapata ombaomba wengi karibu na kanisa Ia Mtakatifu Fatma. Anakumbuka namna alivyomsihi mamake kumpa noti ya shilingi mia moja ili amkabidhi mmoja wa ombaomba wale. Mama mtu alikatalia ombi Ia Umu lakjnl hatimaye baada ya Umu kusisitiza mno, mamake alimkabidhi shilingi ishirini naye umu akaongeza mapeni aliyokuwa akipewa na babake na kumkabidhi ombaomba mmoja shilingi



mia m ili. Ombaomba huyo alimshukuru na kumwita sistee na kuahidi kuwa siku moja atamsaidia Umu. Leo hii Umu anashangaa iwapo bahati itamvutia usaidizi hata kutoka kwa yule maskini wa Mungu. Akipewa msaada wowote hata kama ni jamvi la kuuweka ubavu wake usiku kwenye mitaa atashukuru. Alielekea kwenye mkahawa mkubwa mkabala mwa kanisa. Aliwaona vijana wengi wa mitaani. Umu akayaangaza macho yake kuona kama atampata rafiki yake.

Hakumpata wala hakuona yule aliyekaribiana naye. Alikataa tamaa. Aliamua kuendelea na safari yake, huenda atampata kanisani. Kisadfa, kabla hajatembea hatua chache kutoka pale aliskia sauti ikiita "kipusa". Alipogeuka alimwona yule kijana kazaliwa upya! Nadhifu! Meno meupe! Alijitambulisha kwake

Umu kama Hazina. Serikali ilimwokoa kutokana na kinamasi cha uvutaji gundi na matumizi ya mihadarati. Akapelekwa shuleni akasoma. Walijengewa makao ambapo yeye na wenzake wanaendelea kusaidiwa na kupewa mbinu za kukabiliana na maisha. Hazina alibahatika kujifunza upishi na huduma za hotelini na sasa hivi anafanya kazi kama mhudumu katika hoteli hiyo. Hazina alimwomba IJmu waende akanywe chai.

Umu alimtazama Hazina huku kaduwaa. Akamfuata hotelini alikokula shibe yake. Alimsimulia Hazina mkasa huku mito ya machozi ikiwatiririka wote wawili. Hazina alimwonea imani umu kwa kuharibikiwa na maisha katika kipindi ambapo anahitaji hifadhi ya wazazi. Umu machozi yake yalikuwa mchanganyiko wa furaha na majonzi. Furaha kwa kuona kuwa rafiki yake amefaulu kujitoa katika hali ya utegemezi. Huzuni kwa sababu anahisi kuwa ndugu zake wawili huenda ndi0 walichukua nafasi ya Hazina katika mitaa ya miji. Hazina alimwa

hidi kuwa atamsaidia. Akampeleka moja kwa moja hadi kwenye makao yao na kumjulisha kwa Julida- mama aliyesimamia makao haya.

Julida alimkaribisha na kumtaka asijali. Hapo pangekuwa nyumbani mwao kwa muda kisha Julida wangewasiliana na

Idara ya Watoto kuhusu suala la ndugu zake Umu. Ndugu zake wangetafutwa na wangepatikana. Mwezi mmoja baadaye, Umu alijiunga na Shule ya Tangamano akajiunga na kidato cha pili ambako alijipata kuwa mgeni. Mwalimu Dhahabu akatambua kwa wepesi unyonge aliokuwa nao Umu.

Mwalimu huyu akataka pia kujua usuli wa Umu kutoka kwa mwalimu wa darasa la Umu. Mwalimu huyu wa darasa alipoyahadithia masaibu ya Umu kwa Mwalimu Dhahabu, Bi Dhahabu akawa haishi kumhimiza Umu kuwa jasiri kukabiliana na hali yake

hii mpya. Hata hivyo ilimwia vigumu IJmu kusahau yaliyopita. Hata hivyo IJmu aliendelea kuhimizwa na wenzake ayazoee maisha haya mapya.

Siku moja Kairu alimweleza Umu kuwa ana bahati sana kwani yeye hakupitia waliyoyapitia wao. Wao walitendwa ya kutendwa. Wao walipofurushwa kwao siku hiyo hakujua waendako. Mama akiwa mbele nao kina Kairu nyuma. Mama yao alikuwa amembeba kitindamimba ambaye alijifia mgongoni mwa mamake. Baada ya kuuzika mwili wa ndugu yao, kina Kairu waliendelea na safari wasiojua mwisho wake. Hatimaye nguvu ziliwaisha mama yao akawaashiria kuketi kando ya njia, wakawa wanangojea kifo. Mara waliwajia watu waliO-

kuwa wamevaa mavazi yaliyoandikwa IDR,wakasombWa na kutiwa kambini walikokuwa wamejaa sana watoto kwa watu wazima. Hali hapo ilikuwa ngumu. Miiko ilivunjwa. Waliwmil

ia wakawa wanaishi kwa tumaini wakidhani hali itatengenea.

Wakatumaini kwamba wangerudi kwao. Lakini kinyume na matarajio, uongozi mpya hukuleta ahueni yoyote katika maisha yao. Kilichobadilika ni kuwa walipewa ardhi zaidi ya kujenga mabanda zaidi ili kupunguza msongamano katika mabanda ya awali. Sasa wako pale pale. Kairu alikwenda pale akiwa darasa la sita na sasa ako kidato cha pili. Wangali wanasubiri kurudi nyumbani ila yeye haoni kama mna nyumbani pema zaidi ya hapo kambini ambako wanaishi bila kujali mtu alikotoka. Kairu alimsihi Umu kuvumilia na kuzingatia masomo kwani ndiyo yatakayomtoa katika lindi hilo la huzuni.

Kairu aliendelea kumweleza Umu kuwa ana bahati kupata mfadhili. Yeye Kairu, mzazi wake wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki na baada ya ule mzozo wa ni nani kamiliki

Ziwa kuu, biashara yao imedidimia sana. Samaki wamekuwa adimu sokoni na bei yake imepanda. Mamake Kairu hana mtaji wa kuanzisha biashara nyingine kwa kuwa yeye ni maskini. Maisha yamemwia magumu kwani hata karo yake Kairu imembidi amlilie mwalimu mkuu amruhusu alipe kidogokidogo hadi mwisho wa mwaka. Katika mazungumzo ya Kairu inabainika kuwa babake yu hai na ana familia nyingine na kuwa Kairu alizaliwa nje ya ndoa. Umu anapoyaweka masaibu ya Kairu kwenye mizani anaona kuwa anaona msiba wake kuwa mwepesi sasa.

Mwanaheri naye alianza kusimualia na kusema kuwa baada ya kurudishwa nyumbani kutoka Msitu wa Mamba baba yake

Mwanaheri- Mzee Kaizari, aliweza kuyajenga maisha yao upya. Akajenga myumba kufu yao pale kwenye ganjo lao.

Yeye na dadake Lime walirudi shuleni mlemle kijijini mwao tu. Ikawa rahisi kuyazoea maisha kwani wanafunzi wenzao waliwapenda sana. Lime alikuwa hodari katika michezo ya kuigiza- ile ya kitoto. Alikuwa mcheshi mno na kutokuwapo kwake shuleni kuliwafanya watoto kumpeza. Mwanaheri alikuwa naye anakipalilia kipaji chake Cha kughani mashairi mepesi. Majirani wao nao wakamsaidia baba yao kukabiliana na hali hii mpya ya maisha hata hivyo baba mtu alikuwa na hofu kuwa huenda wangeshambuliwa tena, nao majirani walimhakikishia kuwa hawangeruhusu jambo lolote kuusambaratisha tena udugu baina yao. Kwa hivyo hali ya utulivu ilitawala tena.

Uhusiano kati ya marehemu mamake Mwanaheri na mavyaa yake ulikuwa umeingia ufa. Mama mkwe daima alikuwa akimwonea gere mkaza mwanawe kwa kumwona kama aliyekuja kumbwakura mwanawe. Hali hii ikawa imezidishwa na tofauti za kikabila kati ya mamake Mwanaheri na babake.

Mamake ametoka kwenye jamii ya Bamwezi. Daima anachukuliwa kama mgeni, si katika boma lao tu, bali katika kijiji kizima. Uhasama ulizidi baada ya vurugu za miaka mitano iliyopita. Nyanya yao akimwona mamake Mwanaheri kama chanzo cha kuharibiwa kwa mali yao, kwamba ndiye aliyewafanya majirani kuwachomea boma Iao. Mamake Mwanaheri

alidhoofika kiafya kwa majonzi ya kutengwa na wale aliowadhania kuwa wa aila yake. Siku moja waliamka na kupata kibarua juu ya meza dogo iliyokuwa chumbani mwa Mwanaheri.

Mwanaheri alipofungua barua hii alipata kuwa mama mtu alihiari kuondoka kwa kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiWa kwa asiyotenda.

Mwanaheri aliendelea kuwahadithia wenzake na kusema kuwa baada ya miezi miwili babake alienda kumtafuta mamake kwao asimpate. Baada ya kujuzwa kuwa mama mtu alikuwa ameenda mjini Kisuka kuzumbua riziki, babake Mwanaheri alifululiza mjini kwenda kumtafuta mke wake akiwa menye majuto. Alimtafuta na kumtafuta mwezi baada ya mwezi na alipompata alikuwa amejifia chumbani mwake baada ya kutumia kinywaji kikali. Baba mtu alifanya juhudi na mabaki ya mamake Mwanaheri kuzikwa. Mwanaheri alipomaliza kuhadithia kadhia yake, matone mazitomazito ya machozi yalikuwa yakimdondoka. Umu na Kairu walimwacha autue mzigo wake. Sasa Umu alianza kuhisi mzigo wake ulikuwa mwepesi sana.

Mwanaheri aliendelea kuhadithia kuwa mara nyingi mwalimu anapofundisha mawazo yake hutangatanga. Yeye hujiuliza ni kwa nini mamake akakitekeleza kitendo hicho cha ubinafsi.

Kwa kuwa maji yamekwishamwagika, sasa ameamua kuufuata ushauri wa Mwalimu Dhahabu wa kuandama elimu kama ya kumwezesha kuleta mabadiliko katika jamii. Mwanaheri anasema kuwa iwapo mamake angefuata mikakati bora zaidi ya kuhusiana na wakwe zake badala ya kukata tamaa, huenda maisha yake Mwanaheri na ndugu zake yangekuwa bora zaidi.

Zohali naye alikuwa akiusikiliza utambaji wa marafiki zake nacho kilio kikawa kinamwandama. Baada ya kuwaza ikiwa atawatolea wenzake dukuduku lake hatimaye aaliamua kuwasimulia. Yeye alikuwa mtoto wa nyumba kubwa. Babake alikuwa mkurugenzi katika Shirika la Utoaji wa Huduma za Simu na mamake alikuwa mwalimu mkuu wa Shule maarufu

45

ya kitaifa. Wazazi wake walikuwa walezi wema. Zohali na nduguze hawakupungukiwa na chochote. Maisha yake

Zohali yalianza kwenda tenge alipojiunga na kidato cha pili.

Mtafaruku wa kihisia katika umri huo ulimfanya kufanya mambo kwa papara na kutahamaki akawa ameambulia ujauzito. Mwalimu mkuu alimtaarifu dadake Zohali kuwa aikuwa mjamzito na alifaa kurejeshwa nyumbani na akisha kujifungua wazazi wake waweze kumtafutia Shule nyingine.

Tima(dadake Zohali) alimaka. Kutoka siku hiyo maisha ya

Zohali yalichukua mkondo mpya. Amewahi kulala katika barabara za jiji pamoja na watoto wengine wa mitaani, amewahi kutumia gundi ili kujipurukusha, amewahi kupigana na majitu yaliyokuwa yakitaka kuuhujumu utu wake kwa kumnyanyasa kijinsia. Wakati wenzake waliona siku zake za kujifungua zimekaribia za kujifungua walimpeleka kituo cha

Wakfu wa Mama Fatma. Alikuwa ameyapitia mengi. Zohali anamshukuru Mtawa Pacha aliyemwokoa kutokana na kinamasi cha unguliko la moyo. Baada ya Zohali kumweleza kadhia yake, Mtawa Pacha alitikisa kichwa na kumwahidi kwamba baada ya kujifungua angemrejesha shuleni. Sasa hivi anapoongea anafaa kuwa kidato cha nne lakini uzazi na ulezi ulimpotezea miaka yake miwili. Huwa anatamani sana kumwambia Mtawa Pacha ukweli wa mambo kuwa ana wazazi lakini moyo wake hukataa katakata. Atarnwambiaje kuwa ana wazazi ilhali waliisha kumkana alipohitaji pendO lao? Anaendelea kusema kuwa madhila aliyoyapitia nyumbani kwao hayaelezeki. Baba yao alisema kuwa hakuwa na pesa za kulipa kijakazi tena. Kazi zote za nyumbani zikawa za

Zohali. La kuslkitisha zaidi ni, mama rntu ambaye anajua uchungu wa kule mimba hakutoa sauti ya kumtetea. Baada ya Zohali kuyakamilisha masimulizi yake aliyaondoa macho

yake kwenye ukuta yalikokuwa yameganda.

Chandachema alifuata kusimulia kadhia yake. Kisa chake kikiwa na mshabaha na kile cha Zohali. Alilelewa na bibi yake aliyefariki Chadema akiwa darasa la kwanza. Habari ilisema kuwa baba yake Fumba alikuwa amehamia Uingereza na familia yake na ni mhadhiri katika Chuo kikuu. Baada ya nyanyake kuiaga dunia, mambo yake Chadema yalijaa giza.

***Maswali***.

*i) Elezea kwa kifupi madhila aliyoyapata Zohali nyumbani mwao.*

*ii) Eeza kwa muhtasari kadhia aliyoipata Chandachema tangu kufariki kwa nyanyake.*

*iii) Mwcndishi ametumia mbinu rejeshi kwa mapana no marefu katika sura hii. Ffanua jinsi ilivyotumika kwa kutolea visa vitano kwa muhtasari.*

*iv) Fafanuo maudhui ya malezi kama ya!ivyojitokeza katika suro hii.*

*v) Fofanuo sifa za waahusika hawa.*

*G. Mwajimu Dhahabu b. Umu c. Hazino d. Kairu e. Mvvancheri*



*vi) Ukabila umechorwa kama sababu ya kuvurugika kwa ndoa. Fafanua.*

**SURA YA SABA**

Ni alasiri moja ya joto kali. Mwangeka na Mkewe Apondi wameketi kwenye behewa la nyumba yao. Wameyaelekeza macho yao kwenye kidimbwi ambamo wanao watatu- Sophie, Ridhaa na Umulkheri- wanaogelea. Ukichunguza kwa makini utapata kwamba wawili hawa chochote japo wanatazama. Kila mmoja, Apondi na Mwanageka, amepotea kwenye ulimwengu wake. Mwangeka anapomtazama Apondi anatabasamu. Kisa cha kukutana kwao kilikuwa kama ifuatavyo:

Miaka mitatu ya ujane ilikuwa imemdhihaki Mwangeka.

Babake Mwangeka alikuwa akiishi nyumbani kwa Mwangeka kwa muda. Walikuwa wajane wawili waliokomaa. Hitaji la

Mwangeka kuwa na mshirika wa kumwondolea ukiwa lilimwandama. Baba mtu alimtaka Mwangeka kuwazia suala hili, Alijua kuwa wakati ndio mwamuzi, ipo siku atakapotokeza hurulaini wake Mwangeka. Ataifungua kufuli kubwa iliyoufunga moyo wake na hiyo itakuwa siku ya kumwaga chozi la heri. Baba mtu akaendelea kungojea kwa matarajio makuu, kila jioni akimchunguza mwanawe kuona kumetokea badiIikO lolote. Siku moja alikutana na Rachael Apondi ambaye alifanya kazi katika Wizara ya Vijana na Masuala ya Kijinsia. Apondi alikuwa na shahada katika masuala ya kijamii. Apondi alikuwa mmoja wa wawasilishaji na ilipowadia zamu yake kuwasiliSha aliwasisilisha kwa ustadi wa hali ya juu. Akauteka nyara moyo wa Mwangeka. Apondi alipotoka jukwaani alisindikizwa na makofi ya hadhira yake. Mwangeka akamsindikiza na

macho zaidi ya makofi. Moyo wake uliokuwa umejaa barafu ukayeyuka na kutwaa uvuguvugu. Binti huyu alimkumbusha

Mwangeka marehemu mke wake Lily. Mwangeka na Apondi walipata kujuana vizuri zaidi wakati wa chamcha. Huu ukawa mwanzo wa usuhuba na uchumba wa mwaka mwaka mmoja ambao kilele chake kilikuwa kufunga ndoa. Apondi alikuwa mjane wa marehemu Mandu. Mzee Mandu alijifia ughaibuni katika shughuli za kudumisha amani. Kifo chake Mandu kikamwachia Apondi na Sophie mwanawe wa miaka miwili kilio kisichomithilika.

Apondi akawa mwoga, akachelea kuhusiana na mwanamumemwingineasijeakamwachiaufawa moyo. Miaka sita baada ya kufiwa ndipo alipokutana na

Mwangeka na penzi likazalika, wakapanga kuoana.

Alipojifunguamtotowakiumealimwita Ridhaa. Ridhaa ni bavyaa yake aliyemkubali katika familia yake licha ya kwamba koo zao ni tofauti. Akawa na furaha tele kwakuwa

Sophie amepata mwenzake naye Baba Ridhaa amepata fidia japo kidogo kwa familia yake iliyoteketea.

MwangekanaApondiwalikuwawameamuakuwa watoto wao wawili walitosha kukamilisha familia yao. Lakini, ukarimu wao ulifanya kuzaliwa kwa Umulkheri katika familia yao.

BaadayaIJmukujiunganaShuleyaTangamano, mamaaliyekuwaakiyasimamiamakaoambamoUmu aliishi alishirikiana na mwalimu mkuu wa Tangamano kumtafutia mfadhili. Apondi alikuwa rafiki wa utotoni wa Mwalimu Dhahabu. Alipompigia simu na kumweleza kadhia ya IJmu Apondi alikubali kumchukuaUmukamamtotowakewakupanga.

Baada ya kuwasiliana na Mwangeka, Mwangeka hakuwa na

Pingamizi yoyote kuhusu kuwa mlezi wa Umulkheri. Mwange

49

alirnwambia mewe kuwa umu ni baraka KU

Mwenyezi Mungu na kuwa Mungu amemfidia mwanay aliyekufa umu akapata wazazi wapya. Wakawa wanamlipia karo umu mwanzoni alikuwa na shaka lakini baadaye alikuja kuwapenda kwa dhati. Upendo alioupata kwa wazazi hawa wapya uliponya donge chungu lililokuwa moyoni mwake.

Akawa sasa yu tayari kumsamehe mamake hapa duniani na ahera. Akawazia pia kumsamehe Sauna. Hata hivyo alibaki kujiuliza maswali mfululizo kuhusiana na walikotokomea ndugu zake.

*Zoezi kutoka sura hii i)Eleza kwa muhtasari mambo aliyoyczungumzia Apondi katika hotuba yake.*

*ii)Eleza sifa na umuhimu wa wahusika hawa:*

*a. Mwangeka b. Apondi iii)Jadili maudhui ya mapenzi na ndog kama yanavyojitokeza katika sura hii.*

*iv)Upendo ni tiba ya moyo ulio no jeraha. Onyesha namna upendo ulivyotekeleza jukumu hilo katika sura hii.*

*ni baraka kutoka kwa mwenyezi Mungu. Mungu amenifid ia yule mwanangu aliyekufa "*

*a tiweke dondoo hiji katika muktadha wake.*

*b &fanua sifa tatu za mhusika ukionyesha nanna ali*

*baraka kwa msemaji (unaweza kurejelea matukio mengine kwingineko riwayani)*

*c. Fafanua umuhimu wa msemgUi wa maneno haya.*

## SURA YA NANE

SikuhiiDickalihisikuwauwanjawandegeulikuwa nabaridinamzizimokulikosikunyinginezote.Dick alikuwa akiwaza haya akiwa kasimama katika mlolongo mkubwa wa watu ambao walingoja kuingia kwenye afisi za forodha kukaguliwa.

Akawa anakumbuka siku alipoanza kusafiri kwa ndege. Siku hiyo alijawa na kiwewe kwani biashara haramu ya kubeba dawa za kulevya aliyokuwa amejiingiza kwayo ilikuwa irnewaingiza wengi kwenye mikono ya polisi, wakatiwa mbaroni.

Siku hizo alikuwa mwanagenzi katika uga huu kwani alikuwa na umri wa miaka kumi tu. Zipo siku alipotetemeka karibu ajisaliti lakini hatimaye alizoea

kujipa moyo. Sasa miaka kumi ya adha imepita. Alilazimika kukomaa kwa kuwa ulimwengu haukuhitaji mnyonge. Dick alitoswa katika kinamasi cha kuuza dawa za kulevya na Sauna- kijakazi wao.

Dick amesafirisha maelfu kwa maelfu ya vifurushi vya dawa hizi. Mwanzoni akawa si mraibu wa dawa hizi lakini ilibidi ajizoeshe kwa usalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi alilazimika kuzimeza dawa zenyewe ili kwenda kuzitapika kwenye masoko ya ughaibuni. Jambo hili lilichangiwa na uwepo wa mashine zenye uwezo mkubwa wa kung'amua shehena za dawa zilizofichwa kwenye chupi.

Siku ile baada ya kijakazi Sauna kumwiba Dick alimpelekea

baba mmoja tajiri ambaye alijitia kumpeleka shuleni. KumDe alikuwa amempeleka katika biashara ya kuuza dawa za kulevya. Buda (lakabu ya tajiri wake Dick) alipoona Dick akitaka kukataa kushiriki biashara hii, alimtishia Dick kuwa angetupwa nje, asingiziwe wizi na bila shaka Dick alijua malipo ya wezi ni kutiwa tairi na kuchomwa moto. Wazo la kupata adhabu ya aina hii lilimtetemesha Dick. Akambuka rafiki yake Lemi alivyofishwa kwa njia hii. Kisa cha Lemi kilimfanya kuunasihi moyo wake kuingilia biashara hii haramu ili mwenye nguvu asije akamtumbukiza kaburini.

Akajisemea kuwa huenda siku moja akapata mbinu ya kujinasua. Sababu nyingine iliyomfanya Dick kuingilia biashara hii ni kuwa alihitaji chakula na mahitaji mengine. Akasema potelea mbali kwa lisilo budi hutendwa.

Alipojitosa katika biashara hii haramu aliingilia kwa hamasa za ujana. Miaka mitano ya kwanza ikawa imejaa hekaheka kwani alisafiri kwingi na kuona mengi. Akaweza kuchuma pato Si haba, pato aliloliona ni halali yake baada ya ulimwengu kumpoka maisha yake. Hata hivyo asubuhi moja aliamka baada ya kuamua kuwa hakuumbiwa uhalifu, dhamiri yake ikamsumbua na moyo wake kumsuta. Mawazo mengi yakawa yamempitikia akilini na yakamsukuma kuufikia uamuzi wa mkataa,

akajinasua kutoka kucha za mwajiri wake huyu. Akaacha biashara ile haramu na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa Vya umeme. Leo hii amejiajiri. Ashaamua kuufungua ukurasa mpya katika maisha yake. Amekwisha kuhitirnU masomo katika Chuo cha ufundi ambakO alijifunza teknolojia ya mawasiliano ya Simu. Sasa amepanua mawanda yake ya kibiashara. Anauza vifaa vya simu. Husafiri ng'amb0 mara kwa mara kununua bidhaa ili kuyauzia mashirika yanayotoa

huduma za mawasiliano. Asubuhi hii Dick na kijana mwenzake (mwajiriwa wake) walikuwa katika safari ya kawaida. Alinuiwa kuabiri ndege ya saa moja asubuhi kuelekea ughaibuni ambako alizoea kununua mali yake. Huku akingoja afisi kufunguliwa, mawazo ya nyuma yaliivamia akili yake na akayakunjua maisha yake ya siku za Mlima wa Simba. Akamwazia mama yake kwa masikitiko makuu. Akashanga jinsi ulimwengu unavyoweza kummeza mwanadamu akawacha kuwaazia hata wana wake. Akamkumbuka babake katika dakika ya mwisho ya uhai wake. Maneno yake yalikuwa "wanadamu ni hasidi" ndio waliomsababishia uwele alionao. Dick akiishi, atawaona. Akili yake ikamtuma kumkumbuka Umulkheri- dadake. Anakumbuka alivyomwambia kuwa asijali kwani yeye angewakimu kwa viganja vyake na hawangepungukiwa na chochote. Akawa na maswali chungu nzima kuhusiana na aiiko Umu.

Wakati Dick alikuwa akiwaza kuhusu familia yake, hakujua kuwa Umulkheri alikuwa nyuma yake kapiga foleni. Anasafiri ng'ambo kwa shahada yake ya uhandisi katika masuala ya kilimo. Umu, baada ya kuchukuliwa na Mwangeka na Apondi alifanya bidii masomoni na kufuzu vyema katika mitihani yake. Kisadfa, safari ya Umu imekuwa siku hii ambapo Dick anasafiri. Dick aliposikia Mwangeka akimwita Umu na kumtaarifu kuwa ndege i karibu kuondoka, hakuamini. Mazungumzo baina ya Umu na wazazi wake yalimwamsha Dick kutoka lepe lake la muda. Aligeuka na kutazamana ana kwa ana na Umu. Mwanzoni Umu akidhani macho yanamdanganya. Mikono yake ikamwachilia dadake Sophie, moyo

wake ukamwenda mbio. Ghafla Dick, alimwita dadake Umu na

kumkimbilia. Wakakumbatiana. Wasafiri wote na aila yote ikawatazama kwa mshangao. Machozi yakawadondoka wote wawili na kulia kimyakimya huku wakiambiana kimoyomoyo yote yaliyowakumba. Hatimaye sauti iliita ikitangaza kuwa abiria wa ndege Tumaini waanze kuingia. Walijua kuwa jaala ilikuwa imewakutanisha na hawatawahi kutengana tena.

*Zoezi i)Elezea kwa kifupi namna dawa za kulevya husafirishwa kutoka eneo moja hadi lingine kwa mujibu wa sura hii.*

*ii)Fafanua sifa za Dick kisha uelezee umuhimu wake.*

*iii)Dawa za kulevya zina madhara chungu nzima. Tetea kauli hii.*

*iv) Elezea kwa muhtasari namna Lemi alivyofishwa.*

*v) Ni mambo gani yalimsukuma Dick kujiingiza katika biashara haramu ya kuuza dawa za kulevya?*

*vi) Elezea sadfa ilivyotumika katika sura hii.*



**SURA YA TISA**

Sura hii inaanza kwa Wimbo wake Shamsi. Leo Shamsi anasikika kama amebadilisha wimbo wake kama anawosema

Ridhaa japo kwa sauti ya chini. Wimbo huu wa leo unasikika kama wa kiumbe mwenye maumivu zaidi na mapigo yake hasa ni ya mbolezi. Huu wa leo ni tofauti na majigambo yake ya kila siku. Ridhaa alianza kuyaghani majigambo yake

Shamsi kwa sauti ya chini kama anayeyatia maneno ya majigambo kwenye mizani.

Ridha anamtazama Shamsi akipita kama afanyavyo kila siku.

Mtaa anakoishi Shamsi si mbali na hapa, Shamsi na Ridhaa ni majirani. Huu ni mwezi wa tatu tangu Ridhaa kuhamia mtaa wa Ahueni. Ahueni ni mtaa wa raia wenye kima cha juu kiuchurni. Mtaa huu una sura ya mijengo ya kifahari ya ghorofa.

Daraja kubwa limeutenga mtaa huu na mtaa wa Kazikeni inakoishi familia ya Shamsi na nyingine za aina yake. HukO maisha ni ya kubahatisha. Huu ni mtaa wa mabanda yaliyojengwa kwa udongo na mabati.

Mwangeka aliamua kuhamia mtaa wa Ahueni baada ya mjukuu wake wa mwisho kuzaliwa. Aliona ulikuwa wakati wake kuanza kuyajenga maisha yake upya. Maisha ya

Mwangeka sasa yalitengenea. Baada ya kuzungumza na mwanawe, Ridhaa alimwomba Mwangeka amruhusu aondoke ili akaanze kuyazoea maisha ya ujane. Aliondoka akiwa na azimio la kukamilISha kukijenga kituo cha afya cha

Mwanzo Mpya alichokijenga kwenye ganjo lake. Kituo hicho kingewafaa raia wengi ambao hawangemudu gharama ya matibabu katika hospitali za kibinafsi.



Selume alifanya kazi katika kituo cha afya cha Mwanzo Mpya.

Hali katika kituo hiki ni bora kuliko ilivyokuwa katika hospitali ya umma. Huko alikuwa amechoka kutokana na kuwatazama wagonjwa wakifa kwa kukosa huduma za kimsingi huku shehena za dawa zilizotengewa hospitali hii zikiiShia kwenye maduka ya dawa ya wasimamizi wa hospitali. Alikuwa amechoshwa na mambo mengi. Katika kituo hiki kipya

Selume aliajiriwa kama Muuguzi Mkuu naye Kaizari kama

Afisa wa Matibabu. Sasa huu ni mwaka wa tatu tangu kuanza kazi hapa chini ya usimamizi wa Ridhaa ambaye ndiye mkurugenzi.

Anawahudumia wagonjwa walio na matatizo aina aina. Kuna mgonjwa mmoja aliuguza majeraha katika mgogoro wa ardhi katika eneo la Tamuchungu. Mwingine aliyejifia ni kijana anayesomea shahada ya uzamili, alikuwa mwathiriwa wa pombe haramu. Mgonjwa mwingine wa kike kwa Jina Tuama alikuwa amejipata katika hali mbaya kwa kukubali kupashwa tohara. Alibahatika kwa kuwa hakuiaga dunia kama wenzake.

Tuama anaitetea mila hii ya upashaji tohara kwa wanawake eti haijapitwa na wakati kwani bila tohara mwanamke hubakia kuwa mtoto. Anaendelea kusema kuwa kupashwa tohara hakumaanishi kuacha Shule kwani dadake Hazina alipashwa tohara lakini sasa amehitimu shahada kutoka Chuo kikuu.

Yeye anasema la msingi ni kuwa hakika katika ulengaji shabaha kwenye malengo yako.

Mgonjwa mwingine kwa jina Pete aliendelea kupata ahueni.

Yeye aliokolewa akitaka kujiangamiza pamoja na kitotO chake. Pete alizaliwa katika kijiji cha TOkasa. Yeye ndiye mtoto wa nne katika familia yenye watoto sita. AlipoutambUa



ulimwengu tu, alijipata kwa nyanyake mzaa mama. Sababu yake kujipata katika hali hii ni ule mtafaruku uliokuwa umetokea baina ya mamake na babake Pete kisa na maana, Pete hakuwa na mshabaha hata chembe na babake. Mama yake

Pete kwa kuchelea kuiharibu ndoa yake akampagaza nyanya mzigo wa malezi. Pete hajadiriki kuonja tamu ya kupendwa na wazazi wake. Alipoanza kupata hedhi maisha yalichukua mkondo mwingine. Alipoingia darasa la saba alipashwa tohara nao wajombake wakapokea posa na baadaye mahari

kutoka kwa buda mmoja kwa jina Fungo aliyemuoa kama bibi wa nne. Alipojifungua, akaamua kwa mzee Fungo hakumweki tena. Akaondoka bila kuangalia nyuma. Akaingia jijini kuzumbua riziki. Akapata ajira ya kijishahara duni ambacho hakikutosha kugharamia mahitaji yake yote. Maisha yakazidi kuwa magumu hadi akamzaa mwana wa pili. Kitoto alichonacho zahanatini ni cha tatu na alikipata akiwa katika shughuli za uuzaji pombe. Mambo yalipombainikia kuwa ana watoto watatu kabla ya kufikisha umri wa miaka ishirini na moja, aliona ni heri ajiangamize. Alimwambia jirani yake amchungie watoto kisha akaacha kikaratasi chenye anwani ya bibi yake kwenye kimeza katika chumba chake na kuondoka. Alijiambia kuwa dawa ya panya haingeshindwa kumuua yeye pamoja na kilichomo tumboni na ndipo akamimina kopo la dawa hiyo kinywani. Sasa anapata ahueni katika kituo hiki cha afya.

Kijakazi Sauna anatamani kurudi kitandani alale lakini inambidi amtayarishie Bi. Kangara kiamshakinywa kwani ana miadi ya mapema na mzalendo mmoja jijini. Anapojngia jikoni na kuanza shughuli zake moyo unaanza kumwenda mbio na

vipapasio vya akili kusimama wima. Kwa mbali anaskia mbisho hafifu langoni mwa jumba hili. Anapotoka kwenda kuitikia mbisho huu anakumbana ana kwa ana na polisi. Hii ni wiki ya pili tangu Sauna kuwatorosha Dick na Mwaliko. Dick ni mali ya Mzee Buda naye Mwaliko amepelekewa Bi. Kangara awe na mwili kidogo kisha atafutiwe la kufanya. Sauna ashapata ujira wake na yu tayari kuondoka asubuhi ya kuamkia Krismasi.

Sauna alipachikwa mimba na babake mlezi. Mamake mzazi alimsaidia kuavya kisha akamwonya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama wa babake. Mamake hakumtaka

Sauna kumpaka tope babake. Maneno yale yalimtonesha

Sauna kidonda. Mamake alikuwa mjane wa Mzee Kero.

Baada ya tendo hili, Sauna aliondoka nyumbani kwani hapakumweka tena. Amewahi kufanya kwenyemachimboyamawe,amehudumukatika majumba ya kuuza pombe kwa namna zote amefanyamengi.Bi.Kangarandiyealiyemfunza Sauna mbinu hii mpya ya kuwateka nyara watoto wa waajiri wake na kuwauza. Sasa hii ndiyo siku ya arubaini. Wawili hawa walitiwa mbaroni na kufikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la kukiukahakizawatoto,wakafungwamiakasaba gerezanina kazi ngumu. Polisi walimchukua

Mwaliko katika kituo kimoja cha watoto mayatima ambak0

aliendeleanamasomoyeyenawenzake.



***Zoezi***.

*i)Ni ujumbe gani umetamalaki katika wimbo wa Shamsi?*

*kwa muhtasari ujumbe uliomo katika majigambo aliyoyaghani Ridha.*

*'iii)Jadilimaudhuiyautabakakamayanajitokeza katika sura hii, 'iv)Ni kwa nini Selume aliifurahia hali katika kituo cha afra cha*

*Mwanzo Mpya kinyume na hapo awali a!ipokuwa akifanya katika hospitali ya umma? Elezea.*

*v)Pombe haramu inamothara chungu nzima. Tetea kauli hii kwa mujibu wa sura hii.*

*vi) Eleza sifa za wahusika hawa:*

*a. Selume b. Meko c. Kipanga vii)Kupashwa tohara kwajinsiayakikekunahasaranyingikulikoaida. Tetea kauli hii.*

*viii)Jadili maudhui ya malezi kama yanavyojitokeza katika sura ix)Eleza kwa muhtasari masaibu aliyoyapitia Sauna akabadilika a kuwa mvunja sheria.*



*nye gn na a Izawatoo u wa warnul u WO*

**<u>SURA YA KUMI</u>**

Surainapoanaza,MwangemianamraiNeemaasiwe namawazofinyukuhusukupangamtoto.Anasisitiza kuwa hakuna udhaifu wowote katika kumpanga mtoto. Wamejaribu kupata mtoto kwa muda wa miaka mitano bilamafanikio.

Neemaamewahikutungamimbasimaramojaau mbili, amefanikiwa kuilea mimba hadi ikakomaa wakaweza kukipakata kilaika mikononi mwao. Kitoto hicho kiliaga kabla ya juma moja. Mwangemi na Neema walihuzunika kumpoteza mwana. Sio eti Neema hataki kumlea mwana, la hasha, anatamani kukipakatakilaikakiwechakeauchamwingine.Ni dhamiriyakeambayohumsutasanaakikumbuka nafasi aliyoipoteza aliyopewa na Mungu wakati mmoja ya kumpangamtoto.

Mwangemi alimsihi Neema mke wake asijisulubu kwa kosa ambalo alilitenda kwa kutokuwa na ufahamu bora wa malimwengu. Hayo yamepita. Baada ya Neema kukubali rai ya

Mwangemiwaliendakatikakituochawatotocha Benefactor na leo hii wamo afisini. Walikaribishwa na Mtawa Annastacia aliyewataarifu kuwa alilipata ombiIaolakutakakupangamtotokutokakituochao. Wakaelezwakuwakunakijanammojawakiumena iwapo wangefaulu katika mahojianO kituo hicho kingewakabidhi mtoto huyo. Mahojiano yalipokamilikaMwangeminaNeemawakaondoka wakitarajia kurudi kumchukua mwanao. Waliporudi afiSini mwa Annastacia wana furaha mzomzo kwani walifaulu katika mahojianona

wako tayari kumchukua mwana wao. Mwangemi anahisi kuwa familia yake imekamilika.

Kijana huyu alipoletwa Mwangemi alimtulizia macho, kijana huyu ni mrefu na mwembamba, mwenye sura jamali. Macho yao yalipokutana kijana alitabasamu

na kudhihirisha meno meupe pepepe ambayo yalimkumbusha binamu yake

Mwangeka. Hapohapo nyoyo zao zikaungana kila mmoja akijisemea kimyakimya, "Haikosi huyu atakuwa rafiki wa dhati "

Mwaliko alitambulishwa kwa wazazi wake wapya. Kisha

Mtawa Annastacia akamwahidi kuwa atakuwa akienda kumwangalia mara kwa mara. Mwaliko akamtazama Neema kwa hofu iliyojaa mapenzi. Badaye akamkumbatia Neema na kumwambia kuwa atakwenda naye. Chozi la furaha lilimdondoka Neema, akamkumbatia Mwaliko kwa mapenzi ya mama mzazi. Akahisi kama aliyezaliwa upya. Sasa amepata kizazi.

Hatachekwa tena na walimwengu eti anazaa watoto wenye upungufu kwa sababu aliavya mimba nyingi akiwa shuleni.

Akasema hata kama kitoto hiki si chake kitampa mshawasha wa kufanya kazi zaidi ili kukikimu.

Mwaliko alilelewa na Mwangemi na Neema kwa tunu, tamasha na nidhamu. Akainukia kuwa ghulamu mwenye nidhamu ya hali ya juu, akiwaheshimu wazazi na majirani na akiwatii walimu wake. Alipohitimu kidato cha nne alijiunga na Chuo kikuu kusomea shahada ya Isimu na lugha, wazazi wake wakajua kuwa juhudi zao za malezi hazikuambulia patupu. Walikuwa wamechangia katika kumpa tegemeo mwana wa mwenzao.

Miaka mitatu imepita sasa tangu Mwaliko kukamilisha



masomo yake ya chuo klkuu. Amejisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu. Ameajiriwa na kampuni ya gazeti Tabora kama mhariri katika kitengo cha biashara. Anafanya kazi yake kwa bidii ya mcbwa.

Mwaliko alitamani siku ambayo angekutana na ndugu zake, moyoni aiihisi kuwa walikuwa hai. Mama Neema aliishi kumkumbusha kuwa siku moja atawaona ndugu zake. Siku moja

Mwaliko na baba yake waliamua kwenda kujivinjari. Ilikuwa siku ya kuzaiiwa kwa Mwangemi. Mwaliko akaamua kumnunulia babake chamcha. Walienda katika hoteli ya Majaliwa saa sita unusu adhuhuri. Mwaliko alikuwa akiwaza kuhusu waliko ndugu zake lakini hatimaye akamtakia babake siku njema ya kuzaiiwa kwake.

Kisadfa familia ya kina Umulkheri walikuwa katika hoteli ii hii wakisherehekea siku ya kuzaiiwa kwake Umu. Umu akawa anawashukuru wazazi wake kwa hisani yao. Dick vilevile akawa anatoa shukrani kwa Mwangeka na Apondi.

Mwangemi aliwapata kina Mwangeka wakiwa katika hali ya kutafakari kusu hotuba ya Dick. Mwangemi ni binamu yake

Mwangeka. Mwangeka alishangaa ni sadfa gani iliyomleta

Mwangemi katika maeneo haya. Akamtaarifu ami yake kuwa huwa haji humu ila mwanawe Mwaliko aling'ang'ania kumleta hapa kwa chakula cha mchana. Kisadfa siku hil ilikuwa siku ya kuzaiiwa kwa Umu na Mwangemi. Dick na Umu hawakusikia alichokuwa akisema Mwangemi, walimaka kusikia Mwangemi akitaja jina la Mwaliko. Walishangaa iwapo ni sadfa nyingine kuwa Mwangemi ana mtoto mwenye jina kama la ndugu yao mnuna. Walijiuliza maswali chungu

"

Mwangemi alimwita Mwaliko aje ili amjuze kwa binamu yake

Vuuk (lakabu ya Mwangeka). Alipokuja, Umu alimtazama ghulamu huyu kwa tuo akamtambua kuwa ni nduguye Mwaliko. Dick vile alikuwa keshamtambua nduguye. Mwangemi alimkumbusha

Mwaliko kile kisa ambacho alimsimulia kila mara kuhusu yeye na Vuuk baada ya kumtambulisha kwa

Mwangeka. Mwangeka alicheka kicheko kikubwa na katika kipindi kidogo akayaleta maisha ya kisogoni mbele ya kipaji chake. Wakahadithiana matukio ya utotoni waliyoyafanya pamoja vikiwemo vita vya majogoo nk. Mwangeka akawa amezama katika kisa chake na babu.

Mwangemi aliendelea kumtania Mwangeka kuwa ndiye mhandisi mwenyewe. Yeye ndiye aliyevumbua gari la kwanza la Kiafrika. Mwangemi alipoona amemtonesha kidonda mwenzake na kumbukumbu zake, akatabasamu.

Aliendelea kusema na kumjuza kuwa hayo yote yamepita na hiyo ilikuwa ni hatua ya ukuaji, ilibidi waipitie. Alimgeukia

Mwaliko na kumtambulisha kwa Mwangeka. Akamweleza kuwa si mwana tu bali ni rafiki yake wa dhati. Maisha yake

Mwangemi na Neema yangekuwa tupu bila yeye. Mwangeka na Apondi walipomtazama Mwaliko waliuona mshabaha kati ya Umu, Dick na Mwaliko. Yote yamewabainikia na sasa wanangoja kuhakikishiwa na Umu kuwa huyu ndiye ndugu yao ambaye mamekuwa wakimtafuta mSitu na nyika. Moyo wa

Mwaliko tayari urnemwambia kuwa hawa ni ndugu zake kwa kuwa wameshabihiana na wale watoto walio kwenye picha ambayo baba yao I-unga alipigwa nao kabla ya mauko yake.



Picha hii mwaliko ameihifadhi katika buku lake kama kumbukukumbu ya familia yake. Kijakazi Sauna alikuwa amezoea kumwambia kuwa hao ni Umu na Dick. Mwaliko aliinua macho yake na kuwaita Umu na Dick na kuwaambia kuwa ni yeye na kuwa yu hai. Umu na Dick hakumngojea Mwaliko kumaliza. Walimkimbilia wote na kumkumbatia ndugu yao,

wakaanza kulia huku wakiliwazana. Sophie na Ridhaa nao walijiunga nao, wote wakakumbatiana na kulizana, wakashikana mikono na kufanya mduara kama ule ufanywao na watoto wakicheza. Ikawa wanaunga udugu upya. Wazazi wakabaki kutazama bila kusema lolote. Umu akawaomba wote kuketi chini, yeye akaketi baina ya wazazi wake wawili kama alivyopenda kufanya kila mara. Akasimulia kwa furaha alivyokuwa akihisi huku akimshukuru Mwangemi kwa kumlea

Mwaliko hadi akawa mwana wa kutegemewa. Dick naye hakuchelewa kumshukuru Umu kwa tumaini alilompa kuwa siku moja atamwona ndugu yao. Alimshukuru pia kwa ukarimu wake.

Mwaliko naye akasema kuwa kuja kwao pale kulikuwa kwa heri kwani familia yao imepanuka. Tayari amekutana na mabinamu ambao aliskia tu wakitajwa. Tena ikawa heri kwa kuwa mjomba Mwangeka ndiye mzazi na mlezi wa nduguze.

Mwangemi akawa anamtazama mwanawe kwa imani na furaha kubwa. Sasa watajenga uhusiano wao upya na kumtafuta mama yao na kumsamehe. Mwangeka alisema kuwa

Naomi(mama yao kina Umu) ana haki ya kujua walipo wanawe.

Jambo ambalo Mwangeka hakujua ni kuwa Naomi baada ya kurudi kwao, hakuishi na wazazi wake. Alihamia mjini na



kuwa shangingi kwelikweli. Alikumbana na Bwana Kimbaumbau aliyemweka Naomi kimada kwa muda. Bwana huyu alimpitisha Naomi makuruhu yasiyomithilika, kusimangwa, kupigwa na kuadhibiwa. Naomi akawa anajuta sana. Alijuta kumwacha Lunga(mume wake) wakati ambapo alimhitaji zaidi.

Sasa hana uso wa kuwatazama wanao. Siku aliyopigwa pute na Kimbaumbau, uchungu wa uzazi

ulimtuma kuwatafuta wanawe. Akaenda hadi Mlima wa Simba na kufululiza hadi nyumbani ambapo hapakuwa na mtu, palikuwa mahame.

Alifyeka magugu katika kaburi la mume wake na kunadhifisha kiambo kisha akaweka koja la maua juu ya kaburi. Kwa kweli amekuwa akiwatafuta wanawe. Hamna kituo Cha polisi ambacho hakubisha hodi. Juhudi hizi hazikuzaa matunda.

Kwa sasa hana lolote la kujivunia ila ameanza kuyajenga maisha yake upya. Amefungua kiafisi kidogo karibu na Chuo

Kikuu cha Mbalamwezi anakowapigia wasomi kazi zao chapa na kuisarifu miswada yao.

Dick alisema kuwa mamake ana haki ya kusamehewa kwani hakuna binadamu aliyemkamilifu. Watashirikiana kumtafuta mama yao.

Mwaliko alimwambia baba yake muda wa kufanya hayo upo lakini kwa sasa, la muhimu ni kuwa ndugu zake wako haj.

Sasa ni wakati wa kuondoka kuelekea nyumbani kwani ana hamu ya ya kumwambia Young Neema majaliwa yao ya leo.

*ni)Ndoa bila watoto si kamilifu. Fafanua kwa kurejelea sura hii.*

*ii)Fafanua ufoafu wa nwani chozi la heri ukirejelea matukio katika surg hij.*

*iv) Elezasifa nnenne za wahusika hawa:*

*a. Mwangemi b. Neema c. MwalikO d. Dick e. IJmu f. Apondi g. Mwangeka iv)Mwiba wa kujidunga hauna kilio. Kwa kumrejelea Naomi, onyesha ukweli wa methai hii.*

*v)Onyesha sadfa ilivyojitokeza katika sura hii.*

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu, neno Dhamira lina maana ya kusudi wazo kuu au ujumbe mkuu wa mwandishi. Dhamira pia ni lengo la mwandishi anapoandika kazi.

Kwa hivyo tunapoangazia dhamira ya mwandishi tutajibU swali hili: Je, nialengokusudi la mwandishi huyu ni gani?

Assumpta K. Matei alidhamiria yafuatayo alipokuwa akiandika

Riwaya ya Chozi la Heri. Kuupiga vita ukabila. Tumepata katika Riwaya ukabila ukiwa chanzo cha migogoro. Watu wengi wameathirika vibaya kwa kuwa watu wa kabila tofauti na lao waliwabagua, kuwaumiza au hata kuwafukuza makwao hata kama walikuwa majirani kwa miaka mingi. Kwa mfano mamake Mwanaheri(Subira) alilazimika kuondoka nyumbani bila hiari na kutengana na familia yake kwa kuwa alibaguliwa, akafitiniwa na hata kulaumiwa kwa asiyoyatenda. Alifanyiwa mambo haya yote kwa kuwa Subira alikuwa ametoka kwenye jamii ya

Bamwezi naye babake Mwanaheri alikuwa wa jamii tofauti.

Kila mara Subira alikuwa akiitwa na mama mkwe muki yaani

"huyo wa kuja". Subira alidhhoofika kiafya kwa kutengwa na aliodhania kuwa wa aila yake. Hatima ya mambo haya ilikuwa ni Subira kujitoa uhai.

Kuvipiga vita 'vita vya baada ya kutawazwa ' Vita wa baada ya kutawazwa vilikuwa sababu ya watu kuacha makwao na kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani. Wahafidhina wengi waliathirika sana. Familia zikatengana na watu wakapoteza wapendwa wao na mali zao walizokuwa wametafuta kwa jasho lao wenyewe. Mwandishi huyu ana nia ya kuwahamasisha raia kujitenga kabisa na machafuko hayo kwani huzaa shida na dhiki kuu.

Kuufichua uozo ulio katika jam". Katika Riwaya ya

Chozi la Heri, mwandishi kupitia kwa wahuslka wake na mtindo wake wa uwasilishaji, amefaulu

kuunchu"gozo. I-Jozo ni mambo yote mabaya yanayokinzana na maadlli

Uozo huu ni pamoja na: biashara haramu ya aw kulevya, utekaji nyara wa watoto, kubakwa kwa wasichana, kupashwa tohara kwa wasichana, ndoa za mapema kwa wasichana wadogo, uasherati na uavyaji mimba, matumizi ya mihandarati, WIZi na uporaji wa mali za wenyewe, mauaji ya halaiki, uharibifu wa mazingira, ukabila, ubinafsi wa viongozi, ufisadi nk. Mambo haya yote yamefichuliwa kuwa yapo katika jamii na kuwa hayafai kabisa kwani ni kinyume na maadili ya mwanadamu.

Kuonyesha umuhimu mapenzi katika ndoa na familia. Mwandishi huyu ameonyesha wazi kuwa taasisi ya ndoa na familia inafaa kujengwa katika mapenziupendo. Familia ya Lunga ilisambaratishwa na ubinafsi wa Naomi. Naomi alimwacha mume wake na watoto wao watatu- IJmu, Dick na

Mwaliko. Wana hawa walipata taabu kwa namna mbalimbali kwanj baada ya baba yao kuiaga dunia kijakazi Sauna alipata nafasi ya kuwateka nyara Dick na Mwaliko na kuwauza kwa wateja wake. Watoto hawa walibahatika tu kwa kudura za

Mwenyezi wakapata wazazi wengine wenye utu na mapenzi wakawalea na mwishowe wakawa watu wa kutegemewa.

Kwa hivyo, tasisi hii ya ndoa inafaa kujikita katika upendo.

## MAUDHUI.

Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Hujumuisha mawazo na mafunzo t0fauti yaliyomsukuma

68

### I. MAUDHUI YA MIGOGORO.

Migogoro ni mivutano na mikinzano mbalimbali katika kazi ya fasihi.

Migogoro huweza kuwa kati ya wahusika, familia zao, matabaka tofauti, nyadhifa mbalimbali, kiuchumi, nafasi katika jamii au hata kisiasa.

Aina za migogoro katika riwaya hii.

a) Kuna mgogoro kwenye familia ya Mzee Mwimo Msubili, kwa sababu familia yake ilikuwa kubwa na hakuitosheleza kwa chakula. Uk 9,"Wingi wa vinywa vya kulishwa ulizua uhasama, migogoro na hata uhitaji mkubwa "

b) Mgogoro wa kijamii unajitokeza baada ya mkoloni kupuuza sera za Mwafrika.

Uk 10,"Hatua ya mkoloni ya kupuuza sera za Mwafrika za umiliki wa ardhi na kuamua kujumuisha pamoja ardhi iliyomilikiwa na mtu binafsi na

kuuidhinisha umiliki huu kwa hatimiliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii "

c) Kulijitokeza mgogoro shuleni wakati Ridhaa aliitwa 'mfuata mvua',na kutengwa na wenzake. Walimwona kama mwizi.

Uk 10,"Wewe ni mfuata mvua. Hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda katika mitihani yote. Wewe ndiwe unayetuibia kalamu zetu "

d) Ridhaa alijipata katika hali ya mgogoro na nafsi yake.

Uk 12,"Miguu yake sasa ilianza kulalamika pole pole parafujo za mwili wake zililegea, akaketi juu ya ya wapenzi wake. Baada ya muda wa mvutano, wa hisla na

mawazo, usingizi ulimwiba.

e) Kulikuwa na mgogoro uliosababishwa na wanasiasa, juu y nani atakaye kuwa kiongozi wa jamii, kati ya mwanamke mwananume.

Uk 19,"MijadaIa hii ilizua na kukuza migogoro isiyomithilika "

f) Mgogoro mwingine ulijitokeza kati ya raia na wanapolisi, wakiwa katika harakati zao za kuweka amani.

Uk 19,"Mchezo wa polisi kukimbizana na raia ulianza katika mchezo huo mamia ya roho zisizo na hatia zilisalimu amri chini ya pambaja za risasi na mapigo ya rungu, vitoa machozi navyo vikafanya kazi barabara.

g) Nyamvula anajikuta katika mgogoro wa nafsi yake, wakati ambapo imani yake inakinzana na kazi ya kuwa askari.

Uk 62,"Kulingana na Nyamvula, kuwa askari wa vita kulikinzana na imani yake, hasa kwa vile Nyamvula alisema ni born again. Mwangeka alimsisitizia kuwa kulinda usalama si sawa na kuua "

Katika ukurasa wa 38 Tila anaitaja migogoro kadha iljYO katika Tamthilia ya Hussein. Tamthilia hii ya Mashetani ninayorejelewa ina migogoro mingi sana kama: migogoro ya kisiasa, kiuchumi, na pia ya kijamii.

"Tila:

Nadhani umesahau baba. Suala hili ulisema limeshUghulikiwa katika kazi za kifasihi kama vile Mashetani, ile tarnthilia ya

Hussein inayoisawiri migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya baada ya ukoloni Isitoshe, mwalimu alitaka tu kuonyesha



kwamba upo uhusiano kati ya mfumo wa kiuchumi na mfumo wa kisiasa alituambia kwamba mfumo wa kiuchumi hudhibitiana na mfumo wa kisiasa. Utawala huteuliwa makusudi kuendeleza mfumo uliopo wa kiuchumi kwa maslahi ya watawala na tabaka ambalo linazimiliki nyenzo za uzalishaji mali "

2. **UMASIKIN1**.

Umaskini ni ukata. Ni hali ya kukosa fedhamali nk.

Tunapata kuwa waafrika wanajikuta katika hali ya umasikini;

Uk 7,"Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wdogowadogo, maskini, wasio na ardhi "

Uk 25,"Nyinyi ndio vikaragosi wanaotumiwa na wasaliti wa nia zetu kuendelea kutudidimiza kwenye lindi hili la ukata "

Ridhaa pia anajikuta kwenye lindi la umaskini baada ya mali yake yote kuchomwa, ikiwemo familia yake.

Uk 1,"Ridhaa alisimama kwa maumivu makali, mikono kairudisha nyuma ya mgongo wake uliopinda kwa uchungu. Macho yake yaliyotanda ukungu

alikuwa kayatunga juu angani, akitazama wingu la moshi lililojikokota kwa Kedi na mbwembwe; wingu lililomwonyesha na kumkumbusha ukiwa aliozaliwa nao na ambao alihofia kuwa angeishi na kuzikwa nao "

Tunapata pia kuwa watu wengi wanaiaga dunia wakijaribu kujikomboa kutokana na hali hii

71

ya ukata, wanapoenda kuchota mafuta kwenye lori ambalo limebingirika kisa na maana alienda kuwaokoa watu ambao wa-

Uk 54 "

likuwa wakipora mafuta kutoka kwenye lori, ambalo lilikuwa limebingiria Inasemekana kuwa umaskini uliwasukuma watu hawa kuchukua kisichokuwa haki yao!"

3. **USHIRIKINA**.

Hii ni hali au tabia ya watu kuamini mambo ya utamaduni ambayo mara nyingi, yanajihusisha na uchawi.

Ridhaa anaposikia milio ya bundi, anaamini kuwa milio hii ina maana iliyofichika.

Uk 1,"Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama. Milio hii ndiyo iliyomtia kiwewe zaidi kwani bundi hawakuwa wageni wa kikaida katika janibu hizi "

Uk 2,"Ninashangaa ni vipi daktari mzima hapo ulipo unajishU-

ghulisha na mambo ya ushirikina.

4. **NDOA**.

Haya ni maafikiano rasmi baina ya mume na mke ili waweze kuishi pamoja.

Kuna ndoa kati ya Ridhaa na Terry.

akamgeukia mumewe tena na kusema, ...laiti

Ridhaa angalijua kwamba hii ndiyo mara yake ya mwish0

kuzungumza na mpenzi mkewe. Tunapata kuwa Ridhaa ana

mwoa Terry, uk ll "Baadaye aliamua kuasi ukapera, akapata mke, Terry"

Mwangeka alikuta na Lily Nyamvula katika Chuo kikuu na kumwoa. Walibarikiwa na mtoto mmoja kwa jina Becky.

Ndoa hii haikudumu kwani Lily na Becky waliangamia kwenye janga la moto.

Baada ya ndoa ya mwanzo kusambaratika, Mwangeka alimwoa Apondi. Walibarikiwa na mwana wa kiume kwa jina

Ridhaa.

Mwangemi alimwoa mwanamke kwa jina Neema. Hawakufaulu kupata mwana wao kindakindaki japo walipanga mwana wao kwa jina Mwaliko.

Kangata alikuwa na mke wake kwa jina Ndarine. Walibarikiwa na wana wafuatao. Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na Akelo Kiriri.

Lucia Kiriri —Kangata-,-alikuwa ameolewa katika ukoo wa

Waombwe ambao awali walikuwa maadui sugu wa ukoo wa

Anyamvua. Ndoa hii ilipata pingamizi sana kutoka kwa ukoo mzima lakini kutokana na Msimamo imara wa Kangata ndoa hii ilisimama. Watu wa ukoo wa kina Kangata walishangaa ni kwa nini mwana wao akaozwa kwa watu ambao huvaa nguo ndani nje na pia huzaa majoka ya mdimu ambayo ni machoyo kupindukia.

Kaizari alikuwa na mke kwa jina Subira. Walibarika na mabinti wawili, Lime na Mwanaheri.

73

Lunga alikuwa na mke kwa jina Naomi. Walikuwa na wana watatu, Umu, Dick na Mwaliko. Ndoa hii haikudumu kwani

Naomi alimwacha Lunga na kwenda mjini alikokuwa shangingi kwelikweli.

Pete na Fungo- tunaelezwa kuwa Pete alipoingia darasa la saba alipashwa tohara nao wajombake wakapokea posa na baadaye mahari kutoka kwa buda mmoja kwa jina Fungo aliyemuoa kama bibi wa nne. Ndoa hii haikudumu kwani Pete alihiari kumwacha baba huyu.

5. **MAUT1**.

Hii ni hali ya kuiaga dunia wahusika wengine wanakutana na janga hili la mauti, ilhali wengine walio wakuu hawapatani nalo.

Uk 2;Mamake Ridhaa aliiaga dunia na Ridhaa anakumbuka jinsi mamake alivyokuwa akimwambia "Moyo wa Ridhaa ulipiga kidoko ukataka kumwonya dhidi ya tabia hii ya kike ya kulia Pindi mtu akabiliwapo na vizingiti ambavyo ni kawaida ya maisha, ukamkumbusha maisha maneno ya marehemU mama yake siku za urijali wake "

Terry na wana wake wanakumbana na janga la kifo baada ya kuchomwa wakiwa ndani ya nyumba yao. Uk 3,"uuuui!uuuui!jamani tuisaidieni!uuuui!uuuui!Mzee Kedi usituue!sisi tu majirani!maskini wanangu!maskini mume wangu!"

Tunapata pia kuwa Kangata na mkewe Ndarine wanakumbana na mauti. Uk 66; "Miaka mitano imepita. Kangata na mkewe Ndarine wameipa dunia kisogo "

74

Baada ya Lunga kuachwa na mkewe, alikazana kuwalea watoto wake lakini baadae akaiaga dunia. Uk 82;"Kabla ya mwisho wa mwaka huo, Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wake "

6. **UKOLON1 MAMBO LEO**.

Ukoloni mamboleo ni zao la uongozi mbaya. Viongozi waanzilishi wa mataifa yaliyopata uhuru hawakuzua sera na mikakati mwafaka ya kuhakikisha nchi zao zimepata kujisimamia kiuchumi.

Katika Chozi la Heri, Waafrika wenyewe wanajifanya wakoloni juu ya waafrika wenzao, ambao wako chini yao kitabaka au kisiasa kwa mfano katika ukurasa wa 5,mashamba ya Waafrika yananyakuliwa na watu binafsi baada ya wakoloni kwenda, nao waafrika wanawekwa mahali pamoja ili kuishi katika hali ya ujamaa "Lakini baba, wewe siwe uliyeniambia kuwa mashamba ya Theluji nyeusi yalikuwa milki ya wakoloni?na sasa yanamilikiwa na nani? Si mwana wa yule mlowezi maarufu ambaye wewe hunitajia kila mara? Maekari kwa maekari ya mashamba katika eneo la kisiwa bora yanamilikiwa na nani? Si yule myunani aliyewageuza wenyeji kuwa maskwota katika vitovu vya usuli wao?"

Katika ukurasa wa 24 tunapata kuwa vijana wanakufa kwa mitutu ya bunduki wanapojaribu kujikomboa kutokana na ukoloni wa Mwafrika. Walipigania uhuru wa tatu, ambao ni ukombozi kutokana na uongozi wa Mwafrika "Baada ya muda mfupi, vifua vyao vilikabiliana na risasi zilizorashiwa vifua hivyo kama marashi, vifua vikawa havina uwezo dhidi ya

Shaba, vijana wakaanguka mmoja baada ya mwingine, wame

75

kufa kifo cha kishujaa, wamejitolea mhanga kupigania uhuru wa tatu"

7. **UKOLON1 MKONGWE**.

Huu ni ukoloni uliokuwa wa Waingereza, kabla ya nchi za

Afrika kupata uhuru.

Tunapata kuwa mkoloni anapata fursa ya kuendeleza kilimo katika sehemu za mashamba ya Waafrika zilizotoa mazao mengi. Uk 7, "Mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikajia wa ardhi na Mwafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa yote yakapata wenyeji wageni dau la mwafrika likagonga jabali.

Katika ukurasa wa 7 tunasoma; "Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadogowadogo, maskini, wasio na ardhi. Nadhani unaweza kukisia hali ilivyokuwa kwa familia nyingi za kiafrika. Kama vile baba

Msumbili alivyokuwa akisema, jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambamo wazungu wangeamUa kuchukua vubarua kupalilia mazao yao"

Tunaona kuwa wazungu bado waliwatumia waafrika kama wafanyakazi mashambani 'mwao',ambayo walinyakL kutoka kwa waafrika.



## 8. **UTAMAUISH1**.

Hii ni hali ya wahusika kukata tamaa katika maisha yao au katika jambo fulani.

Wakulima wanakata tamaa baaa ya kutopata waliyotarajia baada ya kupata mazao yao. Uk 6; "Sijui ni kwanini hatujaweza kujisagia kahawa au chai yetu itakuwaje mbegu ziwe zetu, tuchanike kukuza zao lenyewe, kasha tumpelekee mwingine kwenye viwanda vyake, 2isage h%tuuzia hiyo hiyo kahawa na chai kwa bei ya kukatiha ta3

## 9. **ELIMU**.

Haya ni mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu wake. Elimu yaweza kuwa rasmi na kutolewa darasni, au iwe sio rasmi ambayo hutolewa kwenye mazingira ya kawaida yasiyo kuwa ya shuleni au darasani.

Katika ukurasa wa 10; Ridhaa aliungana na vijana wengine kwenda shuleni kupata elimu "Ridhaa alikuwa mmoja wa waathiriwa wa hali hii. Anakumbuka jinsi siku ya kwanza shuleni alivyotengwa na wenzake katika mchezo wao wa kuvuta, mchezo wa kusukuma vifuniko vya chupa ya soda kwa ncha za vidole vyao "Uk 11; "Ridhaa alipea kwenye anga za elimu, akabisha kwenye milango ya vyuo, akafika kilele cha ufanisi alipohtimu kama daktari "

Mwaliko pia anaendeleza masomo yake hadi akafikia kiwango cha Chuo kikuu. Uk 149;

" Hata alipohitimu masomo yake ya kidato cha nne na kujiunga na Chuo kikuu kusomea shahada ya isimu na lugha, M-

Wangemi na Neema walijua kuwa juhudi zao za malezi hazi



kuambulia patupu "

Mwangeka anapatikana akienda shuleni kupata Elimu. Tunaambiwa kuwa Jumamosi moja, Mwangeka alikuwa ametoka shuleni, na siku hizo walimu walikuwa wameng'ang'ania kuwafunza jumamosi wanafunzi waliokaribia 'ICU',kama walivyoliita darasa ala nane (uk 59).Mwangeka anaonekana kuendeleza masomo yake hadi Chuo kikuu na baadae kuajiriwa kazi (uk 62.)

Lunga Kiriri Kangata naye anapata elimu yake, kwani tunapata kumuona kama amri-jeshi wa uhifadhi wa mazingira walipokuwa shuleni. Tunaambiwa kuwa kila Ijumaa wakati wa gwaride, Lunga angehutubia wanafunzi wenzake na walimu kuhusu swala la mazingira (uk 67-68).

Umulkheri pia anaenda kupata elimu yake katika shule. Tunampata mwalimu wake akijaribu kumrejesha Umu darasani wakati fikra zake zinapo ondoka katika shughuli za masomo. Tunapata pia kuwa kwa hali ambayo Umu alikuwa akiishi, mwalimu mkuu wa Shule ya Tangamano, anamsajili kuwa mwanafunzi huko, kwa hisani yake na kwa ushauri wa wizara ya elimu (uk 78).Umulkheri anayaendeleza masom0

yake hadi Chuo kikuu, anapoenda ughaibuni kusomea huko (uk 128).

Mhusika Pete pia anatumika katika kuwasilisha maudhui ya elimu, ingawa elimu yake inagonga mwamba baada ya kuozwa kwa mzee mmoja aliyeitwa kuwa katika darasa la saba, wazazi wake walipomuoza kwa mzee huyu.

Baada ya Naomi kuhangaika kwa miaka mingi akiwatafuta watoto wake, anaamua kuanzisha biashara ndogo karibu na

Chuo kikuu cha Mbalamwezi, na kazi anayoifanya ni kuwapigia wasomi chapa na kuisarifu miswada yao. Kwa hivyo, tunapata kuwa maudhui haya ya elimu yanajitokeza pia, kwa kuwepo kwa Chuo kikuu (uk 193).

**IO.UONGOZI**.

Haya ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia au kuongoza shughuli fulani. Anayepewa mamlaka haya anakuwa ndiye kiongozi. Uongozi waweza kuwa mbaya au uongozi mzuri.

Tunapata kuwa watu wanachagua viongozi wanaotaka, na kampeni pia zinafanywa kwa njia ya kutupa vikaratasi ovyo ovyo. Uk 12;"Sasa ameanza kuelewa kwa nini wiki iliyopita vikaratasi vilienezwa kila mahali vikiwatahadharisha kuwa mna gharika baada ya kutawazwa kwa Msumbi ( kiongozi)

mpya.

"Siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu, hakustahili kuiongoza jamii ya Wahafidhina, kisa na maana alikuwa mwanamke, mbingu zilishuka "

II. **MAPENZI**.

Hii ni hali ya mvuto na upendo alionao mtu kwa mtu mwingine. Pia nia hisia ya upendo anayokuwa nayo mtu kuhusu mtu mwingine.

79

Ridhaa alimpenda sana mkewe Terry na wana wake.

"Polepole parafujo za mwili wake zililegea, akaketi juu ya ma.

jivu-la, juu ya miili ya wapenzi wake "

Tunapata kuwa kuna mapenzi kati ya Mwangeka na baba yake Ridhaa. Haya ni mapenzi ya mzazi kwa mwanawe, Ridhaa alimpenda sana mwanawe Mwangeka kwani ndiye pekee tu aliweza kuepukana na janga la mauti kwa familia yote yake Ridhaa. Mapenzi haya yanadhihirika wakati Ridhaa anamlaki mwanawe kwenye uwanja wa ndege anapokuwa akirudi nyumbani kutoka ughaibuni. Wanaonekana wakikubatiana kwa muda na Mwangeka kujitupa kifuani mwa babake,-

na wanashikana kukutu. Pia wanazungumza kimoyoyo kuhusu jinsi maisha yao yamekuwa; kwa kweli haya ni mazungumzo ya wapendanao (uk 46-47).

Maudhui ya mapenzi pia yanajitokeza kati ya Billy na sally. Sally alikuwa msichana ambaye Billy alichumbia hIJk0

kwao, na kisha akamleta katika nchi hii ya kiafrika ili kun-uonyesha mahali wangeweza kuishi baada ya kufunga akida. Kwa bahati mbaya, Billy anasalitiwa na mpenzi wake sally na kuambiwa kuwa jumba lenyewe ni kama kiota cha ndege, mahali ambapo yeye hawezi akaishi hata kuwe vipi (uk 80). Tunapata pia kuna mapenzi kati ya Subira na wanawe Mwanaheri na Lime. Hili linajidhihirisha baada ya

Subira kumwandikia barua mpenzi mwanawe Mwanaheri. Haya ni mapenzi ya uzazi lakini Subira anawasaliti wanawe (uk 95.)

Pia kuna mapenzi kati ya Umulkheri na wazazi wapya wa kupanga, Mwangeka na mkewe Apondi anaowapata

baadae. Mwangeka na Apondi wanampenda sana Umu ni kusema kuwa ni baraka za Mungu za kumfidia mwana wac aliyeaga dunia. Umulkheri naye anawapenda sana hawa wazazi wake wapya kwani waliweza kumlipia hafi karo. Pia waliweza kumponya uchungu aliokuwa nao moyoni wa kuachwa na wazazi wake (uk 117-118) Kuna mapenzi yanayojidhihirisha katika familia hii ya Mwangeka na Apondi, kwa wana wao. Wakati umulkheri anafikiwa na wakati wa kwenda kuyaendeleza masomo yake ughaibuni, wanamsidikisha hadi kwenye uwanja wa ndege. Mapenzi makali yanajidhihirisha wakati kila mmoja wao analia machozi kwa kuachana na Umu alipokuwa akili-abiri ndege Tumaini (uk 128). Kuna mapenzi kati ya Mwaliko na wazazi wake wa kupanga ambao ni Bwana Mwangemi na Bii Neema, ambao hawakuwa na uwezo wa kukilea kizazi chao, na hatimaye wakaamua kumpanga mwana huyu ili awe wao rasmi. Hawa wawili wa-nampenda sana Mwaliko, naye Mwaliko anawapenda kama wazazi wake halisi (uk 166-167). Naomi anawapenda sana wana wake ingawa alikuwa ame-wasaliti kwa kuwaacha wakiwa wachanga. Ameishi kuwatafu-ta walikopotelea kwa miaka mingi, lakini mwishowe, anawapa-ta wana wake bado wako hai na wamejiendeleza sana kimai-sha na kimasomo. Anawaomba msamaha huku akiwa na uchungu mwingi rohoni mwake. Wana wake wanamsamehe mwishowe kwa mapenzi waliyokuwa payor-k mama-yao (uk 192-193). c-

12. **TEKNOLOJIA**.

Haya ni maarifa ya sayansi na matumizi yake katika mitambo, vyombo na zana katika viwanda, kilimo, ufundi, au njia za mawasiliano.

Kuna matumizi ya vyombo vya habari (runinga) ambavyo ni mazao ya teknolojia mpya. Uk 12; "Katika fikra zake ambazo tangu hapo zilikuwa macho, alikumbuka taarifa ya habari kupitia kwenye runinga, taarifa ambayo japo ilitangazwa miaka minne iliyopita, ilikuwa kana kwamba anaisikiliza sasa "

Katika ukurasa wa 49 tunapata haya; "Nilipoona yaliyotokea humu kupitia kwa runinga, na mitandao mingine ya kijami; ubadhilifu wa mali, uchomaji wa watu kama makaa, msongamano na magonjwa katika kambi, kasha barua meme iliyonijuza kuhusu msiba uliotupata, niliingiwa na kihoro kisicho na kifani "

Matumizi ya runinga na mitandao ya kijamii na pia matumizi ya barua meme, ni uvumbuzi wa teknolojia katika mawasiliano.

13. **UFEMINIST1 TAASUBI YAKIUME**.

Hii ni hali ambapo mwanamke anajidhalilisha ama anadhalilishwa katika jamii. Mwanamke hapewi nafasi katika jamii, ama anajiona kuwa kiumbe dhaifu mwenye hana uwezo.

Katika ukurasa wa 16 tunasoma; "Siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu, hakustahili kuiongoza jamii ya wahafidhi



na, kisa na maana, alikuwa mwanamke.

Katika ukurasa wa 3;"Huku ni kujiumbua hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi; ulitunukiwa makoo "Bibi alikuwa akimwelezea Ridhaa kuwa unyonge haukuumbiwa 'majjmbi'ambao ni wanaume, bali uliumbiwa 'makoo',yaani wanawake. Hivyo basi tunapata kuona kuwa jamii pia iliwadhalilisha wanawake tangu zamani.

Katika ukurasa wa 8; "Mzee mwenye wake na wana wengi alihesabiwa kuwa mkwasi kwelikweli basi wake hawa hawakuchelea kutimiza amri ya

maumbile, wakapania kuujaza ulimwengu " Tunapata kuwa wanawake wanadhalilishwa kwa kuonekana kana kwamba jukumu lao kuu katka jamii ni kuijaza dunia au kuzaa wana. Mwanamke hapewi nyadhifa za umuhimu katika jamii ila tu kazi yake ni kuoleka na kujaaliwa na wana wengi awezavyo.

Katika ukurasa wa 45;"Viongozi wengi wa awali walibwagwa chini na vijana chipukizi. La kuhuzunisha ni kwamba wengi walishindwa kabisa kukubali ushinde, hasa yule ambaye alikuwa anagombea kilele cha uongozi. Kulingana naye, nafasi hii iliumbiwa mwanamume, na kupewa mwanamke ni maonevu yasiyovumilika "Katika hali hii, jamii haikukubali wanawake kuwa viongozi, bali cheo hiki cha uongozi kilikuwa cha jinsia ya uwsanaume.

Katika ukurasa wa 149; "Maisha yangu na Fugo yalikuwa kama ya ng' ombe aliyetiwa shemere na kufungwa nira pamoja na punda ambaye anakaidi kusonga. UIe unene wake, lile kituzi lililotoka kwenye makwapa yake makuza na kUfudikiza kote chumbani, ule wivu wa mke mwenzangu wa



pili, kule kukemewa na kuchekwa na watoto wa mke wa kwanza yote yalininyong' onyeza na kuniumbua. Nilichukia jaala aliyonipa mama kwa kujali maslahi yake tu, nilichukia nguvu ya maumbile iliyoniweka kwenye jinsia ya kike, nilichukia kitoto nilichohimili kwenye mji wangu hata miezi tisa ilipotimia na kupata salama, niliamua kwamba kwa mzee

Fungo hakuniweki tena.

Na unadhani anakwenda wapi?Utawezaje kujitunza wewe na mtoto wako na hali bibi yako ndiye huyo, hana hanani, na wazazi wako walafi walikuuza kwangu ili wapate pesa za kuwasomesha ndugu wako watano wa kiume?Aliuliza

Fungo "

-tukio hili linatuonyesha wazi jinsi mwanamke amedhalilishwa katika jamii.

Kwanza, mamake mtoto huyu msichana anamwoza kwa mzee mwenye wake wawili, (Mzee Fungo),ili aweze kupata pesa za kuwalipia vijana wake karo ya shule.

Msichana anaonekana kutokuwa na umuhimu ya kupelekwa shuleni ili kupata elimu, ilhali yeye mwenyewe aliazimia kuendeleza masomo yake. Maazimio yake ya elimu yanagonga mwamba baada ya kuozwa ka mzee Fungo ambaye anamtesa na mwishowe kumtaliki na kitoto kichanga.

Msicha na huyu mchanga pia anapitia machungu kwenye ndoa yake kwa kuchekwa na kudharauliwa na wake wenza'-

na wana wao.

Katika ukurasa wa 154;"Mlaani shetani' Sauna aliuambia



moyo wake, 'unajua kuwa mimi sikuumbiwa ujalaana, walimwengu ndio walinifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari. Fikiria u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kisha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba Chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna hata uso wa kumtazamia yeyote, wala kinywa cha kumwambia mamako kuhusu feli uliyotendewa. Na utamwambiaje mja huyu ambaye daima ni mwanamke taa, atakalo baba yeye huliridhia bila swali, na ikitokea kwamba atauliza swali, anakuwa mpokezi wa makonde, vitisho na matusi?Hebu yatie haya kwenye mizani; baada ya mwezi mmoja unaanza kushikwa na kisulisuli, kichefuchefu cha asubuhi nacho kinakuandama. Fikra zako za kitoto

zinakutuma kuwaza kuwa ni malaria au homa ya matumbo. Unamwambia mama yako ambaye anaonekana kushtuka kiasi. Mama anapokupeleka hospitali, anapasuliwa mbarika, nawe limbukeni hujui lolote. Mnapofika nyumbani, anakuhoji, nawe hujui kuficha lolote, unamwambia imekuwa mazoea baba yako kukuhujumu kila apatapo nafasi '

"Hili haliwezi kukubaIika!Kujipagaza uzazi na ulezi katika umri huu, tena mzazi mwenzio si mwingine, ila baba yako?'Tukio hili la kufadhaisha linatendeka kwa kumdhalilisha mwanamke. Tunaona kuwa mamke Sauna hana uhuru wa kuzungumza kwake, wala kuuliza maswali, na iwapo ameuliza swali, inakuwa ni vita au kichapo kutoka kwa mumewe.

Sauna naye anadhalilishwa kwa kubakwa na babake mzazi, wala sio mara moja. Hatimaye anapata mimba ya babake mzazi. Jambo hili linamdhalilisha sana Sauna hivi kwamba heshima yake yote inapotea, na hawezi kuzungumza

na mama au baba yake.

14. **UMENKE**.

Ni hali amababpo mwanamume hapewi nafasi katika jamii. Mwanamume amedhalilisha katika jamii na nafasi yake haitambuliki.

Katika Riwaya tunapata haya;"Haiwezekani!hili haliwezekani!Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike-yule anayesimuliwa katika visakale vya majirani wetu -

Kumbuka jinsi katika enzi hiyo ya kiistimari wanaume walivyotumikishwa!si Sisi tuliokuwa tukitifua udongo mashambani huku wanawake kama majeta wanakaa na kututumikisha?"Uk 17;"Fikiria suala la jinsia 'Na usidhani ni jinsia nyingine, ni dada zetu tu. Vyombo wa habari na vikao vya wapigania haki vinapigania elimu ya mtoto wa kike, haja ya kuwainua akina mama kiuchmi, hukumu ya kifo kupitishwa dhidi ya mwanamume, hata muewme atakayepatikana na kosa la kumbaka mke wake.

Uk 20 "Nakumbuka asubuhi ya pili baada ya mtafaruku kuanza. Nilikuwa sebuleni na wanangu tukitazama runinga. Mara nikaskia; 'Hakuna Amani bila kumheshimu mwanamume. Hatuwezi kukubali haya. Hata mizimu itatucheka!'

15. **SHERIA**.

Hizi ni kanuni zinazotungwa na jumuiya fulani kwa mfano bunge au jamii fulani ili kuratibu shughuli za jumuia inayohl-Isika, na adhabu Pindi kanuni hizo zikikiukwa.

Uk 20; "Wengine waliokuwa jasiri walidiriki kuingia kwenye maduka ya wafanyabiashara wa kihindi, kiarabu na hata Waafrika wenzao, wakapora walichoweza kabla ya kukutana na mkono mrefu wa utawala "

Uk 82,tunapata kuwa Umulkheri anaenda kwenye kituo cha polisi kupiga ripoti kuhusu kupotea kwa ndugu zake Dick na

Mwaliko.

Jambo linatuonyesha kuwa kuna sheria ambayo inafuatwa na raia, na pia kwa uwepo wa kituo cha polisi "Mimi ni Umulkheri

Lunga. Ninasomea Shule ya Upili ya Mtende. Nimekuja kutoa taarifa kuhusu kupotea kwa nugu zangu Dick na Mwaliko'alisema umu huku amemkazia macho askari wa zamu, kwa kuhofia kutosikika" Uk 22,Wananchi wanaahidiwa kuwa wale ambao walipata mali ya uma kwa njia isiyo halali watapambana na mkono dhabiti wa sheria "Waliogawiwa au kununua mali ya uma kwa njia za udanganyifu watakabiliana na mkono mrefu wa sheria "

Uk 158, Bi. Kangara na Sauna wanatiwa mbaroni kwa kufanya biashara haramu "Polisi walipopashwa habari kuhusu maficho ya Bi. Kangara, walishika tariki moja kwa moja hadi nyumbani kwake ambako waliwatia mbaroni Bi. Kangara na

Sauna, mabibi hawa walifikishwa mahakamani na kushtakiwakwakosalaukiukajiwahakizawatoto, wakarambishwa miaka saba gerezani na kazi ngumu "

87

16. **UONGOZI MBAYA**.

Hayanimaudhuiyanayojitokezawakativiongozi wanapofanya shughuli zao za uongozi kwa njia isiyofaa. Haya husababisha kuteseka kwa wanajamii au raiya wakawaida.

Uk 21; "Maeneo-gatuzi yenu yanahitaji mabarobaro kama nyinyi kulisukuma gurudumu la maendeleo'.Hapa ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule wlikotoka, wakapewa maelfu na maelfu ya ekari, wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwa makubwa huku wakidaikuwaninjiayakuwahakikishiawenyejihali ya kujitosheleza kwa chakula. Kumbe wanakuja kutufukarisha Zaidi!Tunapolalamika kashafa za unyakuzi wa hata vikata vidogo tulivyo navyo, tunapozwa roho kwa, tumeunda tume ya kuchunguza kashfa hii. Waliogawiwa au kununua mali ya uma kwa njia za udanganyifu watakabiliana na mkono dhabiti wa sheria; Ni wazi kuwa mwanainchiwakawaidahadirikikuzionaripotiza tumehiziautusemeripotihizihuwawageniwarafu za makavazi yakitaifa!"

Tunapatakuwauongoziuliopo ni wakuwanyanyasa raiawakawaidakakunyakuamashambayao,na kuahidi kuwa kuna tume za kushughulikia mambo hayo, ilhali haziko.

17. **UOZO WA MAADILI YA JAMII**.

Hiinihaliambapomaadiliyajamiiyamepunguka kwa kiasi kikubwa, na hivyo mambo yanayofanywa katikajamiihiY0siyakukubalika.Tazamamifano michache ifuatayo ya uozo

88

huu.

Ubakaji.

Hilinijamboambalolimepatikanakatikajamiina husababishwa na ukosefu a maadili mema ya wanajamii. Katika ukurasa wa 25 tunasoma; "Kisha genge hili la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti zangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa. Nilijaribu kwa jino na ukucha kuwaokoa lakini likawa suala la mume nguvuze!Mahasimu hawa walitekeleza unyama wao nakuniachabilakunigusa,niuguzemajerahaya moyo " Wasichana hawa wawili walibakwa hadharani huku baba yao akitazama bila uwezo wa kuwasaidia.

Ulanguzi wa dawa za kulevya.

TunapatakuwaDickanaifanyakaziyakusafirisha dawa za kulevya kutoka nchi moja hadi nyingine, na hii ni biashara ambayo inafanywa na vijana wengi, na kuwafanya wengine kuingia kwenye mtego ya polisi nakuelekeakutumikiakifungochaogerezani.Uk 119;120. "Siku hiyo kiwewe kilikuwa kimemkumbatia kwani kazi ya kubeba dafina'kama walivyoiita biasharaharamuambayokalazimishwakufanyasiku hizo, ilikuwa imewaingiza wengi kwnye nyavu na madema ya polisi, wakatiwa mbaroni "Dick amesafirisha maelfu kwa maelfu ya vifurushi vya dawa hizi. Mwanzoni hakuwa mraibu

Wadawahizilakiniilibidiajizoeshe,kwausalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi ilibidi kuzimeza dawazenyeweilikwendakuzitapikakwenyemasoko ughaibuni "

Uporaji, wizi na ukatili.

Haya ni matendo ya kuchukua mali au milki ya mtu mwingine

89

nakutakakuimilikibilaidhininakwanjiayamabavu.

Tunapata kuwa mali ya watu binafsi yanaharibiwa, kwa mfano nyumba na mali yote ya Ridhaa yanateketezwa, wakiwemo watoto wake na mkewe pia.

Pia, mali ya wananchi kama mashamba yananyakuliwanawanaachwabilachochote.

Katika ukurasa wa 25,tunapata kuwa mabarobaro wanavamia watu na kuwafanyia unyama, "Kabla hajajibu lolote, alikuwa amekula mikato miwili ya sime, akazirai kwa uchungu "

Uendelezaji wa biashara haramu.

Bi. Kangara walifanya baiashara haramu ya kuwauza watoto na vijana. Uk 157;

"Safari yake ilipata mkondo mwingine baada ya polisi kupata fununu kuhusu njama ambazo yeye na Bii Kangara walikuwa wakiendesha. Mabibi hawa walikuwa na mtandao ambao kazi yake ilikuwa kuwauza watoto na vijana "uk 84;

"Sauna alikuwa Chui ambaye hakupigwa na mshipa kujifanya mwema kwa waajiri wake ili aaminiwe, naye apate fursa ya kuwaiba watoto na kuwapeleka kwa bibi mmoja ambaye aliwatumia ka biashara ya nipe nikupe, na katika ulaguzi wa dawa za kulevya " Uk 151; "Zao la muungano huu lilikUWa kuzaliwa kwa mwanangu wa pili. Huyu yumo mtaa wa Sinyaa ambako nilikuwa ninaishi baada ya kupigwa putwe na Nyangumi, mkewe wa halali amemrudia. Analelewa na ndugu yake lnabidi hali iwe hivi kwani Sina pesa za kumlipia kijaka

90

zi, na vinywa hivi viwili lazima vilishwe. Na usidhani hata kitoto hiki Cha pili sikujaribu kukiangamiza. Kwa kweli ukaidi wa kijusi chake ndio mwokozi wacho.

Mwishowe nilimwendea daktari ambaye, badala ya kunisaidia, alikilaani kitendo changu na kuniambia kwamba nisimtie katika majaribu "

Uk 151;"Hiki kilichonilaza hapa nacho kina roho Zaidi ya saba. Ni kijalaana ambacho nilikiokota katika shughuli za uuzaji pombe. Nadhani mmoja kati ya walevi waliozoea kuja kwenye baa nilimoajiriwa kuuza pombe aliniwahi nishai zikiwa zimenilemea, yakatokea ya kutokea, akaniachia ujira wangu wa kuafriti hiki "

Uavyaji mimba.

Tunapata kuwa uavyaji wa mimba ulikuiwa umekidhiri sana, -

na hili ni jambo lisilokubalika katika jamii na pia katika maandiko matakatifu.

Msichana huyu (Sauna) anapata mimba kiholela na kujaribu awezavyo kuiavya, na mwishowe, baada ya kushindwa kuavya mimba, anaamua kujiua. Katika ukurasa wa shetani' Sauna aliuambia moyo wake, 'Unajua kuwa mmi

Sikuumbiwa ujalaana, walimwengu ndio walinifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari. Fikiria u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kasha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba Chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna hata uso wa kumtazamia yeyote, wala kinywa cha kumwambia mamako kuhusu feli

Uliyotendewa. Na utamwambiaje mja huyu ambaye daima ni mwanamke taa, atakalo baba yeye hiliridhia bila swali, na ikitokea kwamba atauliza swali, anakuwa mpokezi wa makonde, vitiShO na matusi?Hebu yatie haya kwenye miza

91

ni; baada ya mwezi mmoja unaanza kushikwa na kisulisuli, -

kichefuchefu cha asubuhi nacho kinakuandama fikra zako za kitoto zinakutuma kuwaza kuwa ni malaria au homa ya matumbo. Unammwambia mama yako ambaye anaonekana kushtuka kiasi. Mama anapokupeleka hospitali, anapasuliwa mbarika, nawe limbukeni hujui lolote. Mnapofika nyumbani, anakuhoji, nawe hujui kuficha lolote, unamwambia imekuwa mazoea baba yako kukuhujumu kila apatapo nafasi '

"Hili haliwezi kukubalika!Kujipagaza uzazi na ulezi katika umri huu, tena mzazi mwenzio si mwingine, ila baba yako?"

Mapenzi kati ya baba mlezi na bintiye.

Babake Sauna anafanya mapenzi na mwanawe apatapo nafasi, na mwishowe, Sauna anapata mimba. Hili ni jambo ambalo halijakubalika katika jamii na pia ni jambo la kufadhaisha sana na lenye kuleta laana. Mbele ya Mwenyezi Mungu, ni jambo linalofaa pigo kubwa sana na hata mauti.

Jambo hili lindhihirisha uozo wa maadili ulioko katika jamii na umefichika sana.

Kutupwa kwa watoto wachanga

Katika ukurasa wa 162 tunasoma hapa ameokotwa na binti huyu kwenye jaa la taka, 'alisema askari, 'Huenda akataka kukueleza kadhia yenyewe, 'akaongeza "Asante sana

Neema, kwa utu wako, 'akasema mtawa huyu, 'Kitoto hiki kimepata kwao. Hapa, tutakiita Nasibu, Nasibu Immaculata -

Najua itatokea familia hitaji itakayokuja kumpanga kama mwanao "

Hili linatudhihirishia jinsi jamii imekuwa na mazoea ya kutupa wu ovyo ovyo bila kujali kuwa hao ni



binadamu. Haswa wasichana wadogo wanapopata mimba bila ya kujipanga, wakishindwa kuavya mimba, wanaelekea kukitupa kitoto hicho kichanga punde tu baada ya kujifungua.

18. **DIN1**.

Hii ni imani inayohusiana na kuwepo kwa Kiumbe mwenye nguvu Zaidi kuliko viumbe wengine (Mungu).

Haya ni maudhui yaliyojitokeza kwenye kitabu hiki kwa njia zifuatazo;

Katika Uk 31 tunasoma, "Shirika la makazi bora lilikuwa limejitolea kuja kuwajengea wakimbizi nyumba bora. Misikiti na makanisa nayo yalikuwa yamekusanya magunia ya vyakula kuwalisha wahasiriwa wa hali hii ya tandabelua; ...sote tulikaa tukitunga macho barabarani tukisubiri jinsi waumini wanavyoambiwa wasubiri kuja tena kwa Masiya"

Pia katika Uk 32 tunasoma kuwa, "Nilikumbuka kifungu kimoja katika sala za waumini(wakati nilipokuwa nikihudhuria ibada),kilichosema, ninawapa Amani mani yangu nawaachia"

19. **UFISAD1**.

Huu ni utumiaji mbaya wa mali ya uma. Pia ni ubadhilifu wa mali ya serikali au chama.

Katika Uk 41 tunapata kuwa kuna tume za kupigana na ufisadi ambazo zinaundwa, na jambo hili ni ishara kuwa kuna ufisadi unaoendelezwa "Je, ni tume ngapi za kuchunguza kashfa za kifisadi ambazo zimeundwa?Hizo si juhudi za kupigana na ufisadi?"



Pia katika uk 13,"Uchukuzi wa milungulu pia ni aina ya ufisadi katika serikali "Wengine walionekana wakitoa milungulu hadharani, wengine wakatishia kuishtaki wizara husika kwa kile walichokiita ukiukaji a haki za umiliki mali "

20. **DEMOKRASIA**.

Huu ni mfumo wa utawala ambao viongozi wake huchaguliwa kwa njia ya kupiga kura.

Katika ukurasa wa 19 tunasema, "Viongozi wenyewe baada ya kupiga kura, walijikalia makwao, na kuendelea kuwatazama masabaha wao kwenye runinga wakiendelea kuzozana!"

21. **MABADILIKO**.

Hii ni hali ambapo mambo yanaenda kinyume na jinsi yalivyokuwa yakienda mbeleni.

Hali ya kufanya mambo inabadilika na kuwa tofauti ya kawaida yake.

Katika ukurasa wa 10; "Hatua ya mkoloni ya kupuuza sera za

Mwafrika za umiliki wa ardhi, na kuamua kujumuisha pamoja ardhi iliyomilikiwa na mtu binafsi, na kuidhinisha umiliki hut-I kwa hati miliki, ilivuruga mshikamano wa kijamii. Katika sera ya kijadi ya umiliki na matumizi ya ardhi, raiya wote, hata wageni, walikaribishwa na kugawiwa mashamba, hiW0

kupata mbinu ya kuyaendeshea maisha. Sera mpya ya umilikaji nafsi wa ardhi ilimaanisha kwamba wale waliokosa pesa za kununulia mashamba wangekosa mahali pa kuishi. Na hata wale waliobahatika kuwa na pesa za kununulia mashamba daima walichukuliwa kama wageni wasiopasa kuaminiwa

Tunapata kuwa mfumo uliokuwepo hapo awali wa kumiliki mashamba barani Afrika ulipigwa marufuku na kukawa na mfumo mpya wa umiliki wa mashamba uliohusisha kupewa kwa hati miliki. Haya ni mabadiliko yanayokuja katika jamii. Katika ukurasa wa ll; "Pengine hata ni mzaha tu. Kesho nitakurudisha shuleni. Nitazungumza na mwalimu Hi awaelekeze

Zaidi 'Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha ya heri kwa

Ridhaa. Baada ya mwalimu kuzungumza na wanafunzi na kuwasisitizia umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano dhihaka na masimangoyaliisha "Kuna mabadiliko yanayofanyika katika shule baada ya mamake Ridhaa kuzung umza na mwalimu wake kuhusu umuhimu wa kuwajuza wa nafunzi ushirikiano na kuishi kwa umoja. Mabadiliko haya yanakuwa ya maana sana kwa Ridhaa kwani elimu yake inaendelea kwa ufasaha na anahitimu hadi chuo kikuu. Katika ukurasa uo huo wa 11 tunasoma; "Mimi binafsi nimefanya juu chini kuhakikisha kuwa kijiji kizima kimepata maji ya mabomba. Eneo ambalo awali likiitwa Kalahari, sasa limetwaa rangi ya chanikiwiti. Miambakofi, mivule na miti mingine mingi imepandwa. Mvua inanyesha majira baada ya mengine "Haya ni mabadiliko yanayofanyika katika mtaa huu ambao ulikuwa hapo awali umekauka sana lakini baada ya maji ya mabomba kufikishiwa watu, tunapata kuwa kunabadilika na ile hali ya kuwa jangwa inaisha, miti mingi inapandwa na hata mvua nyingi kunyesha. Katika ukurasa wa 84, "Maisha ya Umu yalichukua mkondo mpya. Siku ile baada ya kuwapigia polisi ripoti, ilibainika kuwa wanuna wake walikuwa wametekwa nyara na Sauna "

9S

Maisha ya Ridhaa pia yanachukua mkondo mpya au kubadi.

lika wakati familia yake inapoangamia kwenye janga la moto, na mali yake yote kuishia hapo. Maisha yaliyokuwa ya furah pamoja na familia yake yanabadilika na kuwa uchungu mtupu na kilio cha kufiwa na wapenzi wake.

Katika ukurasa wa 40 tunasoma; "Ridhaa:

Na nani akasema viongozi waliopo hawajajikuna wajipatapo? Huoni hata wahasiriwa wa magonjwa sugu kama vile iri na hata UKIMWI wana dawa za bei nafuu za kuwawezesha kudhibiti hali hizi? Je, serikali haijaanzisha sera ya elimu bila malipo kwa Shule zote za msingi? Haijagharamia karo za Shule za kutwa katika Shule za upili? kumbuka pia na ule mradi wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi kuanzia darasa la kwanza ana kipakatalishi chake? Ushaona? Hivi karibuni, nchi inafikia ile vision 2030 hata kabla ya

2030 yenyewe! Je, ni tume ngapi za kuchunguza kashfa za kifisadi ambazo zimeundwa? Hizo si juhudi za kupigana na ufisadi?"

Maelezo haya yote yanatuonyesha jinsi taifa limepiga hatua mbele kimaendeleo. Kumekuwa na mabadiliko mengi sana katika serikali na pia hali ya maisha ya raia, bila kusahaU elimu.

Katika ukurasa wa 63 tunasoma; "Usicheze na binadamU apatapo nyenzo ya kujiinua! kabla ya miaka miWili kuisha, mahali hapa palikuwa pameb. Maa sura mpya-majumba yenye mapaa ya vigae, misitu ya mihindi na miharage, maduka ya jumla, viduka vya rejareja almuradi kila mtu alijifunga mkaja



kutunisha kibindo chake; kufidia alichokuwa amekipoteza hapo awali "Haya ni mabadiliko yanayoendelea katika msitu wa Mamba. Tunaambiwa kuwa msitu huu uligeuka na kuwa nyumbani mwa maelfu ya watu waliogura makwao bila tumaini ya kurudi. Maduka na majumba yanajengwa, na ile hali ya kuwa msitu inabadilika, na mashamba ya watu ndiyo yanayoonekana kwa sasa. Pia katika ukurasa wa 148 tunasoma; "Maisha yangu yalichukua mkondo mwingine nilipojiunga na darasa la saba. Ka tika jamii yangu, inaaminika kuwa msichana akishaisha kupashwa tohara, ameingia utu uzimani, hivyo ataipaka familia yake tope ikiwa ataendelea kuozea kwao bila mume "

22. **UHARIBIFU WA MALI NA MAZINGIRA**.

Assumpta K.Matei amejikita katika maudhui ya uharibifu wa mazingira na pia mali ya watu binafsi. Katika ukurasa wa 20 tunasoma; "Nchi ya Wahafidhina ilitwaa sura mpya. Misafara kwa misafara ya watu waliohama kwao bila kujua waendako ilizipamba barabara na vichochoro vya Wahafidhina. Mizoga ya watu na wanyama, magofu ya majumba yaliyoteketezwa kwa moto, na viunzi vya mimea iliyonyong'onyezwa na moto ilijikita kila mahali; uharibifu wa mali na mazingira ukashamiri "

Katika ukurasa wa 20 tunapata; "Mara hali ilibadilika, nikaona wote wameyazingira magari barabarani na kuanza kuyawasha moto kana kwamba wanayachoma rtiabiwi ya

taka!...Magari yaliwaka moto bila kujali kilichomo ndani "

Matukio haya yanatuonyesha jinsi mali ya watu binafsi ilivyoharibiwa na vijana, kwa kuteketezwa moto.

23. **UJAALA**.

Haya ni maudhui ambayo huhusisha mambo yanayofanyika kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Binadamu hana uwezo wa kuyabadilisha mambo haya, na hayezi kuyaepuka kwa njiayoyote ile. Assumpta K.Matei ametumia mauidhui haya katika kazi yake ya fasihi kwa njia hizi;

Katika ukurasa wa 8 tunasoma;

"Ridhaa hakuwa mkazi asilia wa msitu wa Heri. Alikuwa

'mfuata mvua',kama walivyoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki. Hakupachagua mahali hapa, majaaliwa yalitaka, na majaaliwa yana nguvu!"

Ridhaa hakujichagulia kuishi kule, ila alijikuta humo kwa nguvu zake Maulana ambazo haziwezi kuepukika.

Katika ukurasa wa 128 tunasoma; "Hata waliposikia kwa mbali sauti ikitangaza kuwa abiria wanaoabiri ndege Tumaini waanze kuingia, walijua jaala ilikuwa imewakutanisha, kwamba hawatawahi kutengana tena "

Haukuwa uwezo wao kukutana, ila tu ni kwa uwezo wake

Mungu.

## 24. **UTAMADUN1**.

Hizi ni mila, desturi, asili, Imani na itikadi za watu fulani au jamii fulani.

Lazima watu hawa ama jamii hii ifuate mila zake, ili kila mmoja atambulike kuwa mmoja kati ya hao watu ama wanajamii.

Katika ukurasa wa 8 tunasoma; "Unajua zama hizo hali ilivyokuwa! Mzee wenye wake na wana wengi alihesabiwa kuwa mkwasi kwelikweli. Basi wake hawa hawakuchelea kutimiza amri ya maumbile, wakapania kuujaza ulimwengu!"

Ulikuwa ni utamaduni wa kiafrika kuoa wanawake wengi, na kuwa na familia kubwa uwezavyo, na kwa hayo, unakuwa mtu wa kuheshimiwa, na kuhesabiwa kati ya wakwasi wa jamii hiyo.

Hii ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli aidha za kikazi, ili kuafikia lengo moja sawa.

Katika ukurasa wa 9 tunasoma; "Ilipotokea kwamba kulikuwa na upungufu wa ardhi katika eneo Fulani, watu wangehama na kuishi na watu wa ukoo mwingine. Lilikuwa jambo la kawaida kuwapata watu wakiishi na kulima katika mashamba ya majirani, marafiki na jamaa. Baada ya kuyalima mashamba haya kwa muda, yaliishia kuwa yao. Hawakuhitajika kuyanunua kama wanavyofanya sasa "

Tunapata kuona kuwa nyakati za hapo awali, kulikuwa na ushirikiano mkuu katika jamii, na kila mtu aliishi kwa udugu na mwenzake, wakafanya kazi pamoja, wakaishi pamo



ja, wakalima mashamba pamoja, na hivyo basi, ufanisi ukawa mkubwa sana.

## 26. **UTABAKA**.

Hii ni hali ya kuwa na kundi fulani katika jamii linalotofautiana na kundi lingine katika jamii iyo hiyo, kwa misingi ya kiuchumi, kielimu na kadhalika. Utabaka mara nyingi hujitokeza wakati kunapopatikana matajiri na masikini katika jamii. Pia kuna matabaka ya wasomi, wafanyakazi, wafanya biashara, na kadhalika.

Katika ukurasa wa 14 uliopo ni ule wa hali, mazoea na silika. Hapa tulipo tupamwe na wamwe na walokuwa nacho na wachochole. Unaweza kusema kuna kiasi

Fulani cha usawa watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni! KiIe ambacho hawajuia ni kwamba hata katika kifo, hamna usawa. Pana tofauti kati ya mandhari wanamofia. Kuna wanaokufa wakipewa na wauguzi katika zahanati za kijiji. Wapo wanaolala maumivu yao yakiwa yamefishwa ganzi kwenye hospitali za kifahari, wakiliwazwa na mashine, kila mmoja akihimiza wenzake kuushikilia kukutu uhai wa mheshimiwa huyu. Hawa wafapo sura zao huwa tulivu; wameziachilia huru roho zao kwa faraja. Huwezi kuzilinganiSha nyuso zao na za wanaokufa kwa hamaniko wakizingirwa na jamaa ambao hawana hata hela za kununulia sindano ya kuingiza dawa mwilini! Kuna wale ambao hufia kwenye vitanda vya mwakisu vitongojini baada ya kupiga maji haramu. Hawa husemekana kuwa wamekuwa nzi ambao hufia dondani sio hasara. HuIaumiwa kwa kujitosa katika msiba wa kujiW kia. Tofauti hizi zote unazijua. Unajua pia kuna tofau hata katika mitindo ya mazishi, viviga vinavyohusishwa na sherehe



za mazishi na hata mavazi ya "mwenda zake" na wafiwa. Hata majeneza yenyewe huhitilafiana!"

Kuna matabaka mawili yaliyoangaziwa sana hapa, yale ya walala hoi, na walala heri.

Matabaka haya mawili yanatofautiana sana kihali, na jinsi ya kufanya mambo yao.

27. **UTALA**.

Hii ni hali ya mume mmoja kuwa na wake wengi, au Zaidi ya wawili.

Hali hii inapatikana sana katika jamii za waafrika, na mzee huheshimiwa akiwa na familia kubwa Zaidi na wana wengi. Mtala ni mmoja wa wake wengi waliooleka kwa mume mmoja.

Assumpta K. Matei anajikita katika maudhui haya kama tunavyo ona kutokana na mifano ifuatayo.

Katika ukurasa wa 7 tunasoma; "Baba yake yasemekana alikuwa na wake kumi na wawili. Unajua zama hizo hali ilivyokuwa! Mzee mwenye wake na wana wengi alihesabiwa kuwa mkwasi kwelikweli "

Katika ukurasa wa 148 tunasoma; "Wajomba zangu hawakuchelea kupokea posa na baadaye mahari kutoka kwa buda mmoja ambaye alinioa kama mke wa nne "

Katika ukurasa wa 151 tunasoma; "Zao la muungano huu lilikuwa kuzaliwa kwa mwanangu wa pili. Huyo yumo mtaa wa

Sinyaa ambako nilikuwa ninaishi baada ya kupigwa pute na

Nyangumi, mkewe wa halali amemrudia "



Kutokana na hali hizi tofauti, tunapata kuona kuwa jambo la wanawake kuoleka kwa bwana mmoja lilikuwa limekithiri sana katika jamii.

28. **MALEZ1**.

Hii ni hali ya mzazi kumlea mtoto aliyemzaa au hata wa kupanga.

Katika riwaya hii, swala la ulezi limejikita sana katika hali tofauti. Kunao wazazi ambao wanawalea wana wao kwa njia inayofaa, wengine baada ya kuwazaa wana wao, huwatupa kwenye majaa ya taka ili waage dunia. Kunao wengine ambao baada ya kujifungua, na kutopata haja ya kuwa na malaika huyo, wanaamua kumtupa langoni la nyumbani mwa watoto wasiokuwa na wazazi ili mwana huyu aweze kutelekezwa na kulelewa huku na wasamaria hawa wema.

Kunao wazazi wengine ambao wanawalea wana wao katika hali ya umaskini, lakini baadae, watoto hawa wanakuwa ndio wa kuwasaidia wazazi wao.

".Lunga ilibidi kuwa baba na mama wa watoto wake, na hi10

usilione kama jambo jepesi, Hakuwaacha watoto wake kama alivyofanya mkewe Naomi'

Tunapata kuwa kuna kina mama wengine ambao wanawaa chia kina baba watoto ili wawalee. Haya ni malezi mabaya kutokana na wazazi wa kike.



**MASWALI YA MARUDiO**

*1. a) Ujaala ni nini (alama 2).*

*b) Kwa kutoa mifano kutokana na riwaya hii, eleza jinsi ujaala umejitokeza katika jamii (alama 10).*

*2. Jadili maudhui haya kama yanavyo jitokeza katika riwaya ya*

*Chozi la Heri (alama 20.)*

*a)Utamaduni.*

*b)Demokrasia.*

*c)Mapenzi.*

*d)Teknolojia.*

*3. Elimu ndiyo nguzo ya maendeleo katika kila jamii. Elimu pia imesababisho mabadiiko mengi katika jamii. Kwa kurejelea riwaya hii, jadifi kaui hii inoyohusiana na elimu (alama 20).*

*4. Janga la mauti au kifo limewaadhiri wahusika kadhaa katika riwaya hii. Kwa kurejelea wahusika kadhaa, eleza jinsi mauti yameadhiri kupitishwa kwa maudhui na mwandishi (alama 20).*

*5. Thibitisha jinsi maudhui ya ukoloni mkongwe na ukoloni mambo leo yanavyojitokeza katika riwaya hii ya Chozi la*

*Heri (alama 20).*

*6. Ufeministi ni hali ya mwanamke kudhalilishwa katika jamii. Kwa kutolea mifano kutoka kwa riwaya hii, eleza jinsi ufeministi ulivyokidhiri katika jamii ya mwafrika (alama 20).*

*7. Kwa kutolea mifano kutokana na riwaya hii, eleza jinsi*



*marizi yanavyofaniw- a no wazazi wengl atika faro ra amo 1 r 8. Kama walivyosema waswahili, umoja ni nguvu, utengano udhaifu; tetea kauli hii, huku ukiangazia riwaya ya Chozi is Heri (alama 20.) 9. Utala ni swala ambalo limejitokeza sana katika jomii za Kiafri-ka. Kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri, eleza umuhimu no udhaifu wa utamaduni huu (alama 20). 10. "Bila shako hill ni zoo lingine la husuda " Kwa kurejelea riwaya hii, elezea jinsi husuda ilileta balaa kwa wanajamii waj nchi hii ya kiafrika (alama 20).*

## *8.* WAHUSIKA NA UHUSIKA

Mhusika ni mtu katika riwaya au hadithi fulani anayetenda mambo kadha wa kadha, kadri mtunzi wa hadithi au riwaya atakavyo, ili kujenga hadithi yake. Wahusika hutumika kuafikisha maudhui ambayo mtunzi anataka kupitisha kwa msomaji. Kila mhusika huwa na sifa na umuhimu wake katika kazi hii ya ubunifu ya mwandishi.

### I. **RIDHAA**.

Huyu ni mumewe Terry. Ni mhusika mkuu ambaye ana sifa kadhaa.

**SIFA**

(a) Mshirikina.

Uk 1,"Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama. Milio hiyo ndiyo iliyomtia kiwewe zaidi kwani bundi hawakuwa wageni wa kikaida katika janibu hizi "

Pia anamwambia mkewe Terry, "milio hii ni kama mbiu ya mgambo, huenda kukawa na jambo"

Kwa hivyo Ridhaa ni mhusika aliyekuwa na imani katika mambo ya ushirikina. Uk 2 "Ninashangaa vipi daktari mzima hapo ulipo unajishughulisha na mambo ya ushirikina"

Huu ni ushahidi mwingine wa kuonyesha kuwa Ridhaa alikuwa mshirikina.

(b) Mwepesi wa moyo.

Ridhaa ni mwepesi wa moyo kwani anapopatwa na mawazo ya hapo awali ambayo ni ya kukatisha tamaa, analia kwa urahisi, kinyume na matarajio ya jamii kuwa mwanaume hafai kulia.



UK 2,"machozi yaliturika uwezo wake wa kuona " Uk 3 "Ridhaa mwanangu, mwanamume hufumbika chozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabalia ya maisha. Huku ni kujiumbua hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi, ulitunukiwa makoo" (c) Mwenye bidii. Uk 4,"Alikuwa amesafiri kwa shughuli za ujenzi wa taifa, ka-ma alivyoziita safari zake za kikazi" Tunapata kuwa Ridhaa alikuwa

ni mwenye bidii za mchwa katika kazi yake ya kila siku aliyoiita 'ujenzi wa taifa'. (d) Mvumilivu. Aliweza kuvumilia matukio yaliyomkumba kijijini mwake, ya-kiwemo kutotakwa huko, na kufukuzwa, mali yake kuharibiwa na familia yake kuuliwa. Anapiga moyo konde kukabiliana na hall hiyo mpya (uk 25). (e) Mwenye busara. Ridhaa anapozisikia sauti za hawa ndege, anajua kuwa kuna jambo ambalo lingeweza kutendeka na ambalo si la kupende-za. Pia anamwambia mkewe, uk 2,"wewe endelea kupiga hulu tu, lakini utakuja kuniambia " Baadaye tunapata kuona kuwa kuna janga linaloipata familia yake na kwa hivyo, Ridhaa alikuwa na uwezo wa kuhisi kuwa kuna jambo lisilokuwa la kupendeza litakaloifikia jamii yake 2. TERRY Huyu ni mkewe Ridhaa. Aliangamia katika mkasa wa moto.

(a) Mcheshi

Terry ana sifa moja kuu ya kuwa yeye ni mcheshi.

Uk 2 "Terry kwa ucheshi wake mwingi wa kawaida, hakunyamaza "

Tunaona kuwa ucheshi ulikuwa ni mazoea yake au kawaida yake.

(b) Mwenye busara.

Anamwambia mumewe, (uk 2) "wewe huishi kufanya tumbo moto!Kila jambo kwako lazima liwe na kiini utakuja kujitia fadhaa bure

Anajaribu kumpa ushauri mumewe baada ya kumwona mumewe kuwa mshirikina.

(Terry anaiaga dunia pamoja na wanawe, baada ya nyumba yao kuteketezwa)

**3.MZEE KEDI**.

Huyu ni jirani yake Terry na Ridhaa.

Anaonekana kuwa muuaji.

Uk 3,"Uuuui!uuuui!Jamani tusaidieni!Uuuui!Uuuui! Mzee

Kedi, usituue, sisi tu majirani!Maskini wanangu!Maskini mume wangu!"

Huyu ni mwanawe Ridhaa. Anapatwa na janga la moto na kuiaga dunia pamoja na mamake. Jina lake kamili lilikuwa

Alionekana kuwa na sifa ya kuwa mwana mwerevu sana. Ba



ba yake anakumbuka jinsi walivyokuwa wakijadiliana vikali kuhusu mafanikio ya baada ya uhuru, uk 5,"Anakumbuka mjadala mkali aliokuwa nao na bintiye, Tila, kuhusu mafanikio ya baada ya uhuru, mjadala ambao hakuna mmoja katika aila yake aliyethubutu kUuchangia kwani kwenye maswala ya sheria na siasa, hakuna aliyempiku

Tila "

5. **BECKY**.

Huyu ni mjukuu wake Ridhaa.

Yeye pia anajipata katika janga la moto na kuiaga dunia.

6. **MZEE MWIMO MSUBILI**.

Huyu alikuwa babake Ridhaa.

-Alikuwa na familia kubwa, yenye madume ishirini; uk

7. Ridhaa akiwemo kati ya madume hao ishirini.

-Alikuwa mwenye busara, kwa sababu alihamisha familia yake msitu wa heri, ili kupunguza msongamano nyumbani pake.

-Ni mwenye bidii kwani mtu kuilisha familia kubwa namna hiyo si jambo nyepesi. Alikuwa mwenye wake wengi na wana wengi pia.

-Pia aliwapeleka wanawe shuleni kupata elimu, kama Ridhaa.

Uk 10. "Anakumbuka jinsi siku ya kwanza shuleni alivyotengwa na wenzake katika mchezo wao wa kuvuta

7. **MAMA RIDHAA**.

Alikuwa mzazi wake Ridhaa wa kike, na mmoja kati ya wake wa mzee Mwimo.

Ni mwenye busara. Anamfunza Ridhaa namna ya kuishi na wenzake.

Uk11,"Mama Ridhaa alisikiliza malalamishi ya mwanawe akamwambia, 'Mwanangu, ni vyema kujifunza kuishi na wenzako, bila kujali tofauti za ukoo na nasaba. Elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo wala sio fujo na chuki "

8.**SELUME**.

Alikuwa mwenye matumaini mengi, uk 31,"Selume alitueleza kuwa alikuwa amesikia fununu kuwa upo mradi wa kuwakwamua wakimbizi kutokana na hali hii. Maneno ya Selume yaliwasha mwenge wa tumaini "

**9.BILLY**

Alikuwa mlowezi.

Alibagua wengine kwa misingi ya rangi, na kuwadhalilisha wanawake wa Kiafrika, hivyo basi kutafuta mchumba huko kwao ughaibuni.

**IO.SALLY**.

Alikuwa mchumba wake Billy ambaye Billy alitaka kufunga ndoa naye.

Alikuwa mwenye majivuno na maringo, uk 80,"Kipusa akawa ameliona jumba la mpenziwe kama tundu Ia makinda, akachukua virago na kurudi kwao ughaibuni "

II.**NAOMI**.

Alikuwa mkewe Lunga.

Tabia zake zilifananishwa na za Sally aliyemwacha mumewe kwa dharau.



Uk 81,"Nimeondoka. Acha nitambae na ulimwengu, huenc nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikjtika uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao.

Kwaheri.

Naomi "

Sifa a) Ni mwenye dharau kwa familia yake, kwa jinsi anavyowaa

Cha. Tazama, Uk 81,"Nimeondoka. Acha nitambae na ulim wengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia.

Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao.

b) Ni katili.

Anaiacha familia yake na kwenda kuizuru dunia uk 84,"Alimlaani mama yake ambaye aliwatelekeza kwa ubinafsi na ukatili mkuu "

c) Mwenye majuto.

Baada ya kuwaacha wana wake, anarudi nyumbani baada ya miaka kadhaa na kukuta hali ya huko ikiwa mahame tu. Anakuta kaburi la mumewe tu, likiwa halijafyekewa kwa miaka mingi. Anaanza kazi ya kutafuta walikokwenda wana wake. Kwa bahati nzuri, mwishowe wanapatana na wana wake wakiwa bado hai. Kwa miaka mingi, anaishi kwa majuto ya kuwaacha wana wake (uk 192-193).

12. **LUNGA**.

Alikuwa mumewe Naomi.

Sifa.

a) Mwenye mapenzi kwa mkewe.

ni kwamba hili linauma na kudhalilisha zaidi kwani lunga alijisabilia kwa hali na mali kumridhia na kumpendeza mkewe "

b) Mvumilivu.

Alijikaza na kuvumilia machungu yaliyomkumba alipoachwa na mpenzi wake Naomi.

Uk 81,"lakini mkono wake ulimkataza kujidhalilisha zaidi. Alimeza funda chungu la mate na kuamua kusalimu amri ya usaliti wa Naomi "

-pia alivumilia kuwalea wanawe alioachiwa na mke wake.

Uk 81,"mwaka mmoja wa kwanza ulikuwa mgumu mno "

c) Mlezi mwema.

".Lunga ilibidi kuwa baba na mama wa watoto wake, na hilo usilione kama jambo jepesi, Hakuwaacha watoto wake kama alivyofanya mkewe Naomi.

**13. <u>UMULKHER1 (UMU)</u>**

Ni dadake Dick na Mwaliko.

Sifa.

a) Ni msomi.

Tunamwona kuwa anasomea Shule ya upili ya mtende.

Uk 82."Ninasomea Shule ya upili ya Mtende "

Uk 85,"Huenda akapata pa kuishi na hata kuyaendeleza masomo yake!"

b) Ni mwenye busara

Anapowakosa nduguzake, anawatafuta kila mahali, na hati



maye kupiga ripoti kwenye kituo cha polisi kuhusu kupotea kwa watoto wao.

c)Ni mwenye upendo.

Anawapenda ndugu zake, na hivyo, anatia bidii kuwatafuta waliko kwenda, kwa kupiga ripoti kwenye kituo cha polisi.

Uk 85,"fikra za ndugu zake zilimfanya kuzizima na hata kuishiwa na nguvu "

d) Mpenda haki.

Alijitahidi kutafuta haki yake na ndugu zake, na kuamua kuulinda utu wake kwa hali na mali uk 85,"Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu. Nitatafuta haki ilikojifi-

Cha "

e) Mwenye bidii.

Tunaona kuwa anaamka asubuhi na mapema kwenda kuitafuta haki yake.

Uk 85,"Asubuhi moja mbichi ilimpata Umu kwenye kituo cha gari moshi, akiwa amewasili kutoka mlima wa Simba, yu katikati ya mji "

f) Mpenda Dini.

Tunapata kuwa Umu aliweza kuhudhuria ibada jijini na wazazi wake kila jumapili.

Uk 85,"Kila alipokuja jijini Jumapili alikuwa akaandamana na wazazi wake kwa ubada "

g) Mwenye huruma na utu.

Anawahurumia sana vijana wa mtaani, na kutaka kuwasaidia. Anamwomba mamake pesa kidogo aweze kumsaidia



kijana mmoja. Uk 86,"Umu alitia mkono ndani ya mfuko wa dangirizi yake, akatoa shilingi mia mbili alizokuwa amedunduliza kuto-kana na mapeni

aliyokuwa akipewa na baba yake kama ma-surufu, akampa mvulana mmoja ombaomba" 14.SAUNA. Ni kijakazi aliyekuwa akiwaangalia Umu, Mwaliko na Dick uto-toni wao. Sifa a) Si mwaminifu Kijakazi huyu alitoweka na watoto, kinyume na matarajio ya kuwaangalia wana hao. Uk 84,".ilibainika kuwa wanuna wake walikuwa wametekwa nyara na Sauna" b) Katili Anawapeleka watoto aliowateka nyara kwa bibi mmoja ambaye aliwatumia binadamu kama malighafi" 15.HAZINA. Huyu alikuwa kijana wa mtaani aliyekuwa akiombaomba mapeni huko barabarani, na alisaidiwa na Umu kwa pesa alizozitumia kununulia mkate. Sifa a) Mwenye heshima. Anamshukuru sana Umu baada ya kumpa pesa za kununua mkate. Uk 86,"Poa sana sistee, we ni mnoma. Siku moja nitakuhelp 113

b) Ni msomi.

Alienda shuleni na kupata elimu.

Uk 88,"Nilipelekwa shuleni nikasoma, nina elimu japo akali. Amesomea upishi na huduma za hotelini katika chuo.

c) Mwenye upendourafiki wa dhati.

Anamwita Umu anapomwona, kwa kukumbuka wema aliomtendea wakati mmoja. Hazina alimpeleka Umu kwenye hoteli na kumpa chakula mpaka akashiba. Aliahidi pia kumsaidia

Umu, na akampeleka kwao nyumbani.

Uk 89,"Hazina alimwahidi Umu kuwa atamsaidia. Alimpeleka moja kwa moja hdi kwenye makao yao, akamjulisha kwa mama aliyesimamia makao hayo"

**16.JULIDA**.

Ni mama aliyesimamia makao yaliyokuwa ya wana wa mitaani.

Sifa.

a) Mwenye utu na upendo-Anamkaribisha kwa upendo

Umu, na kumpa tumaini.

Uk 89,"Julida alimgusa Umulkheri begani na kumwambia, 'usijali mwanangu. Hapa patakuwa penu kwa muda"

b) Mwenye huruma.

Kwa kumgusa Umu begani, anaonyesha kuwa anamhurumia mwana huyu kwa yaliyomfika.

114

**17. KAIRU**

Sifa a)Ni mvumilivu.

Kulingana na jinsi anavyomwambia Umu, inaonekana kuwa yeye ameyapitia magumu, na kuyavumilia.

hujapitia tuliyo yapitia. Tulitendwa ya kutendwa "

b) Ni msomi.

Ingawa anajipata katika hali ya ufukara uliozidi, mamake anajaribu kuzungumza na mwalimu mkuu baada yake kufukuzwa shuleni kwa ajili ya kukosa karo. Jambo hili linamsaidia kuendeleza masomo yake shuleni kama wanafunzi wengine.

Uk 93."Hata karo yangu imebidi amlilie mwalimu mkuu amruhusu alipe kidogo kidogo hadi mwisho wa mwaka "

Pia tunapata kuwa walipofika huku, Kairu alikuwa katika darasa la sita, na kwa sasa, ako katika kidato cha pili. Hii ina maana kuwa amekuwa akiendeleza masomo yake kwa ufasaha.

Uk 92,"nilikwenda hapo nikiwa katika darasa la sita, sasa ni katika kidato cha pili "

18. **MZEE KAIZARI**.

Alikuwa babake Mwanaheri, na Lime.

115

Sifa.

a) Mwenye Busara.

Aliyajenga maisha ya familia yake upya baada ya kutoka msituni na kurudi nyumbani.

Uk 93,"baada ya kurudishwa nyumbani kutoka msitu wa mamba, baba yangu mzee Kaizari aliweza kuyajenga maisha yetu upya "

b) Mwenye mapenzi kwa familia yake.

Aliweza kuijengea familia yake nyumba pale ambapo waliishi zamani. Baada ya mkewe kutoweka, tunamwona Mzee Kaizari akitia bidii sana katika kumtafuta kwao na pia mjini.

Uk 96,"Baba alikwenda kumtafuta mama kwao asimpate baba alifululiza mjini kumtafuta mama, majuto yamemjaa kifua"

c) Mvumilivu.

Anapompata mkewe akiwa ameaga dunia, alivumilia uchungu wa kumpoteza ampendaye, na akamzoazoa na kumzika pamoja na wanawe.

Uk 96,"Baba alizoazoa kilichobakizwa na uozo, tukakizika "

**19.MWANAHER1**

Huyu ni mwanawe mzee Kaizari.

Sifa.

a) Ni mpenda mashairi.

Anawaelezea wenzake kuwa alijaribu kupalilia kipawa chake cha kughani mashairi mepesi uk 93.

116

b) Ni msomi.

Anaendeleza masomo yake pamoja na wenzake, akina Kairu.

c) Ni mvumilivu.

Anayapitia mambo machungu tangu kuachwa na mamake, mpaka wakati walipomzika katika kaburi la sahau.

Barua aliyoiandika mama kabla ya kutoweka ilimtonesha kidonda rohoni mwake.

20.**LIME**.

Ni ndugu yake Mwanaheri, na wote wawili ni wana wake Mzee

Kaizari.

Sifa.

a) Ni msomi.

Walisoma pamoja na dada yake huko kijijini.

Uk 93."mimi na ndugu tulirudi shuleni mle mle kijijini mwetu tu "

b) Ni hodari katika michezo ya kuigiza.

Uk 93,"Lime alikuwa hodari katika michezo ya kuigiza -ile ya kitoto "

c)Mcheshi.

Alipendwa sana shuleni kwa ucheshi wake.

Uk 93,"Alikuwa mcheshi sana, kwa hivyo kutokuwepo kwake shuleni kuliwafanya watoto kumpeza "

117

**1. KANGARA**.

ifa.

a) Mkiukaji haki za watoto.

Bii kangara anakiuka haki za watoto kwa kuwashika na kuwauza katika madanguro, na kwa matajiri, ili wawe watumishi, na kutumika kama ala biashara haramu.

Uk 157,"Bi. Kangara alifanikiwa kupata wasichana wa kuuza katika madanguro, wavulana wa kuwapelekea matajiri ambao walishiriki katika ulaguzi wa dawa za kulevya, na wafanya kazi katika makasri ya matajiri, na katika mashamba ya mikahawa na michai "

Uk 158,"mabibi hawa walifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la ukiukaji wa haki za watoto "

b) Mwanabiashara haramu.

Anafanya biashara haramu ya kuwauza watoto, na baadaye, anakamatwa na kufungwa gerezani miaka saba ".wakarambishwa miaka saba gerezani na kazi ngumu "

**22. SAUNA**.

Wanafanya kazi pamoja na Bi. Kangara.

Sifa.

a) Mlaguzi wa binadamu.

Wanafanya kazi ya kuwauza watoto pamoja na Bi. Kangara

Uk 157,"Hatimaye ulaguzi wa binadamu uligeuka ukawa ngozi yake"



b) Mwenye bidii. Alifanya kazi yake kwa bidii, Uk 157, "Sauna aliianza kazi yake. Ni kazi iliyompa pa to kubwa sana, hata akataka kusahau yaliyopita na kuwasamehe walezi wake.

c) Mtumwa.

Alifanya kazi chini ya masharti yake Bi. Kangara.

Uk 157."Hatimaye, ulanguzi wa binadamu uligeuka kuwa ngozi yake. Na sasa yu tayari kushika tariki kutekeleza utumwa mwingine wa Bi. Kangara "

***MASWALITARAJIWA KUHUSU WAHUSIKA***.

*1. Mzee Kaizari ni mhusika mwenye manufaa mengi katika jamii. Tetea kauli hii kwa kutolea umuhimu wake kama unavyojitokeza kwenye riwaya hii (alama 20).*

*2. Taja sifa kumi za mhusika Ridhaa kama zinavyojitokeza kwenye riwaya hii (alama 20).*

*3. Taja umuhimu wa wahusika wafuatao katika kuwasilisha maudhi (alama 20).*

*a) Sauna.*

*b) Bi. Kangara.*

*c) Lime d) Umulkheri.*

*4. Mhusika Hazina ametumika kudhihirisha maisha ya vijana yalivyo huko mitaani. Kulingana na matukio yanayomkumba mhusika huyu, tolea mapendekezo ambayo yangeweza kufuatwa Hi kuwasaidia vijana wengine kama hawa (alama 20)*

*5. Taja sifa zake Umulkheri kama zinvyojitokeza katika riwaya hii (alama 7).*

*6. Taja sifa zake Lunga na umuhimu wake katika kupitisha maudhui ya riwaya hii (alama 20).*

*7. Mwandishi wa riwaya hutumia wahusika kama vyombo vya kuwasilisha maudhui yake kwa msomaji. Kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri, eleza maudhui yanayopitishwa kupitia kwa mhusika Ridhaa (alama 20).*

*8. a) Ni nini tofauti kati ya mhusika mkuu na mhusika mwingine asiye mkuu (alama 2)*

*b) Kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri, taja wahusika watano wakuu, na watano wasio wakuu (alama 5)*

*c) Taja sifa tano za mhusika mkuu yeyote (alama 5)*

*9 a)Eleza sifa tcno za mhusika Kairu katika riwaya hii (alama b) Kairu ametumika na mwandishi kupitisha maudhui yepi?*

*Eleza (alama 10).*

*10. a) Mhusika Naomi ametumika na mwandishi katika kuwasilishha maudhui kadhaa kwa msomaji. Kwa kutolea mifano, thibitisha haya (alama 10)*

*b) Taja sifa tatu za mhusika Billy (alama 3).*

*c) Eleza umuhimu wa mhusika Billy katika kuwasilisha maudhui kwa msomaji (alama 2).*



9. **FANI- MBINU ZA LUGHA NA MBINU ZA/ TAMATHALI MBINU ZA UANDISHI**...

Tamathali za uandishi ni matumizi ya kwa narrina fulani ili kuifanya lugha iwe ya kuvutia na kuifanya kazi ya Sanaa iwe ya kupendeza. Mbinu hizi za uandishi zimegawika katika makundi mawili makuu: MbinuFani za lugha. Mbinu za Sanaa a)Mbinu za lugha Huu ni uteuzi wa maneno iii kuifanya lugha iwe ya kupendeza na kuvutia. Pia hujulikana kama mapambo ya lugha b)Mbinu za Sanaa Huu ni ubunifu wa kisanaa unaojitokeza baada ya kusoma kazi ya fasihi au kusikiliza masimulizi. Mifano ya mbinu za lugha katika riwaya hii 1.3

**JAZANDA**.

Hii ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja bila kutumia viunganishi. Katika ukurasa wa 4 tunasoma; "Mwangekaalisema Ridhaa kupitia kwa sauti ya mawazoni mwake, kumbe wewe ni sawa na yule Mwangeka wa kihistoria ambaye kivuli chake kikitem-bea siku zote mbele yake, ambaye mwili wake ulikuwa kaka tu, roho yenyewe iliishi nje ya kaka hill kwa kutotaka kudhibi-tiwa?Umewezaje kunusurika? Kumbe wadhifa waliokupa wa 

kwenda u umisha Amani katika mashirika ya kati umetokea kuwa wongovu wako?"

Hapa, Ridhaa anamlinganisha Mwangeka wa kisasa na yule

Mwangeka wa kihistoria.

*Katika ukurasa wa 6 tunasoma; "Basi niambie, baba, unatumia mantiki gani kusema kuwa Sisi si watoto wa miaka hamsini? Je, miaka hamsini ya uhuru imetukuza kiuchumi au tumebaki kuwa wategemezi wa hao hao ambao walitupa uhuru?"

Hapa kuna ulinganishi kati ya miaka hamsini ya uhuru wa taifa, na miaka hamsini ya kuzaliwa kwa hawa watu ambao bado hawajajikomboa kutokana na ule ukolonio mambo leo.

Katika ukurasa wa 8 tunasoma; "Ardhi ya mzee Mwimo

Msumbili ikawa haitoshi kuyalea madume yake ishirini "

Vijana wake Mzee Mwimo wanalinganishwa na madume ishirini.

Katika ukurasa wa 29 tunasoma; "Nilihisi kwamba ingekuwa bora kama tungefia katika mazingira tuliyoyazoea; huenda hata tungepata wa kutuomboleza, kuliko kufia ugenini "Sasa umeanza kufikiria kama wafuasi wa nabii Musa ambao baada ya kukosa chakula huko jangwani, walimshutumu kwa kuwatoa kule Misri. Walidai kuwa huko Misri wangekula matikitimaji yao pamoja na kuwa watumwa!"

Hapa, msemewa anafananishwa na wale wana wa Israeli waliOtamani kuwa ni heri wangekufia huko misri badala ya kupelekwa jangwani na Musa kufia huko.

2. **TASHIHISI/UHUISHAJI**.

Hii ni mbinu ya kupatia kitu kisicho uhai sifa za kiumbe mwenye uhai, au sifa za kibinadamu. Katika ukurasa wa 3 tunasoma; "Alijiona akiamka asubuhi ambayo ilizaa usiku wa jana, usiku ambao ulitandaza kiza katika maisha yake "

Usiku unapewa sifa za kuwa na uhai na kupewa uwezo wa kuzaa asubuhi kama mwana.

4 tunasoma; "Familia yangu na mali yote hii kuteketea siku moja?Bila shaka hili ni zao lingine la husuda "

Husuda inapewa sifa ya kibinadamu na kuwa na uwezo wa kuzaa maovu aliyotendeka. Katika ukurasa wa 7 tunasoma; "...mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri"

Tunapata kuwa hapa, mashamba yanapewa sifa ya kuwa na uhai, kwani kuna sehemu zilizozaa mazao mengi.

pia ardhi inaonekana ikiwa katika hali ya ukengeushi; hivyo kupewa sifa ya kuwa na uhai. Katika ukurasa wa 8 tunasoma; "Ardhi ya Mzee Mwimo

Msumbili ikawa haitoshi kuyalelea madume yake ishirini ifiga-*

wanywa hadi ikawa vikata, ikalimwa na kupaliliwa mpaka ikachoka "



shamba hili linapewa sifa kuwa na uhai, kwani linachoka baada ya kufanyiwa kazi nyingi.

Katika ukurasa wa 12 tunasoma; "Ridhaa hakujua alikuwa amesimama pale kwa muda gani. Miguu yake sasa ilianza kulalamika "

Tunapata kufahamu kuwa miguu ya Ridhaa inalalamika.

Hapa miguu imepewa sifa ya kuwa uhai na kuwa na uwezo wa kulalamika kama binadamu.

Tunasoma pia; "Baada ya muda wa mvutano wa hisia na mawazo, usingizi ulimwiba "

Usingizi umepewa sifa ya kibinadamu na kuwa na uwezo wa kuiba.

Katika ukurasa wa 14 tunapata haya; "Tumo katika kambi fulani-la, si kambi, mabanda hasa yaliyosongamana na kutazamana kwa jitimai na dhiki, vibanda vya mtomeo hasa "

Vibanda hivi vinapewa sifa ya kibinadamu, kwa vinaweza kusongamana na pia kutazamana kwa jitimai na dhiki, kana kwamba vina macho na hisia.

Katika ukurasa wa 15; "Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kasha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; "

Mawingu yanapewa sifa za kuwa na uhai kama binadamu, yanatembea kwqa kedi na nadaha. Pia mawingu haya yanashiba na kuataka kutapika. Pia yanagooka, yanakaribiana na pia



Rupigana busu; hizi zote zikiwa ni sifa za kibinadamu.

Katika ukurasa wa19; "Tunahitaji kumpa nafasi Mwekevu. Hu_

enda hata hatukwamulia uchumi ambao unachechemea "

Uchumi unapewa sifa ya kibinadamu ya, na uwezo wa kuchechemea.

Katika ukurasa wa 35; "Undugu na utangamano wa wakimbizi wenzake uliyahuisha maisha yake, ukayajenga upya, ukamfunza Zaidi kuhusu maisha yake, ukayajenga upya, ukamfunza

Zaidi kuhusu thamani ya binadamu "

Ridhaa anakumbuka jinsi maisha yake yalivyokuwa yamekosa maana lakini baadae yakahuishwa na wakimbizi wenzake, yakajengeka upya na akaelewa Zaidi kuhusu dhamani ya binadamu.

Katika ukurasa wa 76; "Walipokuja hapa, ardhi hiyo haikuwa bikira, wakatifua udongo wakailima?"

Ardhi inapewa sifa kama za binadamu za kuwa bikira, hivyo basi, mbinu ya uhuishaji kujitokeza.

Katika ukurasa wa 143; "Kipanga sasa ameanza kuuhuisha utu wake"

Mbeleni maisha yake hayakuwa na maana lakini kwa sag anayapa uhai, na hivyo yanapata maana, na utu wake unawwa kamili.

Katika ukurasa wa 156; "Asubuhi moja mbichi ilinipay kwenye baraste kuu; nimmeamua kutamba na ulimwengU



Asubuhi inapewa sifa za kuwa na uhai na kuwa mbichi au changa. Pia asubuhi hii inampata kwenye baraste kana kwamba inatembea.

3.**SEM1**.

semi ni fungu la maneno linalotumika kutoa maana tofauti na ile ya maneno yaliyotumika. Semi hutumika kuficha ukali wa maneno au kupamba lugha.

Kwa jumla, kuna aina mbili za semi.

a)Nahau.

b)Misemo.

Nahau.

Ni fungu la maneno lenye maana fiche, isiyotokana na maana ya maneno halisi yaliyotuimika katika uandishi.

Katika ukurasa wa 2; "Wewe endelea kupiga hulu tu, lakini utakuja kuniambia"

Katika ukurasa wa 3; "Angesema bibi huyu amebugia chumvi ya maisha ikamrishai "Alijihisi kama mpigana masumbwi aliyebwagwa na kufululizwa makonde bila mwombbezi "

Katika ukurasa wa 6; "Na kazi zenyewe si kazi, ni vibarua vya kijungujiko tu '

Katika ukurasa wa 7; "Mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi "



**MISEMO**.

Haya ni mafungu ya maneno yenye maana maalum ambayo hutoa mafundisho kwa jamii.

Katika ukurasa wa 4;"Alikuwa amesafiri kwa shughuli za ujenzi wa taifa kama alivyoziita safari zake za kikazi. Uchungu wa mwanagenzi ukawa haujui simile, ukabisha hodi, naye mwangeka akazaliwa "

Katika ukurasa wa 6; "Imekuwa tunaubadili ule msemo wa mtegemea nundu haachi kunona "

Katika ukurasa wa 7; "Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa mhuri, umilikaji wa ardhi na waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku"

Katika ukurasa wa 9; "Mzee mwimo akaona ku moto, akaamua kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa

Heri, ama Ughaishu kama walivyouita watu wa huko "

Katika ukurasa wa 10; "wewe ni mfuata mvua. Hatutaki kucheza nawe"

Katika ukurasa wa 11; "Baadaye aliamua kuuasi ukapera, akapata mke; Terry "

Katika ukurasa wa 16; "Wamesema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi "

Katika ukurasa wa 25; "Wakati tukitazama ubahaimu huu wa



Firauni, hatukujua kuwa tulikuwa kuni kwenye uchaga, chuma chetu kilikuwa motoni "

Katika ukurasa wa 71; "Rai ya wakubwa hata hivyo haikuwanyamazisha Lunga. Aliendelea kulipinga tendo hili kwa jino na ukucha "

Katika ukurasa wa 92; "Lakini, lo!wanasema wajuao kuwa msitu ni mpya, ila nyani ni wale wale "

Katika ukurasa wa 148; "Akiisha kutimiza maazimio yake, atajichagulia kijana mwenzake wafunge akida "

Katika ukurasa wa 150; "Hata hivyo, fahamu kuwa mara zote binadamu huhitajika kujikuna ajipatapo; "

Katika ukurasa wa 183; "Ule msemo maarufu wa baba yangu, usiisifu njaa ya mbwa kabla usiku haujaingia ukahakikisha kuwa mbwa amelala njaa, ukatimia "



4. **METHAL1**.

Hii ni misemo ya hekima yenye maana iliyofumbwa. Mwandi.

shi hutumia methali kupitisha ujumbe fulani.

Katika ukurasa wa 12; "Kweli jaza ya hisani ni madhila?"

Katika ukurasa wa 36; "Hata Ridhaa anapomfikiria Kaizari anajiambia, 'Heri nusu shari kuliko shari kamili '

Katika ukurasa wa 50; "Moyoni alijua kuwa bado palikuwa na kazi ngumu ya kujenga upya ukuta ambao ufa wake ulikuwa umepuuzwa " Methali inayorejelea ni 'usipoziba ufa utajenga ukuta'

Katika ukurasa wa 51; "Alimtazama baba yake kana kwamba anataka kuhakikishiwa jambo, naye Ridhaa akamjibu kwa mtazamo uliojaa Imani, "Mwenye macho haambiwi tazama"

Katika ukurasa wa 53; "Akili yake ilimkumbusha methali aliyozoea kumtolea mpinzani wake darasani kila mara Mwangeka alipomshinda kuwa, 'Wino wa mungu haufutiki '"

Katika ukurasa wa 55; "kumbe amekwenda kuingia kwenye mtego wa panya unaowanasa waliomo na wasiokuwemo!"

Katika ukurasa wa 75; Kulikuwa pia na maskini ambao kupata kwao ahueni kulitegemea utashi wa matajari. Dau la mnyonge tangu lini likaenda joshi?"

Katika ukurasa wa 113; "Kumbukeni methali isemayo, uling0

wa kwae haulindi manda "



Katika ukurasa wa 183; "Msemo huu ni sawa na methali ya

Kiswahili isemayo, Mungu hamsahau mja wake; au hata bora zaidi, kuregarega sio kufa, kufa ni kuoza tumbo "

5. **LAKABU**.

ni mbinu ya mhusika kupewa ama kubandikwa jina na wahusika wengine ama yeye mwenyewe kujibandika jina linalooana na tabia au sifa zake.

Katika ukurasa wa 94, "Haikuwa ibra kumsikia nyanya akimrejelea mama kama Muki, yaani, huyo wa kuja, na kusema kwamba msichana wa bamwezi, hata akiwa na umri wa miaka tisini, ni msichana wa Bamwezi tu.

Katika ukurasa wa 178; "Pongezi engineer Vuuk. Naona hili litatusaidia kumhepa Kumuku mwenye kuchungulia kutoka dirisha ndogo la kibanda chake. Kumuku ilikuwa lakabu ambayo vijana hawa walikuwa wamembandika babu yao; lakabu ambayo ilikuwa msiba wa kujitakia "

Katika ukurasa wa 182; "Jumamosi hii kinyang'anyiro kiliku-

Wa katia ya majimbi wawili-wa Mwangeka akiitwa Kyenza kabisa)na wa Mwangemi akiitwa

Mumina (kamaliza)."

## 6. **RITIFAA**.

Hii ni mbinu ya kuzungumza na mtu aliyekufa au asiyekuwe-

Po kana kwambo yupo pamoja nawe.



Katika ukurasa wa 6; "Ni kweli binti yangu, kwa kutumia fals fa hii, una haki ya kusema Sisi tu watoto wa miaka hart sini; Ridhaa sasa analiambia lima la jivu ambalo anaarnil ndilo mabaki ya mwili wa bintiye 'ffunapata kuwa Ridha anazungumza na nafsi ya bintiye aliyeiaga dunia kutokana n kuteketezwa moto.

Katika ukurasa wa 12; "Ridhaa hakujua majibu ya maswal haya. Alilojua ni kwamba haya siyo aliyotumaini baada miongo mitano ya maisha katika maskani haya. Alitamani kupiga ukemi kumwamsha mkewe lakini akili ilimkumbusha kuwa huyo hayupo tena katika ulimwengu huu "Ridhaa anatamani kumwamsha mkewe ambaye kwa sasa ni majivu tu, hayupo tena kwa hali halisia, bali yupo katika nafsi yake Ridhaa.

## 7. **UTOHOZ1**.

Hii ni mbinu ya kuswahilisha maneno ya lugha nyingine, yatumike kama ya Kiswahili.

Katika ukurasa wa 6; "Si yule myunani ambaye amewageuza wenyeji kuwa maskwota katika vitovu vya usuli wao?" Maskwota kutoka 'squatter'.

Katika ukurasa wa 13,".kupitia kwa halmashauri ya kitaifa ya barabara, ilikuwa imewapa notisi mabwanyenye wanaoyamiliki majumba haya " Neno notisi kutoka 'notice'.

Katika ukurasa wa 34; "Opresheni rudi kanani " opresheni



kutokana na 'operation'.

Katika ukurasa wa 70; "Mkulima namba wani " Namba wani kutokana na 'Number one'.

Katika ukurasa wa 189; "Najihisi kama Kurwa katika novela ya Kurwa na Doto novela kutokana na 'novel'.

## **8.WCHANGANYA NDIMI.**

Hii ni mbinu ya kuweka maneno yasiyo ya Kiswahili katika sentensi ya Kiswahili.

Katika ukurasa wa 2; "na hata kukawa na jambo, what can

Katika ukurasa wa 6; "Mara ngapi umesimama kwenye shopping mall yake ukiwa safarini

Katika ukurasa wa 7; "Ama hii ndiyo ile wanayoiita historical injustice?"

Katika ukurasa wa 17; "...hawa watu wamekuwa wakitusumbua na Affirmative Action, na A third should be women"

Katika ukurasa wa 23; "Wewe tutakuteuwa kama Education

Attache huko Uingereza "

Katika ukurasa wa 86; "Alipoinua macho yake alikiona kibao kilichoandikwa church road, na mara anakumbuka ilikoelekea ile barabara "

133

Katika ukurasa wa 86; "Poa sana sistee, we ni mnoma siku moja nitakuhelp hata mimi "

"Eazie, nenda ukanunue loaf. Na promise hutanunua glue pliz pliz bratha, "

Katika ukurasa wa 113; "Katika kozi zenu mmefunzwa Effective Communication and Conflict Resolution, "Vilio vya raja kuhusu kile wanachokiita extra judicial killings vimehanikiza kote "

Katika ukurasa wa 114; "Watetezi wa haki wanalilia kile wanachokiita untimely deaths of innocent people, many of whom are youth "

Katika ukurasa wa 159;"haikuwa Baraka yetu, mwanetu

Bahati was a sickle-cell case "

**9.KUHAMISHA NDIMI**.

Ni mbinu ya kuingiza hii sentensi ya lugha nyingine katika kifungu cha lugha ya Kiswahili. Kinyume na kuchanganya ndimi, (ambapo mwandishi huchanganya maneno katika tensi moja),katika kuhamisha ndimi, sentensi kamilifu lugha nyingine hutumika miongoni mwa sentensi za Kiswahili sanifu.

Katika ukurasa wa 2; "Since when has man ever changed destiny?"

134

Katika ukurasa wa 25; "As for me and my family, we will support our mother "

Katika ukurasa wa 31;"Peace be with you "

Katika ukurasa wa 43; "If there is no bread, let them eat cake "

Katika ukurasa wa 80; "Darling, this will be your home soon after our honeymoon "

Katika ukurasa wa 86;"Mum pliz, just a red!These guys are needy!"These are pretenders. They have been sent by their stinking rich relatives I cant give them even a penny "

Katika ukurasa wa 159;"She did not survive her first week "

Katika ukurasa wa 171; "Thankyou Mummy, for reminding

Daddy that there is another engineer in the family "

Katika ukurasa wa 182; "Come on, Kyenza Kinyenyo, give him another one, just like the other one!"

**10.1STIARA**.

Hii ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kutumia kiungo 'ni' au 'kuwa'. Mbinu hii pia hujulikana kama sitiari au istiari.

Katika ukurasa wa 1; Kunguru wanalinganishwa na jeshi.

135

"Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba yake ya nyumbani adhuhuri ya juzi ile "

Katika ukurasa wa 5;"Umekuwa kama jani linalopukutika msimu wa machipuko!Umetoweka katika ulimwengu huu ukiwa teketeke, hata ubwabwa wa Shingo haujakutoka "

Katika kurasa za 8-9; Maisha ya familia ya Mzee Mwimo yanalinganishwa na ndege kwenye kiota. Anasema kuwa hata kipunga akiona kuwa wana wake wamekuwa wakubwa na bado hawataki kutoka kiotani, yeye hukifanya kiota chenyewe kukosa raha kwa kukiweka miiba. Hapo ndipo hawa vifaranga huona kuwa wakati wao wa kuondoka ushatimia.

Anasema kuwa hao vifaranga hawaambiwi na mtu kuwa wakati wao wa kupambana na dunia umefika, na hivyo basi, wao hujiondokea bila kuambiwa. Vivyo hivyo, ndivyo kuko katika hii familia ya Mzee Mwimo Msumbili.

Tunaambiwa kuwa kwa kuwa na wana wengi, wanao hitaji chakula kila siku, huko nyumbani kwake mzee kukatokea uhasama, na pia migogoro. Kutokana na hayo, mzee Mwimo akaamua kuwahamisha wanawake wake wawili wa mwisho. Wao walipelekwa katika msitu wa Heri kama ulivyojulikana.

Katika kurasa za 14-15;Anasema kuwa ugeni uliopo ni ule wa hali, mazoea na silika. Anasema pia kuwa walipo hapo wak0

pamoja na matajiri na pia walio masikini. Anasema kuwa unaweza dhani kuwa kuna kiasi cha usawa, lakini binadamU husema kuwa hakuna usawa kati ya binadamu ila tu katika



kifo. Anasema kuwa kile ambacho hawajui ni kuwa hata katika kifo, binadamu hawawi sawa hata kidogo. Kunao wanaoaga dunia huku wakiwa wamefishwa ganzi, kiasi cha kuwa hawatausikia uchungu wa kifo. Kuna tofauti pia kati ya mandhari wanamofia hawa binadamu. Kunao wanaokufia katika zananati huku daktari akijaribu kuwaokoa. Wengine wanakufia katika hospitali za kifahari, huku wakiliwazwa na mashine, -

na kila mtu anashughulika na kuushikilia uhai wa huyu mheshimiwa. Anasema kuwa wanapokufa hawa, nyuso zao huwa huwa zimetulia, na pia wanaziachilia roho zao kwa faraja. Tunaambiwa kuwa hatuwezi kulinganisha nyuso za hawa na wale wanaofia kwenye hamaniko wakizingirwa na jamaa ambao hawana hata hela za kununulia sindano angalau ya kuwaingiza dawa mwilini. Pia kuna wale wanaokufia vitongojini, kwenye vitanda vya mwakisu baada ya kunywa pombe haramu. Hawa nao wanalinganishwa na nzi amabao hufia dondani na

hiyo isiwe ni hasara. Wanalaumiwa kwa kujiingiza katika msiba wa kujitakia. Pia kuna tofauti katika mitindo ya mazishi, viviga vinavyohusishwa na sherehe za mazishi na hata mavazi ya "mwenda zake". Pia jeneza analozikwa nalo pia lina tofauti, kwani tajiri atazikwa kwa jeneza la dhamani kubwa kulinganisha na huyu masikini.

Maelezo haya yote yanaleta tofauti kati ya matabaka mawili. Tunalinganisha matabalka haya mawili na kuona tofauti iliyokuwepo katika hali zote.

Katika ukurasa wa 18; Tunaambiwa kuwa mwamu wake

Ridhaa, kabla tu ya kusikia mlio wa bunduki, mitutu yake iliku



wa ishatema risasi kama bafe atemavyo mate. Utemaji wa risasi unalinganishwa na utemaji wa mate kwa bafe.

Katika ukurasa wa 50; Anasema kuwa elimu yoyote bila kielelezo chema kutoka kwa wanaoitoa elimu yenyewe ni sawa tu na juhudi zile za mfa maji.

Katika ukurasa wa 149; Maisha yake na Fungo yalibadilika na kuwa kama yale ya ng' ombe aliyetiwa shemere na Maisha yangu kufungwa nira pamoja na puna ambaye anakataa kusonga mbele. Maisha ya hawa wahusika wawili yanalinganishwa na huyu ng' ombe aliyefungwa pamoja na punda.

## II. TAASHIRA.

Haya ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani. Jina au kitu fulani kinatumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa.

Katika ukurasa wa 3; "Katikati ya mito hii ya machozi, Ridhaa aliileta picha ya maisha yake mbele ya kipaji chake "

Katika ukurasa wa 5; "Lakini baba, wewe siwe uliyeniambia kuwa mashamba ya theluji nyeusi yalikuwa milki ya wakolo-

Katika ukurasa wa 12; "Ridhaa hakujua alikuwa amesimama pale kwa muda gani. Miguu yake sasa ilianza kulalamika. P01e pole parafujo za mwili wake zililegea, akaketi juu ya majivu-la juu ya miili ya wapenzi wake "

138

Katika ukurasa wa 46; "Alikuwa ameumwa na nyoka, bafe hasa, na billa shaka mwenye kuumwa na nyoka akiona ung' ongo hushtuka " Matukio yaliyokuwa yamemkumba

Ridhaa yanafananishwa na nyoka ambaye alimuuma, na hivyo, hawezi kuyasahau.

Katika ukurasa wa 59; "Alikuwa ametoka shuleni, siku hizo walimu walikuwa wameng' angl ania kuwafunza Jumamosi, wanafunzi waliokaribia "ICU" kama walivyoliita darasa

Ia nane " Darasa la nane linalinganishwa na "ICU".

**12.TAKRIR1**.

Hii ni mbinu ya kurudia rudia neon moja au fungu la maneno ili kusisitiza ujumbe Fulani.

Katika ukurasa wa 4; "Ridhaa alirudi nyumbani na kusimama katikati mwa chumba ambacho yeye na aila yake walikuwa wamekitumia kama sebule kwa miaka na mikaka "

Katika ukurasa wa 14; "Na usidhani ni mazingira mageni, kweli si mageni, si mageni kwani tu mumu humu mwetu, hatumo ughaibuni wala nchi jirani. Tu katika jimbo lile lile tulilozoea, kilichobadilika ni kijiji tu, ni kama kutoka chumba cha malazi, kwenda sebuleni!"

Katika ukurasa wa 16; "Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye subira wangu wa zamani. Siye, siye, siyeee. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi "

139

Katika ukurasa wa 48; "Siye!siye hata kidogo!kilichobaK lite tabasamu lake la daima, lililozoea kumhakikishia usalama siku zote, tabasamu ambalo lilidhihirisha meno meupe pepepe yenye mwanya mkubwa wa kuvutia, mwanya ambao Ridhaa alikuwa amezoea kumwambia Mwangeka kuwa mwanya huo ndio ndoana ambayo aliitumia kumvulia mama yake!"

Katika ukurasa wa 138;

"La!la!la mwanangu!Hayo unayoyawazia siyo, ila naona ni muhimu nihamie ile nyumba yangu ya afueni "

Katika ukurasa wa 154;"Mlaani shetani' Sauna aliuambia moyo wake, 'unajua kuwa mimi sikuumbiwa ujalaana, walimwengu ndio walinifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari. Fikiria u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kasha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna hata uso wa kumtazamia yeyote.

**13.UZUNGUMZ1 NAFSIA**.

Hii ni mbinu inayomhusu mhusika, anapojizungumzia, ama kwa kuongea au kuwaza, bila kukusudia kusikika na yeyote.

Katika ukurasa wa 4; Ridhaa kupitia kwa sauti yake ya moyoni anamwita Mwangeka, na kumwambia kuwa yeye alikuwa tu kama yule Mwangeka wa kihistoria ambaye kivuli chake kilitembea siku zote mbele yake. Mwangeka huyu pia mwili wake ulikuwa kaka tu, roho yenyewe iliishi nje ya kaka hili kwa kutotaka kudhibitiwa. Ridhaa anajiuliza ni aje mwana

we Mwangeka angeweza kunusurika tu. Anajiambia kuwa wadhifa ambao Mwangeka alipewa wa kwenda kudumisha

Amani katika mashirika ya kati ulitokea kuwa ndilo jambo la kumuokoa yeye.

Pia anajizungumzia kwenye mawazo yake na kujiambia kuhusu mkaza mwananwe, masikini Lily. Anajiambia kuwa amekuwa kama jani linalopukutika wakati msimu wa machipuko! Anasema kuwa Lily ametoweka katika dunia hii hata kabla ya ubwabwa wa Shingo kumtoka.

Katika ukurasa wa 5; Mawazoni mwake Ridhaa anaskia sauti yake Becky ambaye alikuwa mjukuu wake ikimwita. Ridhaa anaskia sauti za mjukuu wake zikimwita akilini mwake, ilhali katika hali halisi hayupo, Katika ukurasa wa 47;Ridhaa anasema kuwa anamsikitia mwanawe kwa kuwa hakuwa na familia ya kuendea. Anajisemea kuwa wanuna wake Mwangeka waliangamia wote. Anasema kuwa mkazamwanawe na wanao aliangamizwa na moto, hivi kwamba hata mafuvu ya kuzika hayakubakia. Anaendelea kusema kuwa hata makaburi ya kuwekea makoja ya maua ambayo Mwangeka alikuwa akiyatunga akilini mwake hamna.

Ridhaa anajipata katika hali hii ya kuzungumza na nafsi yake, kuhusu hisia na fikra za mwanawe kuhusiana na suala la kuangamia kwa familia yao. Mazungumzo haya yote yanajikita katika nafsi yake Ridhaa.



Katika ukurasa wa 48; Mwangeka aliinua kipaji chake, akata zamana na baba yake. Aliona kuwa babake alikuwa amekon.

ga Zaidi. Uso wake umeshamiri weusi na unyonge. Aliendelea kujisemea akilini mwake kuwa sasa babake alimshabihi babu

Mwimo Zaidi, hasa kule kupwaya kwa ngozi yake.

Katika ukurasa wa 78; Umulkheri aliyaambia macho yake, ya_

toke huko mbali yalikokuwa yametanga, akayarudisha darasani, yakatazamana na mwalimu Dhahabu bila yeye

Umulkheri kumwona mwalimu mwenyewe.

Katika ukurasa wa 152; "Usinitazame kana kwamba unataka nikwambie yaliyotokea baadae, 'nilijisemea kana kwamba ninajibu mtazamo wa Selume, 'nyinyi ndio wa kuniambia kwani nilijipata hapa penu, "Pete aliongeza na kukatisha ghafala usimulizi uliokuwa mawazoni mwake 'NMawio ya leo yanaelekea kuwa na kiza kisicho cha kawaida, "alijisemea kijakazi Sauna huku akijipindua kuusikiliza mlio wa king'ora unaosikika kwa mbali"

Katika ukurasa wa 153; "Kwa mbali, anasikia mbisho hafifu langoni mwa jumba hili. Anatoka nje kwenda kuitika mbisho huu. Ghafla, uso wake unakumbana ana kwa ana na polisi! Mara anasikia moyo wake ukimwambia, "Yako ya arubaini imefika, "huku akijaribu kuvaa tabasamu na kuwakaribisha maafisa hawa nyumbani"

Sauna ameisha kupata ujira wake kwa kazi hii pia, naye u tayari kuondoka asubuhi ya kuamkia krismasi. Hata sauna

anapowazia matendo yake, hasa ya hivi maajuzi, anatamani kujisuta. Anahisi kwamba hafurahii kazi hii yake. Hata hivyo ndani ya nafsi yake anaukemea moyo wake ambao unataka kuipweza ari yake.

"Mlaani shetani, "Sauna anauambia moyo wake. Anaendelea kujiambia kuwa yeye hakuumbiwa ujalaana, kuwa walimwengu ndio walimfinyanga upya, wakampa moyo wa ujabari. Fikiria u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kisha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna hata uso wa kumtazamia yeyote, wala kinywa cha kumwambia mamako kuhusu feli uliyotendewa. Na utamwambiaje mja huyu ambaye daima ni

mwanamke taa, atakalo baba yeye hiliridhia bila swali, na ikitokea kwamba atauliza swali, anakuwa mpokezi wa makonde, vitisho na matusi?Hebu yatie haya kwenye mizani; baada ya mwezi mmoja unaanza kushikwa na kisulisuli, kichefuchefu cha asubuhi nacho kinakuandama. Fikra zako za kitoto zinakutuma kuwaza kuwa ni malaria au homa ya matumbo. Unammwambia mama yako ambaye anaonekana kushtuka kiasi. Mama anapokupeleka hospitali, anapasuliwa mbarika, nawe limbukeni hujui lolote. Mnapofika nyumbani, anakuhoji, nawe hujui kuficha lolote, unamwambia imekuwa mazoea baba yako kukuhujumu kila apatapo nafasi. Anajisemea kuwa hili haliwezi kukubalikalKujipagaza uzazi na ulezi katika umri huu, tena mzazi mwenzio si mwingine, ila baba yako?Haya yote ni mawazo yanayoendelea katika fikra zake Sauna, na mbinu hii ndiyo uzungumzi nafsia.



**14.MAJAZ1**.

Hii ni mbinu ambayo mtunzi wa kazi ya fasihi hufananisha tabia za wahusika na majina yao halisi. Tabia zao na na majina waliyopewa. Mfano katika ukurasa wa 6;

"Maekari na maekari ya mashamba katika eneo la Kisiwa

Bora yanamilikiwa na nani?" Neno Kisiwa Bora limeturnika kimajazi kuonyesha kuwa ni mahali ambapo kulikuwa na mshamba mazuri, na labda yenye kutoa mazao kibaba, ndio maana yakanyakuliwa na yule Myunanai ili aweze kufanyia kilimo chake bora hapo.

Katika ukurasa wa 9; "Mzee Mwimo akaona ku moto, akamua kuwahamisha wake wawili wa mwisho msitu wa Heri au

Ughaishu kama walivyouita watu wa huko " Neno Msitu wa

Heri limetumika kimajazi pia, kuonyesha kuwa msitu huu ulikuwa na fanaka na wa Baraka. Labda ndio maana Mzee

Mwimo akaamua kuwahamishia wake zake huko, wakaishi kwa heri, badala ya msongamano uliokuwepo kwake nyumbani.

Katika ukurasa wa 11;"Mimi binafsi nimefanya juu chini kuhakikisha kuwa kijiji kizima kimepata maji ya mabom ba. Eneo ambalo awali likiitwa Kalahari, sasa limetwaa rangi ya Chani kiwiti " Jina Kalahari, kama lilivyoitwa eneo hib awali, lilitumika kimajazi kuonyesha jinsi eneo hilo ilikuwa limekauka mithili ya jangwa la Kalahari.

Katika ukurasa wa 13; "Siku hiyo ambayo matrekta yakit?

keleza amri ya Bwana Mkubwa, Ridhaa alitazama picha za

majumba yake matatu kwenye mulishi wa runinga " Jina

Bwana Mkubwa linatumika kimajazi kuonyesha cheo au nyadhifa alizokuwa nazo mtaajika huyo.

Jina lenyewe linaonyesha kuwa cheo chake kilikuwa cha hali ya juu, na ndiyo maana akawa na uwezo wa kutoa amri, majumba ya watu kubomolewa, na wafanya kazi wakaweza kumtii, na kutumia matrekta kutekeleza amri hiyo.

Katika ukurasa wa 15; Tunaambiwa kuwa mipaka ya kitabaka imebanwa. Kwa kweli haipo kwani hata nisemapo nang' angs ania chakula-uji haswa-na aliyekuwa waziri wa fedha miaka mitano iliyopita. Hilo usilione dogo kwani unajua kuwa wenzetu hawa katika hali ya kawaida ni watu wenye shughuli na hali zao lla sasa inabidi waniite ndugu; hasa

Ndugu Kaizari. Jina Ndugu Kaizari limetumika kimajazi kwani maana ya kaizari ni cheo cha mtawala wa zamani wa dola ya kirumi. Hivyo basi, jina hili lina maana ya mtawala wa zamani.

Katika ukurasa wa 137; Ridhaa anamtazama Shamsi akipita hapa kama afanyavyo kila siku. Mtaa anakoishi Shamsi ni mbali na hapa, unaweza kusema Shamsi na Ridhaa ni majirani. Hili la kuwa jirani wa shamsi limetokea baada ya miezi mingi ya fikira na tafakuri. Kwa kweli, huu ni mwezi wa tatu tangu Ridhaa kuhamia kwenye mtaa wa Afueni. Afueni ni mtaa wa raia wenye kima cha juu kiuchumi. Mtu anapoutazama mtaa huu anasalimiwa na majengo ya kifahari ya ghorofa, yale ambayo yanaitwa katika janibu hizi town houses. Jina

Ridhaa limetumika kirnajazi. Ridhaa maana yake ni hali ya

kukubali jambo kwa hiari. Mhusika huyu anapewa jina hili kimajazi kuonyesha kuwa ameyakubali matukio yaliyomkum.

ba yeye na familia yake, na hana budi ila kuyaendeleza maisha yake, ingawaje yamekumbwa na kiza cha mauti.

Mhusika Shamsi pia amepewa jina hili kimajazi kwani maana yake ni jua la asubuhi linapochomoza na kuleta matumaini mapya kwa watu. Mhusika huyu kazi yake kuu katika jamii ni kutunga nyimbo ambazo zinaliwaza nyoyo za watu, na pia kutumika kupitishia ujumbe tofauti kwa hadhira. Kama miale ya jua la asubuhi, mhusika huyu Shamsi analeta furaha na matumaini mapya kwa watu, kupitia kwa nyimbo zake anazotunga.

Mtaa wa Afueni pia ni jina lililotumika kimajazi, na lina maana ya ndani inayowakilisha mazingira haya halisi. Afueni ni tendo la kupungua kwa maradhi, au hali ya kupata hujambo. Hivyo basi mtaa huu ni mtaa ambao hujambo. Wanasema kuwa wanapoutazama mtaa huu, wanasalimiwa na majengo ya kifahari, ya ghorofa. Hivyo basi, watu wanaoishi katika mtaa huu ni watu matajiri watajika. Haina budi basi ila kuuita mtaa huu

'Afueni'.

Katika ukurasa wa 146;"Nilizaliwa katika kijiji cha Tokosa mimi ndiye mtoto wan ne kati ya watoyto sita. Nina wazazi wawili, ila hawa ni wazazi tu, hawajadiriki kuwa walezi wangu, wala jina 'mlezi' haliwaafiki " Kijiji cha Tokosa kimepewa jina hili kimajazi. Kutokosa ni kupika chakula kwa kuchemsha tu boila kutia viungo vyovyote kwenye chaula hicho. Hali hii

146

KUWKV O maanihirisha ukata au umaskini katika jamii, kwani anayetokosa chakula ina maana kuwa hana uwezo wa kubuni kununua hata mafuta ya kukaangia, au chumvi ya kutilia radha, na pia viungo Vingine. Kulingana na maelezo ya mwandishi, tunapata kuwa mtajwa aliyapiba masha magumu ya umasikini, kwani hata hawatambui wazazi wake kama 'wazazi',kwa kuwa hawakuwa na uwezo wa wwalea na kuwakimu wana wao kwa njia inayofaa. Hivyo basi, jjna hili 'Tokosa' lililopewa kijiji hiki lilitumika kimajazi, kumaanisha kijiji chenye ukata.

Katika ukurasa wa 149; "Basi nenda mwanakwenda, 'alisema

Fungo, 'kichukue pia kijalaana hiki chako, hata kuwepo kwenu hapa hakuzidishi hakupunguzi"Mwanakwenda ni jina lililotumiwa kimajazi, kumaanisha kuwa huyu mke kazi yake ni kwenda tu. Tunapata kuwa anasema kwamba atatokomea kokote kule, Afadhali kuishi jehanamu kuliko kwenye husuni yam Fungo. Anapoamua kuenda, anaambiwa achukue hadi kitoto chake aende nacho, basi jina hili ni la kimajazi na linatuonyesha tabia hasa ya huyu mhusika.

Katlka ukurasa wa 163;"Asante sana Neema kwa utu wak0,'akasema Mtawa huyu, 'kitoto hiki kimepata kwao. Hapa tutakjita Nasibu, Nasibu Immaculata "Mhusika Neema anapewa jina hili kimajazi. Neno neema lina maana ya mafanikio aliyonayo mtu kutokana na majaljwa ya Mwenyezi Mungu au

IJdi zake. Neema ni mhusika mwenye juhudi kwani anakjokitoto kichanga kilichokuwa kimetupwa pipani

na kukipeleka katika kitua cha polisi, na baadae wakakipeleka

kwenye hifadhi ya watoto wasiokuwa na wazazi wao lngawa hakujaaliwa na wana, baadae anapanga mwana na anakuwa wa Baraka nyingi sana kwao, na wanapendana kama mamake mzazi na mwanawe. Hivyo basi, jina Neema lilitumika kimajazi kuonyesha sifa zake mhusika huyu.

Mtawa Cizarina pia ni mhusika aliyepewa jina lake kima.

jazi. Neno mtawa lina maana ya mtu mcha Mungu anayeishi katika makazi maalumu mbali na watu wengine. Mara nyingi huwa ni mwanamke. Sifa za Cizarina ni kuwa alikuwa rntu mwenye rehema, utu, mpole, na mwenye kukaribisha. Aliishi katika kituo cha watoto, akiwashughulikia wana walioletwa hapa baada ya kutupwa na mama zao wasio kuwa na utu wala hisia. Hivyo basi jina Mtawa alilopewa Cizarina lilikuwa na maana ya ndani, kuwa alikuwa mtu mcha mungu aliyeishi katika makazi ya kituo cha watoto, mbali na watu wengine, ili kuwatumikia watoto hao.

Kitoto hiki cha kuokotwa kilipewa jina Nasibu Immaculata na

Mtawa Cizarina. Jina hili 'Nasibu' lilipewa kitoto hiki kimajazi, kwani nasibu ni neon lenye maana iliyolingana na sifa za kitoto huki. Nasibu kwanza lina maana ya jambo litokealo bila ya kutarajiiwa au kwa bahati. Pili, nasibu humaanisha kugundua au kujua ukoo wa mtu fulani. Hivyo basi, kitoto hiki kilikuwa na bahati kwani baada ya kutupwa pipani na mamake, hakikuliwa na majibwa yaliyokuwa yakichokora mapipa kutaftia mabaki ya chakula. Kitoto hiki pia hakikupatwa na magonjwa wala ajali yoyote huko mapipani, bali kilipata msamaria mwema, (Neema),aliyekichukua na kukiokoa. HiW0

basi, ni kitoto chenye bahati na Baraka pia. Kulingana na

Una

maana ya Pill ya neno Nasibu, tunaweza linganisha na maneno aliyosema Cizarina kuwa; "Najua itatokea familia hitaji kuja kutaka kumpanga kama mwanao. Siku hizi hata wali0 na watoto wao halisi hujitolea kuwachukua na kuwahalaliSha wana wa wengine kuwa wao "Hili lina maana kuwa jina hili Nasibu lilitumika kimajazi kuonyesha kuwa siku moja mtoto huyu angepata ukoo wake.

Katika ukurasa wa 169; "Mwaliko ndiye aliyeendesha gari siku hiyo; Birthday Boy akaambiwa apumzike. Walifika kwenye hoteli ya Majaliwa saa sita unusu adhuhuri; wakaketi mahali ambapo walikuwa wamezoea kuketi kila mara ambapo hawakutaka kughasiwa na pitapita za watu "Mwaliko alikuwa mhusika aliyepewa jina hili kimajazi. Neno lenyewe lina maana ya ujumbe wa kumwita mtu kwenye shughuli Fulani kwa mfano sherehe. Katika kisa hiki, kuna sherehe ya kuzaliwa kwa Umulkheri, ambayo inaendelea kwenye hoteli ya Majaliwa. Jina mwaliko linatumika kimajazi hapa, kuonyesha kuwa anawaalika watu kuja kusherehekea siku hii ya maana kwa

Umu.

Hoteli ya majaliwa pia imepewa jina lenyewe kimajazi. Neno majaliwa lina maana ya mambo yafanyikayo kwa mappenzi ya mungu. Mambo yanayofanyika katika hoteli hii ni kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu, kwani katika sherehe hizi, ndipo familia na mandugu hawa wote wanapopatana baada ya miaka mingi ya kutoishi pamoja. Mwaliko, Mwangemi, M-

wangeka, Dick, na Neema wpote wanafurahia kuwa pamoja kwa majaaliwa yake Mungu, kuwakutanisha tena wakiwa



hai. Hivyo basi, hoteli hii inapewa jina 'Majaaliwa' kimajazj.

Umulkheri pia anapewa jina kimajazi, na kuitwa 'BirthdayBoy

Hili ni kkwa sababu ile ilikuwa ni siku yake ya kuzaliwa, na kwa kweli ilikuwa yake ya kuzaliwa kwani aliweza kukutana tena na ndugu zake na furaha ikawa tele. Katika ukurasa

63-64; Familia ya bwana Kangata ilikuwa miongoni mwa zilizoselelea kwenye msitu huu. Kwa Kangata na mkewe, Ndarine, hapa palikuwa afadhali. Hawakuwa na pa kwenda, kwani hata kule ambako walikuwa wakiishi awali, hakukuwa kwao. Walikuwa wamelowea katika shamba la mwajiri wao ambaye alikuwa akiishi jijini. Waliishi hapa hata watu wakadhani kuwa hii ilikuwa milki yao. Wengine hata walidhani kuwa Kangata na familia yake walikuwa akraba kindakindaki ya mwajiri wao. Kwa hakika hata watoto wa Kangata walipokwenda shuleni walijisajilisha kama wana wa tajiri baba yao!

Jina Kangata limepewa mhusika huyu ambaye ni mzee mwenye familia na watoto wake wanakwenda shuleni.

Jina kangata linatumika kimajazi kuonyesha sifa halisi za huyu mzee. Kangata ni neno lenye maana ya kushikilia jambo mpaka ufanikiwe kutaka ukitakacho. Kulingana na kisa hiki, tunaona kuwa Kangata anashikilia kuishi kkwa tajiri wake, hadi watu wanamwona kama yeye ndiye tajiri mwenyewe. Hata watoto wake shuleni wanabadilisha majina lakiani baadae anahofia jina lake huenda likasahaulika kwani alikuwa amengata utajiri wa mkwasi huyu, hadi sifa zake zikadidimia.



**15.TASWIRA**.

Haya ni matumizi ya lughamaneno yanayojenga picha ya hali au jambo Fulani kwa msomaji. Ni mchoro au picha ya kitu au hali Fulani inayotokea katika fikira za mtu asomapo kazi ya

Katika ukurasa wa 7; Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadogowadogo, maskini, wasio na ardhi. Nadhani unaweza kukisia hali ilivyokuwa kwa familia nyingi za kiafrika. Kama vile baba Msumbili alivyokuwa akisema, jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambamo wazungu wangeamua nkuchukua vubarua kupalilia mazao yao. Kuna taswira inayojengeka kwenye akili za msomaji kuhusu jinsi hali ya familia nyingi za kiafrika ilivyokuwa, na jinsi waafrika walivyokuwa wakiishi baada ya mashamba yao kunyakuliwa na wakoloni.

Katika ukurasa wa 15;Jua lilichomoza, halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linnafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Kutokana na maelezo haya ya mvvandishi, tunajengewa taswira kuhusu mawingu makubwa angani yanayotembea kwa madaha na kufunika jua, kuna

Picha ya umeme inayojengeka akilini pia, na radi zinazofuata umeme.



Katika ukurasa wa 47; "Nakusikitikia mwanangu, kuwa huna hata familia ya kuendea. Wanuna wako wote wamean.

gamia. Mkaza mwanangu na maskini wanao waliunguzwa moto, wasibakia hata mafuvu ya kuzika!huna hata makabun ya kuwekea hayo makoja ya maua unayotunga akilini ko "Kuna picha inayojengeka akilini mwa msomaji kuhusu maneno yake Ridhaa yanayojikita katika fikra zake tu. Jinsi familia yake ilivyo angamizwa na moto, makoja ya maua ya kuweka kwenye makaburi ya hawa walioangamia; .haya yote tunayachora kwenye fikra zetu tu. Pia Ridhaa mwenyewe anayachora mawazo haya akilini mwake tu, na kufikiri jinsi mwanawe anavyowaza kuhusiana na suala hilo.

**16.MASWAL1 YA BALAGHA**.

Haya ni maswali yanayoulizwa na msimulizi au mhusika ambayo hayahitaji jibu. Wakati mwingine yaweza kuitwa mubalagha. Assumpta K. Matei pia amejikita katika matumizi ya maswali ya baalagha katika kazi yake ya Chozi la Heri kama tunavyoona katika ukurasa wa kumi na moja.

Katika ukurasa wa 12; "Je, huu si mchango tosha wa mtu kuitwa ndugu hata angawa mgeni?Kweli jaza ya hisani madhila?Vipi watu wawa hawa walioniita 'ndugu' na

'mzee',tukala na kunywa pamoja, tukazungumza ya kupwa na kujaa wananilipulia aila na kuyasambaratisha maisha yangu7

Ridhaa hakujua majibu ya maswali haya " Haya ni maswali aliyojiuliza Ridhaa lakini hayakuhitaji majibu, hivyo basi ikawa ni mbinu ya kutumia maswali ya mbalgha katika kazi ya kifasihi.



**17.UKINZAN1TANAKUZ1**.

Hii ni mbinu ya kusisitiza ujumbe kwa kuambatanisha maneno ya kinyume au yanayokinzana. Kukinzana ni hali ya kutofautiana, au kuwa na ubishani, au yenye kutokubaliana. Mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri amejikita katika matumiZi ya ukinzani katika kuwasilisha maudhui yake kwa njia zifuatazo.

Katika ukurasa wa 14; "Na usidhani ni mazingira mageni, kweli si mageni, si mageni kwani tu mumu humu mwetu, hatumo ughaibuni wala nchi jirani. Tu katika jimbo lile lile tulilozoea, kilichobadilika ni kijiji tu, ni kama kutoka chumba cha malazi, kwenda sebuleni!"Kuna mkinzano wa mawazo kuwa mazingira yamebadoilika ilhali la, ni yale yale tu ya awali, waliyozoea, ni sehemu tu wamehama wakaenda katika sehemu tofauti, ya m, azingira yale yale. Anathibitisha haya kwa kufananisha hali hii na kutoka chumba cha malazi, kwenda sebuleni. Katika ukurasa wa 15; "Mipaka ya kitabaka imebanwa. Kwa kweli haipo kwani hata sasa nisemapo nang' ang' ania chakula-uji haswa-na aliyekuwa waziri wa fedha miaka mitano iliyopita " Kuna mkinzano wa mawazo tunapoambiwa kuwa kwa sasa, wanang' ang' ania chakula, la sio chakula, bali uji, na aliye kuwa waziri wa fedha miaka mitano iliyopita.

Katika ukurasa wa 16; Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu kwa mbali namwona Ridhaa-mwamu hasa-akitafuna kitu Fulani, nadhani ni mzizi mwitu!Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi!daktari mzima!mkurugenzi mzima wa wakfu wa matibabu nchini. Wanasema wajuao kuuwa samba akikosa



nyama hula nyasi. Wazo hill linaleta mkinzano Kwenye hkra za msomaji kwani si kawaida ya daktari mzima na mwenye cheo na wadhifa aina ile kua akila mizizi msituni, lakini lisilo budi hubidi, na hivyo basi, inambidi aile mizizi tu, badala ya kuangamizwa na njaa.

**18.TASHBIHI**.

Hii ni mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; kama, mithili ya, sawa na, au pia ja. Assumpta K.Matei amejikita katika matumizi ya mbinu hii ya tashbihi katika kazi yake ya kuwasilisha maudhui kwa msomaji kwa njia zifuatazo;

Katika ukurasa wa 16; "Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira!" Uso wake unalinganishwa na unga wa ngano uliotiwa hamira kwa jinsi ulivyo vimbiana kwa majeraha. Katika ukurasa wa 49; Sasa ninaamini usemi wa Tila wa kila mara kuwa:

"Usicheze na uwezo wa vijana, wao ni kama nanga. Huweza kuzamisha na kuiongoa merikebu " Uwezo wa vijana unalinganishwa na nanga, ambayo iko na uwezo wa kuzamisha na kuongoa melikebu.

154

**i9.LAKADU**

Hii ni mbinu ya mhusika kupewakubandikwa jina na wahusikawengine amayeye mwenyewe kujibandika jiana linalooana na tabia au sifa zake.

Katikaukurasawa70;"SasaLunganimkulimastadi. Marafikizakewamempajinalamsimbo Mkulima NambaWani"Lungaanapewajinahililamsimbo kwa sifa yake ya ukulima hodari. Hakuna anayempiku katika Nyanja za ukulima.

**MBINU ZA SANAA.**

**I. KINAYA.**

Hii ni mbinu inayofanya matukio katika kazi ya Sanaa kuwa kinyume na matarajio ya hadhira.

Katikaukurasawa5;"Naonaumeanzakuitiaakili yangukwenyemtihanimgumu.Unanichanganya hasa!Kwanza sijui wapi kapata moto wa miaka hamsini " Ni kinaya kuwa mototo ana miaka hamsini, kinyume na matarajio ya kawaida ya kuwa mototo ni yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane.

Katika ukurasa wa 62; Mwangeka aliajiriwa na kupanda ngazi moja baada ya nyingine hadi alipoendakudumishaAmanikwingine,namkewe kufa kutokana na ukosefu wa usalama nchini mwao huu ukawa mwisho wa ndoa yao ya miaka mitatu. Ni kinaya kuwa Mwangeka anaenda kuweka usalama kwenye mataifa mengine ilhali kwao bado usalama ni balaa, -

na hili linasababisha kuuliwa kwa mkewe.

155

Katika ukurasa wa 65; Alipofikiria kila asubuhi, kama alivyo_

sikika akisema, alihisi kinaya. Wanawe walipoenda kusomea

Ngambo, kama wafanyavyo wana wa viongozi ambao wana_

iona elimu ya humu kama isiyowahakikishia mustakabalimwemaraiyawake,...Nikinayakuwa viongozi wa nchi za kiafrika wanaiona elimu ya humu kuwa duni ilhali ni wao wanaoisimamia elimu yenyewe; badala, wanawapeleka Wana wao kusomea nchini za mbali ambako wanadhania kuwa kiwango cha elimu ki juu.

Katikaukurasawa65;This country has nothing to offer. Nchi ambayo hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mishahara ya mkia wa mbuzi!mimi sitakufa maskini acha niwkeze huku mbali ambako Sina hofu ya mali yangu kuibwa au kuchomwa na waivu wangu... Ni kinaya kuwa wana hawa wanakataa kurudi kwao nyumbani walikozaliwa kwa kuona kuwa hali ya maisha huku ni duni sana na si ya kiwango walichofikia huko ughaibuni walikoenda kupata elimu.

Ni kinaya kuwa kiongozi wa dini anawaambia watu 'amani iwe nanyi'ilhali hawa watu hawana Amani kwani chakula, mavuzi na makao hawana. Wanaishi msituni kama wanyama pori; Katika ukurasa wa 28;"...haikosi alikuwa kiongozi wa kidini-alitoka na kutusalimu: peace be with you, .

2.**SADFA**.

Sadfa ni mgongano wa vitendo viwili vinavyohusiana kkana kwamba vimepangwa, japo havikuwa vimepangwa.

Katika ukurasa wa 175; "Tesi!sadfa gani hii?Unafanya nini

h apa?Ulikuja lini jijini humu?Yu wapi wifi Nema?Niliskia motto wenu amehitimu chuoni!Ajabu hatujapata kukutana naye, 'Mwangeka aliyauliza

maswali haya moja baada ya lingine bila kumpa mwnzake muda wa kujibu hata la kwanza wengine walimtazama wakishangaa kwa nini hata hamwachi mgeni akawasalimu "Hii ni sadfa kubwa sana mimi huwa siji hapa sana lakini mwanangu Mwaliko alinganganiakunileta hapa kwa chakula cha mchana "

sadfa inajitokeza wakati Mwangeka na Tesi wanakutana mahali pamoja, ilhali hawakuwa wamepanga lolote kuhusu mkutano wao. Jambo hili linatokana na uwezo wake Mungu bali si kwa mipango ya hawa wa wahusika wawili.

Katika ukurasa wa 175; "Nakumbuka sana. Na kweli hii ni sadfa kwa sababu pia ni siku ya kuzaliwa kwa binti yangu

Umulkheri " Inasadifu pia kuwa wote wanakutana pamoja siku ya kuzaliwa kwake Umulkheri.

Katika ukurasa wa 183; "Tunawatarajia walioenda sokoni kurui. Kisadfa, wakati huo huo, babu Mwimo Msumbili akawa ndio anatoka kwenye shughuli zake za usili (ujaji)" Inasadifu kuwa wakati watu wanapotarajiwa kuwa wakirudi, wakati huohuo babu Msumbili akawa amewasili kutoka shughuli zake.

3.**KISENGERE NYUMA**.

Katika mbinu hii, mwandishi hurudi nyuma na kusimulia kisa kilichokuwa kimetendeka kabla ya alichokuwa ana



simulia. Aidha mwandishi hubadilishawa I wa masimuliZi kuwa wakati wa kisa hicho. Mbinu hii hutumika sana kuonk sha mhusika anapokumbuka kitu, au kutuelezea jinsi mambo yalivyoanza. Mbinu hii pia hujulikana kama mbinu rejeshi.

Katika ukurasa wa 1;"Sasa anakumbuka vyema. Anakumbuka kupepesa kwa jicho lake la kuli kwa muda wa wiki mbili mtawaliwa. Anakumbuka anguko aliloanguka nalo sebuleni mwake, akatafuta kilichomfanya kujikwaa asikione. Anakum. buka mavune yaliyouandama mwili wake na kuunyongonye za kwa muda hata pasi na kuudhili kwa kazi yoyote ya haja. Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa ya maktaba yake ya nyumbani adhuhuri ya juzi ile "

Ridhaa anayakumbuka yaliyokuwa yametendeka ingawa ilikuwa miaka mingi iliyopita.

Katika ukurasa wa 3;"Katikati ya mito hiyo ya machozi, Ridhaa aliileta picha ya maisha yake mbele ya kipaji chake. Alijiona akiamka asubuhi ambayo ilizaa usiku wa jana, usiku ambao ulitandaza kiza maishani mwake. Kwa mbali alianza kuskia sauti ya mkewe ikilia kwa kite "Anakumbuka akiskia mlipuk0

mkubwa, kasha kushikwa na uziwi wa muda uliofwata na sauti nyingine ya mkewe, yamekwisha!" Haya yote ni mawazo yanayomjia Ridhaa. Ni matukio yaliyotendeka zamani lakini mawazo haya bado yako akilini mmwake, hayajafutikatna anayarelea kila wakati kwenye fikrazake.

Kurasa 9-10; Hapa Ridhaa anayakumbuka maisha yac

tangu utotonj nadi akiwa mtu mzima, mkondo ambao maisha yake yamechukua. Anakumbuka jinsi siku ya kwanza shuleni aljwotengwa na wenzake katika mchezo wao wa kuvuta, mchezo wa kusukuma vifuniko vya chupa za soda kwa ncha za vidole vyao. Anakumbuka mwanafunzi mmoja ambaye kwa kawaida aljpenda kuwachokoza wenzake akimwambia, wewe ni mfuata mvua. Hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa wtushinda katika mitihani yote. Wewe ndiwe unayetuibia kalamu zetu.

Katika ukurasa wa 13; Siku hiyo ambayo matrekta yakitekeleza amri ya bwana mkubwa, Ridhaa alitazama picha za majumba yake matatu kwenye mulishi wa runinga. Anayatazama hata sasa katika ruya yake. Majumba haya sasa yamegeuka dongo. Anayasoma usingizini na kutoa kidoko ambacho tribu kimwamshe. Hili la sasa ni pigo la pili ambalo ni kali

Zaidi. Hapa pia Ridhaa anaendelea kuyawaza matukio yaliyompata nyakati zile ambazo mali yake ilipoharibiwa.

Katika ukurasa wa 45; Sasa Ridhaa anapotazama picha iliyo mbele ya macho ya akili yake, anajua fika kuwa Tila wake hayupo, kilichobaki ni kumbukumbu ambazo zinang' ata kama mkia wa nge, kumbukumbu ambazo kila mara zilifungua

Chemchemi za machozi, yakalovya kifua chake. Ridhaa anakumbuka mwana wake na kulia kwa machungu aliyokuwa nayo moyoni mwake.

4. **NYIMB0**.

ni maneno na sauti zilizopangwa na huandamana na

muziki unaotokana na ala za kimuziki kama vile ngoma saut hizi za muziki pia huwa zimepangwa ili kuandamana maneno vizuri na kwa urari. Wimbo huweza kutuumika kupitisha ujumbe wa mwandishi ambao ni dhamira. Katika riwaya hii, kuna matumizi ya nyimbo katika matukio tofaut:

Katika ukurasa wa 20; "Wote walikuwa wakighani rnkarara huu: Tawala Wahafidhina tawala, Mwanzi wetu tawala Waha.

fidhina tawala 'Wimbo huu ulitumika wakati wa shughuli kupiga kampeni kabla ya uchaguzi kufika. Wimbo wenyewe unampigia dembe kiongozi anayetakwa na wananchi.

Katika ukurasa wa 49;"Mama mtu angemshika mabegani na kumwimbia mkarara mmoja wa wimbo pendwa wa kidini:

Salama, salama

Rohoni, rohoni

Ni salama, rohoni mwangu"

Katika ukurasa wa 60; "Wengine walijilazimisha kupiga ukemi, eti wanaomboleza kifo cha Dedan Kimathi.

*Walianza kulizunguka lile 'jeneza' wakiimba mbolezi.*

*Walimwimbia Kim wao, kwaheri.*

*Kwaheri we Kim wetu*

*Kwaheri, kwaheri*

*Kwaheri we Kim kipenzi chetu kwaheri*

*Kwaheri na malaika wakungoje.*

*Umewaacha wazazi kwa majonzi*

*Kwaheri, kwaheri*

*umewaacna nauguzo kwa ukiwa*

*Kwaheri na mababu wakulaki peponi.*

*Kurasa 129-135; Huu ni Wimbo ambao Shamsi aliuimba kuhusiana na hali ya kisiasa iliyokuwemo nchini. Haukuwa*

*Alimwimbia Chupa ambaye alikuwa kipenzi chake.*

*Alikuwa mboni yajicho lake, mwendani wake.*

*Alikuwa shujaa, Hakuhisi shinikizo la majabali, Alimzingira kwa mahangaiko pia, Alimjaza kwa tuo, Akampa maji matamu*

*Maji hayo yakawa dawa mujarabu.*

*Dawa hiyo ikawa ya kuuguzia banguzi.*

*Waliomsababishia mahasidi.*

*Chupa yake, alijua pia walimcheka*

*Wachunguliao kwenye madirisha*

*Waliokwenye maroshani yao "*

Kurasa 136-137; Kwa sauti ya chini, Ridhaa alisema kuwa

Shamsi anasikika kama amebadilisha wimbo wake. Huu wa leo unahisika kama wa kiumbe mwenye maumivu zaidi, mapigo yake hasa ni ya mbolezi, ni

tofauti na yale majigambo yake ya kila siku, Akaongeza Ridhaa huku akiyaghani majigambo

Ya Shamsi kwa sauti ya chini kama anayeyatia maneno ya majigambo yenyewe kwenye mizani.

Anasema kuwa hawa wanaomfuata wanamwacha kwa ukoo wake mtukufu.

tlen

Kwa jadi yenye majagina, wa mioyo na vitendo

Wananicha kwa kuwa wa kwanza kijijini

Kuvishwa taji kwa kusoma kwa bidii

Kwa kuwa jogoo wa kwanza kuwika kwenye anga za elimu

Idhini nikapewa ya kuendeleza utafiti, Nikapewa mamlaka ya kuwaza kwa niaba ya jamii.

***<u>5. MATUMIZ1 YA BARUA.</u>***

Lunga anapokea barua rasmi ya kumfuta kazi. Ni fupi lakini yenye ukali na kukatisha tamaa (Uk 72;) Barua yenyewe iliandikwa na bwana Kalima ambaye alikuwa mwenyekiti wa

Halmashauri ya kitaifa ya uhifadhi wa nafaka. Yeye ni mkuru.

genzi wa Halmashauri ya Kitaifa ya Uhifadhi wa Nafaka. Anamwandikia bwana Lunga waraka na kumwambia kuwa amestaafishwa kazi. Anastaafishwa kazi kutokana na gharama ya uzalishaji mali ambayo inaendelea kupanda kila uchao, shirika hilo limekumbwa na changamoto kubwa ya kifedha. Halmashauri inayosimamia shirika hili imeamua kupunguza idadi ya wafanyakazi katika ngazi za juu, kama hatua mojawapo ya kudhibiti gharama ya uzalishaji. Shirika hilo lilisikitika kumwarifu Lunga kuwa yeye ni mmoja wa walioadhirika na kwamba ameachishwa kazi kuanzia tarehe

31 mwezi wa Julai, mwaka huo. Shirika hili lilimshukurU

Lunga kwa uwajibikaji wake alionao katika utenda kazi wake. Pia walimshukuru kwa mchango wake katika kuliendeleza shirika hilo. Shirika hilo pia lilimtakia kila laheri bwana

Lunga, katika shughuli zake za kitaaluma.

Lunga pia anaandikiwa waraka mwingine mfupi na mkewe

162

Naomi (uk 81) Mkewe Naomi anamwambia kuwa ameondoka. Ameenda kutamba na ulimwengu, na huenda akaambulia cha kumsaidia mumewe kuikimu familia yaao. Anasema kuwa anasikitika kwa uchungu atakaousababisha kwa mumewe na pia wana wao. Baada ya kumwandikia waraka huu, anam wambia kwaheri. Barua hii pia inamuumiza sana Lunga moyom, kwam aliachiwa watoto na mkewe awalee peke yake. Pia ni uchungu kwani alimdhamini na kumpenda sana mkewe

Naomi ambaye sasa amemwacha katika hali ya upweke. Subira pia anamwandikia mwanawe Mwanaheri barua, akimjulisha kuwa yeye amekwenda zake na labda hawatapatana tena maishani. Barua hii pia ni ya kukatisha tamaa kwani

Mwanaheri alipoisoma barua ile, alihisi kuwa imejaa ujumbe wa mauti (UK.95)Barua hii inaandikwa tarehe mbili mwezi wa sita mwaka wa elfu mbili na tisa. Inaandikwa kwa mpenzi wake Mwanaheri. Anasema kuwa, Mwanaheri atakapoisoma barua ile, labda yeye hatakuwa hapo au pia katika ulimwngu huu. Ila tu ajue kuwa imembidi kuondoka. Anasema kuwa hakudhamiria kuondoka au hata kuawaacha kwa siku moja yeye na Li me, wa la hata baba yao. Lakini uvumilivu wake ulishindwa kumletea mbivu. Anasema kuwa amemeza shubira kwa miaka mingi, kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiwa kwa asiyoyatenda. Anaendelea kusema kuwa amechoka kukilovya kifua chake kwa machozi kila mara.

Amechoka kuitwa mwizi wa mayai ambayo kuku wayatagayo amewafuga yeye. Amechoka kuitwa mwizi wa mali yake. Amechoka pia kupigania penzi la mwenzi na mavyaa na mwenzi mwenyewe haoni anampagaza machungu. Anajuta sana kwa kuwaacha wana

kuwa kila binadamu ana jukumu la kudumisha Amani na usalama. Hata hivyo, wafanyakazi wa umma, na hasa polisi na wanajeshi wana jukumU kubwa Zaidi la kudumisha usalama na Amani.

164

wake. Hata hivyo, anaomba jambo moja tu kwa rnwanawe

Mwanaheri: kuwa amtunze Lime, na Zaidi mno wamtii baba yao na pia kuzingatia masomo yao. Anaomba pia Mwenyei

Mungu aweze kuwaepusha kutokana na maovu yote. Asitokee mja akawadhulumu furaha yao jinsi tu ulimwengu Ulivyomhi.

ni utulivu. Baadaye anawaambia wanawe kwaheri na kuwaambia kuwa wangeweza kupatana siku moja, inshallah.

Hiyo ikawa ni barua yake Subira ambaye alikuwa mamke

Mwanaheri.

6. **HOTUBA**.

Haya ni mazunguzmzo yanayohusu jambo maalum kwa mfano siasa ambayo hutolewa kwa hadhira na mtu mmoja.

(uk 112-114), Hotuba hii inatolewa na Apondi, Alianza kwa kuiita hadhira kwa maneno, "Mabibi na mabwana"Anaendelea na kusema kuwa swala la usalama haliwezi tena kupuuzwa. Anasema kuwa usalama umekuwa mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu. Na kwa hakika, tunaweza kusema kuwa usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu. Kwa hakika, usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi.

Anasema kuwa bila usalama, binadamu hawezi hata kushiriki katika shughuli za kuzalisha mali, hivyo hata mahitaji yake mengine ya kimsingi kama vile chakula, malazi na makazi hayawezi kukidhiwa. Anasema

kuwa kila mmoja anafaa kupakata mikono na kungoja kuliniwa, la hasha!Kila mmoja wetu anastahili kuhakikisha kuwa ameepuka vitendo vya Khalifu. Anasema kuwa pia ni vyema mtu kuwaangaza wahalifu wakati wote. Vikosi vya poliSi na wanajeshi vimefunzwa maarifa ya kukabiliana na kadhia za jinai na upelelezi; Kwa hiW0,wana dhima kubwa Zaidi ya kudumisha Amani. Aidha, wana ujuzi wa njia mwafaka za kutatua migogoro na kupalilia maridhiano. Wanajua ni lini watashambulia na ni lini watarudi kinyumenyume, kuepuka shambulizi la adui. Anawasihi waajibike Zaidi katika kazi zao, kwa kuwa wamefunzwa effective communication and conflict resolu-

Kurasa za 68-69;Kila ijumaa wakati wa gwaride, ungemskia akihutubia kwa mhemko "Mkuu wa shule, walimu na wanafunzi, suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumeona jinsi misitu ilivyovamiwa na viongozi wenyw mate ya fisi. Nasikia baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali za umma wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kuwapoka makazi yao. MaeIfu ya maekari ya misitu yamefyekwa na kujengwa viwanda. Badala ya miambakofi na miti mingine inayosafisha hewa, michai imetwaa nafasi yake. Wanaohusika na matendo haya wanapoulizwa huidai kuwa michai Si adui ya mazingira!wengine wanasema kuwa misitu haina bui kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula, kwani jamii lazima ijitosheleze kwa chakula. La kuhuzunisha ni kwamba hawa hawa wanaosema hivyo ndio wanaokita majengo ya kifahari katika sehemu ambazo zinastahili kutengwa

upanzi wa chakula!Wengine wamediriki kunyakua hata mad.

habahu kwenye mlima wa Nasibu ili kujenga hoteli kubwa kitalii. Wazee wetu hata hawana mahali pa kuchomea kafara!

Tunakata miti bila kupanda mingine. Tazameni shuleni humu!Hata mabustani ya maua tunashindwa kuyastaw.

isha!Tukiendelea hivyo, bila shaka sehemu yetu itazidi kuwa jangwa"

7. **MAHOJIANO**.

Hii ni mbinu ya kuuliza maswali ili kufahamu maarifa anayojua mtu. Mahojiano hutumika mtu atakapo kupata taarifa ulani kutoka kwa mtu mwingine anayehojiwa.

Kuna mahojiano yanayoendelea kwenye kituo cha polisi, wakati mwanapolisi aliye katika zamu anapomdadisi

Umulkheri (uk 83).

"Umasema watoto walipotea?unajuaje walipotea?"

"Kwanza walikuwa wamevaa vipi walipoondoka nyumbani?

"Walibeba nini?walikwambia wameenda wapi?Kwanini watoto wenyewe hawajaandikisha kupotea kwao kwenye

"unasema pia kijakazi wenu hayupo?"akauliza askari.

"na hakukujuza alikokwenda?"aliongeza askari yule.

"Jina la huyo kijakazi?"akauliza yule askari wa kwanza.

Katika ukurasa wa 100;"pacha aliyeonekana kutoyaamini maneno yangu alinidadisi: '

"una hakika na unayoyasema?"

**8. TAHARUK1**

Hii ni mbinu ya kusimulia au kuandika riwaya kwa kufanya hadhira au wasomi wajawe na hamu ya kutaka kujua kitakach0tokea baadaye; hamu ya kutaka kuendelea kusoma. Baadhi ya hadithi huishia kwa taharuki na kulazimisha hadhira yake ijikamilishie au ibaki ikijiuliza maswali.

Taharuki pia yaweza kujitokeza katika hali ya kawaida wakati jambo fulani linatarajiwa kutendeka, aidha jambo nzuri au la kukatisha tamaa.

Katika ukurasa wa 19; "Mijadala hii ilizua na kukuza migogoro isiyomithilika. Hali ya taharuki ilitamalaki, vyombo vya dola vikatumwa kudumisha usalama katika vijiji, mitaa ikajaa Sisimizi walioshika bunduki. Hali hii ilileta chachawizo Zaidi katika vijiji na mitaa " Katika hali hii, kulikuwa na taharuki juu ya mambo yaliyotarajiwa kutokea baada ya mtafaruku uliokuweko kwa sababu ya siasa.

Katika ukurasa wa 152;"Usisnitazame kana kwamba unataka nikwambe yaliyotokea baadaye, 'nilijisemea kana kwamba ninajibu mtazamo wa ndio kuniambia kwani nilijipata hapa penu, oete aliongeza na kukatisha ghafla usimulizi uliokuwa mawazoni mwake. Pete anatuacha na taharuki bila kutuambia yaliyotokea baadaye. Anakatisha masimulizi yake kwa ghafla.

9. **MASIMULIZ1**.

Haya ni maelezo ya jambo fulani kwa njia ya

kusimulia. Mwandishi ametumia mbinu hii kuwasilisha maud.

hui yake kwenye riwaya hii.

Katika ukurasa wa 16; "kumbe hata wewe shemeji Kaizari upo?Ridhaa ananiuliza kwa unyonge. Hili linanizindua kutoka lepe langu la muda, linanitonesha kidonda si haba 'Ndio tu hapa na wengine wengi, 'ninamjibu, kasha ninaanza kumsimulia yaliyojiri kana kwamba ni mgeni wa hali ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu hakustahili kuiongoza jamii ya wahafidhina, kisa na maana, alikuwa mwanamke, mbingu zilishuka. Watu

walishika silaha kupigania na uhuru wao; uhuru ambao walidai kuwa hawakupewa, waliupigania "Anasimulia jinsi uongozi wa nchi ulivyo, na jinsi uhuru ulipiganiwa.

Katika ukurasa wa 146; Pete anasimulia kisa cha maisha yake kwa marafiki zake akina Selume "Pete alifungua pazia la jukwaa la maisha yake, akaanza kuwasimulia akina Selume kisa chake mwanzoni, kimya kimya moyoni akisema kwamba huenda wakakielewa kiini chake kutenda alichokitenda 'Nilizaliwa katika kijiji cha Tokosa. Mimi ndiye mtoto wa nne katika familia yenye watoto sita. Nina wazazi wawili, ila hawa ni wazazi tu, hawajadiriki kuwa walezi wangu, wala jina mlezi haliwaafiki. Naona mnaniuliza vipi mtu kuwa mzazi na asiwe mlezi Ila nataka mjue kuwa haya hutokea mara nyingi. Hamuwezi kujua haya nyinyi, yaonekana mlilelewa kwa nun na cerelac, hamjaonja shubiri ya maisha "



"Maneno haya yalifunga pazia la jukwaa la mawazo ya Neema, akaanza kumsimulia mumewe, la, kuisimulia hadithi aliyoitunga yeye mwenyewe kwa matendo yake miaka kumi iliyopita 'siku hizo nilikuwa nikifanya kazi kama hasibu mwandamizi katika hazina ya kitaifa, 'alianza Neema "Asubuhi moja ya ummande ilinipata nimeshuka kutoka kwenye daladala, nashika tariki kuelekea afisini. Mzizimo wa Julai ulidhulumu ngozi yangu laini, nikalaani msongamano wa magari jijini, ukosefu wa mahali pa kuegeshea, na ada kubwa iliyotozwa walioazimia kuendesha magari yao hadi kitovu cha jiji. Laiti vinara wa jiji wangeweza kuboresha hali, ningeweza kulitumia gari langu " Neema anamsimulia mumewe Mwangemi kuhusu matukio yalivyokuwa siku hizo zilizokuwa zimepita.

Katika ukurasa wa 162; "Nilimsimulia Cizarina kisa changu alikisikiliza bila kuonyesha hisia yoyote ya kushtuka ila uso wake ulitwaa vituta vilivyoficha huzuni na kuudhika " Neema anamwelezea Cizarina kwa njia ya masimulizi jinsi alivyoweza kukiokota kitoto kilichokuwa kimetupwa kwenye jaa la taka ili kiage dunia ama kipate msamaria mwema wa kukichukua kitoto kile.

**<u>IO.MAZUNGUMZO</u>**.

Haya ni majailiano ya jambo Fulani baina ya watu wawili au

Zaidi. Kila mtu huzungumza kwa wakati wake, na kumpa mwingine nafasi ya kusikiliza.

Uk 38;

"Tila:



Shikamoo baba.

Ridhaa:

Marahaba mwanangu. Umeshindaje?

Tila:

(kwa uchangamfu)vyema. Baba, leo somo letu la fasihi lilivutia mno.

Ridhaa:

Kwani waliwafunza nini huko?Ama ni zile siasa zenu zisizoisha?

Leo mwalimu Meli alitueleza jinsi mifumo ya uzal-

Tila:

ishaji mmali ilivyobadilika, kuanzia wakati wa ujima, ukabila, ubwanyenye, ujamaa hadi sasa tunapopambana na utandawazi. Lakini anasema ujamaa si rahisi kutekelezwa.

Ridhaa: (kwa wasiwasi) Kipi kiini hasa cha kufunza mada hii kwa watoto wakembe kama nyinyi?siku zetu sikumbuki kuona mada hii hata katika mtalaa wa kidato cha sita!

Nadhani umesahau baba. Suala hili ulisema limeshu-

Tila:

ghulikiwa katika kazi za kifasihi kama vile Mashetani, ile tamthilia ya Hussein inayoisawiri migogoro ya kisiasa, kiuchU-

mi na kijamii ya baada ya ukoloni Isitoshe, mwalimu alitaka tu kuonyesha kwamba upo uhusiano kati ya mfumo wa kiuchU

170

na rmurnv wa Kislasa alituambia kwamba mfumo wa kiuchumi hudhibitiana na mfumo wa kisiasa. Utawala huteuliwa makusUdi kuendeleza mfumo uliopo wa kiuchumi kwa maslaya watawala na tabaka ambalo linazimiliki nyenzo za uzalishaji mmali.

(kama aliyeudhika).Naona mmeanza kuingjlia

Ridhaa:

Nyanja ambazo ni michezo yaw engine na wanafaa kuachiwa wao.

Lakini baba, unajua hatuwezi kuyafumbia macho

Tila:

mabadiliko yanayozikumba jamii zetu kwa mfano, kura ya maoni ya hivi maajuzi yaonyesha kwamba majimbo mengi nchini yanamuunga mkono Bi. Mwekevu Tendakazi. Ameongoza kwa asilimia sitini. Mpinzani wake wa karibu wa kiume ana asilimia thelahini. Mwalimu alisema kuwa wakati umefika kwa jamii kuacha kuacha kupima uwajibikaji wa mtu kwa misingi ya kijinsia. Wote waume kwa wake wapewe nafasi sawa.

Si kwamaba napinga hili. Ningekuwa hasidi wa

Ridhaa:

usawa wa kijinsia nisingewapelekeni nyinyi shuleni. Ningemshughulikia Mwangeka tu ambaye jamii inaamini kuwa nndiye mridhi wa mali yangu.

Hata hivyo, naona kwamba ni mapema mno kuanza kulitolea hukumu suala la nani anaongoza. Huku kutakuwa kukata mbeleko kabla ya mtoto kuzaliwa.

171

(akichekacheka)Dalili ya mvua ni mawingu baba. Mara hii kama wapiga kura tumeamua kujaribu rnbinju mpya za kilimo. Haya matumzi ya visagalimma yarneanza kupitwa na wakati.

Ridhaa: Tila!Kummbuka hapo ulipo hata kura yenyewe hauna!Naona wamekutia maneno ya uchokozi. Ngojea kipindi kingine cha uchaguzi kifike, utakuwa na haki ya kUChukua kura na kumpigia mwanamke umtakaye. Kwa sasa itabidi utosheke na chaguo letu!

Tila: Lakini baba, sijasema tunataka kipongozi mwanamke. Sisi tunataka kiongozi yeyote awe mwanamke au mwamume, atakayeweza kulielekeza jahazi hili letu kwenye visiwa vya hazina. Tufikie kilele cha maendeleo pale tutakapofikia malengo ya nkimaenndeleo ya kimilenia. Kiongozi ambaye ataendeleza Zaidi juhudi za kukabiliana na na wale maadui ambao wewe daima huniambii kuhusu: umaskini, ujinga, magonjw (akisita kumtazama baba) uhaba wa nafasi za kazi na ufuisadi. Je, huu sio uliokuwa muono wa waliopigania uhuru?siyo ambayo viongozi waliochukua hatamu za uongozi kutoka kwa watu weupe waliyofanya juu chini kutekeleza?

Ridhaa:

Na nani akasema viongozi waliopo hawajajikuna wajipatapo?Huoni hata wahasiriwa wa magonjwa sugu kama vile iri na hata UKIMWI wana dawa za bei nafuu za kuwawezesha kudhibiti hali hizi?Je, serikali haijaanzisha sera ya elimu bila malipo kwa Shule zote za msingi?Haijagharamia karo za Shule za kutwa katika Shule za upili?kumbuka pia na

172

ule mradi wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi kuanzia darasa la kwanza ana kipakatalishi

chake?Ushaona?Hivi karibuni, nchi Inafikia ile vision 2030 hata kabla ya 2030 yenyewe!

Je, ni tume ngapi za kuchunguza kashfa za kifisadi ambazo zimeundwa?Hizo si juhudi za kupigana na ufisadi?Serikali imetumia bilioni ngapi katika shughuli ya kuhesabiwa kwa watu mwaka jana?Unajua sababu ya shughuli hiiTvoiongozi wanataka kupata takwimu sahihi Zaidi na za kutegemewa, zitakazowawezesha viongozi kujua mahitaji ya kiuchumi na ya kijamii ya kila jimbo. Huduma zitaweza kutolewa kwa urahisi

Zaidi katika kila eneoo la ugatuzi. Tila: Na umaskini, je, baba?Mara nyingi hukuona umejishika tama ukilalamikia asilimia kubwa ya raia ambao hawamudu hata gharama ya matibabu ya kimsingi si wewe unayesema kwamba vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano husababishwa na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa lishe bora, pamoja na wazazi na walezi kutopata elimu kuhusu njia za kujikinga dhidi ya baadhi ya magonjwa?

Ridhaa: (kwa msisitizo)Kumbuka kwamba haya malengo ya kimilenia hayajaanza kupigiwa

Shabaha sasa. Kilichobadilika ni istilahi ya kuyarejelea jawapo ya haki za kibinadamu ambazo wanaharakati mapinduzi walipigania ni matibabu boila malipo kwa wasioji.

weza kiuchumi, na elimu ya lazima, na bila malipo kwa watoto wote, kufikia umri wa miaka kumi na mitano. Na nadhani kile ambacho mmwalimu wenu angewasisitizia Zaidi ni kwamba vijana wana jukumu la kuelimishana kuhusu nafasi ya kila mmoja wao katika kuuboresha uongozi uliopo sasa. Watumie vipawa vyao kwa njia endelevu ili kusaidia katika kuzalisha nafasi za kazi badala ya kungojea serikali iwatilie riziki vinywani. Nchi haijjengwi kwa mihemko na papara za ujana. Na suala la umaskini?Naona hili ni tatizo la kijaamii. Mathalan, watu wanaoishi katika sehemu kame wanastahili kujitahidi kuvumbua mbinu za kuyahifahi maji ya mvua. Pia kila eneo la ugatuzi halina budi kuwashajiisha wataalamu wake kujizika katika uafiti ili kuvumbua rasilimali

zinazopatiakana katika maeneo haya, hili litawawezesha maeneo yenyewe kuzitumia raslimali kwa njia endelevu. Haya yote yatasaidia kupunguzu mng' ato wa uhawinde.

Tila: Watayahifadhi vipi maji haya kama mvua yenyewe hainyeshi?Baba, wewe mwenyewe unalalamika kiangazi ambacho kimmezikumba sehemu mbalimbali nchini lsitoshe, mwalimu asema kwamba asilimia kubwa ya wakazi wa sehemu kame haiwezi hata kumudu kula mara mbili kwa siku. Hiz0

hela za kununulia matangi ya kuhifadhia maji na kufanyia utafiti watazitoa wapi?

Ridhaa: Basi watumie maji ya mabombalSi lazima wahifadhi ya mvualNa huyo mwalimu naona anapanda mbegu za uhasama kati ya viongozi na vijana. Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu za kuvulia, nao wanaona wangoje kuletewa samaki!

Tila: (akionyesha kuvunjika moyo)Baba!Umekuwa kama yule kiongozi wa kifaransa, unayeniambia wewe kila mara, ambaye alipoambiwa kuwa wanyonge hawakuwa na mkate alisema, "if there is no bread, let them eat cake!"

Watu wengi huko mashambani hutegemea mashamba, mvua haijakubali kunyesha kwa muda. Wengi wa wanaofanya kazi za ajira, hufanya kazi za kijungujiko. Sasa mabomba yatatoka wapi?na hata kama mabomba yenyewe yangekuwepo, juzi nimeskia kwenye runinga kkwamba bwawa la Fanisi ambalo ndilo lililotegemewa sana kutoa maji kwenye sehemu kame halitasambaza maji tena kwa sababu kiwango cha maji kimeshuka sana. Mabomba yenyewe yamejikaukia!

Ridhaa: Serikali imeanzisha mpango wa kusambaza huduma za maji na umeme katika sehemu za mashambani, hususan zile kame. Wanachohitaji ni subira tu. Na nadhani mwalimu wenu alisahau kuwaambia kuwa katika baadhi ya sehemu mna machimbo ya mawe ya ujenzi, vito, na hazina za

mamfuta. Wenyeji wana jukumu la kutumia raslimali hizi kujiendeleza.

Tila: Alituambia hayo pia. Lakini kuna tayari kampuni zakibinafsiambazo zimetumwahukokuchimbua madini haya. Isitoshe, kampuni zilioshinda zabuni za kuyachimbuamadinihayanizakigeni.Uchimbaji wenyeweunafadhiliwanawawekezajiwakigeni. Raiya watafaidika vipi?Fedha zinazotokana na raslimali hii yahofiwa kuwa zitaishia kwenye mifuko ya wageni. Zinatumwa kuendeleza nchi za hao hao wawekezajiwanaodaiwakuwawawekezaji.Ridhaa: Ni kweli lakini kumbuka kuwa kampuni hizi zimebuni nafasi za kazi. Wenyeji wamepata ajira!

Tila:Ambayomshaharawakenimkiawambuzi. Baba, kile ambacho raiyaa wanahitaji ni mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi na sera zenyewe za uongozilNa naona awamu hii, kama asemavyo mwalimu, wingu la mabadiliko limetanda.

**II. KISENGERE MBELE**.

Hii ni mbinu ambayo mwandishi hutumia katika Sanaa yake.

Inahusisha mwandishi kubadilisha wakati na kusimuliamamboyatakavyokuwasiku zausoni; au kutumia isiyo moja kwa moja kutabiri yatakayojiri. Mbinu hii pia huitwa utabiri.

Katika ukurasa wa 45;"Sasa anapotazama nyuma anaona kuwa ule utabiri wa 'wingu la mabadiliko' wa mwalimu ulikuja

Kutumia "Ni kweli mwalimu alikuwa ametabiri kuhusu wingu hili Ia mabadiliko ambalo kwa sasa limetanda (uk 44)

Tila:Ambayomshaharawakenimkiawambuzi. Baba, kile ambacho raiyaa wanahitaji ni mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi na sera zenyewe za uongozi!Nanaonaawamuhii,kamaasemavyo mwalimu, wingu la mabadiliko limetanda.

Katika ukurasa wa 70;Lunga alikuwa ameona kuwa maishayakeyalikuwayakielekeakudidimiahata kabla ya kuhamia makao hayo yake mapya ambayo anadai kuwa jaala kampeleka huko "Ametononeka si haba katika msitu huu. Hadiriki kuwaza kwamba msituhuuunastahilikuhifadhiwakwamatumiziya baadaye!Kabla ya jaala kumleta hapa, lunga aliuona mstakabali wa maisha yake ukiporomoka. Alikuwa ameipoteza kazi yake"

12. **NJOZ1 AU NDOTO**.

Mwandishi hutumia njozi au ndoto kutabiri jambo litakalofanyika au kufumbua jambo lililokuwa limefumbwa.

Katika ukurasa wa 2;

"Anakumbuka akimwambia mkewe Terry, "Milio hii ni kama mbiu ya mgambo, huenda kukawa na jam_

bo "Terry kwa ucheshi wake wa kawaida hakunyamaza "

"Ridhaa akamwambia, "wewe endelea kupiga hulu tu, lakini utakujakuniambia!"

Ridhaa alikuwa na ndoto ya kuwa kuna jambo mbaya au lisilo la kupendeza ambalo lingeweza kutendeka, na kwa kweli, njozi lake likawa ni la ukkweli wakati lilipo timia.

13. **KEJEL1**.

Hii ni mbinu ya Sanaa inayotumia maneno kudharau au kukemea kitendo au mtu fulani. Mwandishi pia anatumia mbinu hii kuwasilisha maudhui yake kwenye kazi yake ya kifasihi.

Katika ukurasa wa 15; "Kuna wale ambao hufia kwenye vitanda vyao vya mwakisu vitongojini baada ya kupiga haramu. Hawa husemekana kuwa wamekuwa nzi ambao kufia dondani si hasara. Hulaumiwa kwa kujitosa katika msiba wa kujitakia "

Hawa watua mabao wanakunywa pombe haramu na kufia kwao nyumbani ambako kumekithiri ukata, wanadharauliwa na kulinganishwa na huyo nzi afaye kwenye donda, kwani wanafanya jambo kwa hiari yao, huku wakijua madhara na matokeo yake ni yepi.

**14. UNUKUZ1 KUTOKA BIBI-IA.**

Hii ni mbinu ya kunukuu visa tofauti kutoka kwenye Biblia. As sumpta K.Matlei amejikita sana katika mbinu hii ya kunukuu

Biblia, kama tunavyoona kutokana na mifano ifuatayo.

Katika ukurasa wa 36; "Aliweza kuudhibiti ugonjwa wa shinikizo la damu ambao ulitokana na mshtuko wa kupoteza jamaa na mali yake dafrao moja. Awali akijihisi kama yule

Ayubu kwenye kitabu kitakatifu ambaye ibilisi aliifakamia familia na mali yake takriban kutwa moja!"

Katika ukurasa wa 46; "Umbali ulio kati yao, japo ni hatua tatu tu, waonekana kama upana wa bahari ya Shamu wakati Waisraeli walipokuwa wakikamia wokovu wao kutokana na dhuluma ya wamisri "

Katika ukurasa wa 47;

"Walishikana kukutu, kila mmoja akimwambia mmwenzake kimoyomoyo, "Ni hai! Sijafa!"

Ikawa ni kama Yesu anamhakikishia "Tomaso asiyeamini","Tazama hii mikono yangu. Nipe mkono wako, utie ubavuni mwangu. Usikose kuamini tena.

Katika ukurasa wa 34;

"Baada ya kuishi kwenye msitu wa Mamba kwa miezi sita, Ridhaa, Kaizari na familia yake walibahatika kurudi nyumbani kufuatia mradi ulioitwa na wanaharakati wa kupigania haki za kibinadamu: Operesheni Rudi Edeni "



**MARUDIO**

**AINA YA MASWALI**

Rapa mna maswali ya aina mbili.

-*Maswali ya insha*

-*maswali ya Muktadha wa dondo.*

***Maswali ya Insha.*** Haya ni maswali ambayo hutoa kauli inayohitaji kujibiwa kwa kirefu na kwa kina. Swali linaweza kuwa la jumla yaani linalohusu Riwaya nzima. Pia, swali laweza kulenga sehemu ya kazi husika katika nyanja na maudhui, wahusika na hulka zao, mafunzo na fani. Maswali haya huhitaji zaidi uwezo wa kukumbuka wa mtu, kupanga hoja na kuelezea msimamo au maoni yake kuhusiana nayo. Mtahini anahitajika kutoa hoja na kuziteteta kwa mifano dhabiti. Mtahiniwa asitumie vistari vistari, afafanue hoja kikamilifu akiandamisha mifano mingi kutoka kwa Riwaya

***Maswali ya muktadha wa dondoo.***

Maswali haya hujitokeza kwa namna ya maneno yaliyodondolewa kutoka kwenye kazi ya Fasihi. Dondoo hunukuliwa kisha maswali yanyohusiana na dondoo hilo huulizwa.

Dondoo laweza kuwa maneno ya mhusika mmoja ambaye hatatajwa au maelezo katika kazi. Maswali huenda yakarejelea matukio yaliyotokea kabla au baada ya dondoo. Katika

181

kulijibu swali la muktadha wa dondoo, mtahiniwa huhitajika kuangazia mambo yafuatayo;

*i) Kumtaja msemaji wa maneno haya v ii) Kumtaja msemewa(anayerejelewa)*

*iii) Kueleza mahali yalikofanyika mazungumzo haya.*

*iv) Kueleza kiinisababu ya mazungumzo haya kutokea.*

*1." Lakini itakuwaje historical injustice, nawe Ridhaa, hapo ulipo sichO kitovu chako?"*

*a) Eleza muktadha wadondoo*

**Jibu**

Hayo ni maneno ya Ridhac yaliyokuwa yokimpikia baada ya kumjibu Tila mawazoni. Hii ni baada ya Ridhaa kukubali maneno ya Tila ya hapo awai. Inadhihirika kuwa amekubali kuwa yeye ni mgeni, si mwenyeji.

*b) Eleza tamathali mbili za lugho zilizotumika kwenye dondOO hili (alama4)*

**Jibu**

Swali balagha- ...hapo ulipo sicho kitovu chako?

Kuchanganya ndimi- historical injustice.

*c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 6)*

Msemaji wa Maneno haya ni Ridhaa.

182

umuhimu wake.

Ridhaa ametumiwa na mwandishi kutLidnyesha na ukabila.

Ridhaa ni kielelezo cho Watu wasiobagua Watu wengihk hdkujali wanakijiji wenzake ni wa ukoo gani bali yeyea'iteke!20.

miradi ya maendeleo ili kuwafaidi wote.

Ridhaa ametumiwa kuuonyesha udhalimu wa watavoa qqac hadithia namna majumba yake yalivobomolewao

d)***Ni mambo gani yaliyowokumba wale ambao kitovu chOQSthO walicho ( Alamo 6)***

***Jibu***

Walichomewo nvurnbo zao kwa rnfano Ridha Olichomewa jumba lake (a kifahari.

Watu wao waliuwawa kwa mfanofamilia ya Ridhaa ilichomwg na Bwana Kedi jirani yao.

Walikimbia na kutorokea msituni.

Watoto woo walibakwa kwa mfano mabinti zake Kaizari walibakwa na vijcna wenzao.

Walitoroka kuacha makwao wakawa maskwotaau wakimbindgni kwa ndani.

Vllbumwa wenyjiFku hdikWjih7a a

***2.Maovu yametamalaki katika jamii ya Riwaya ya ChQj1a***

***Heri retea kauli hii kwa kutolea hoja kumi zisizopinglka (***

***ma 20)***

Katika jamii hii kuna biashara haramu koma ile ya uuzaji wa dawa za kulevya. Dick alipotekwa nyara oiazimika kuuza dawo za kulevya kwa muda wa miaka kumi.

Kuna ukabila- suaa hili la ukabiQ ilijitokeza kikamilifu wakati kulizuka vita vya boada ya kutawazwa. Majironi waliwageuko wenzao amboo wa!ikuwa wametoka katika kabia au ukoo tofauti na woo.

Kuna mauaji- watu wengj waiiwapoteza wapendwa wao kutokano no migogoro iiyozuko boada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya.

Katika jamii hii kuna matumizi ya pombe haramu- vijana wa vyuo vikuu wanabugia pombe hii ya sumu inayowafanya wengine kuiaga dunia.

Kuna ukeketaji wa watoto wa kike- wasichana wa Shule ya msingi wanapitishwa tohara. Wasichana wengine wanayapoteza maisha yao huku wengine wakiponea chupuchupu na kuwwa hospitalini kwa mfano Tuama anayeitetea mila hii iiyopitwa na wakati aliponea kidogo kuiaga dunia.

ndoa za mapema- wasichana wachanga wanglimishwa wolewa na vizee na kuacha masomo yao.

Kuna wiziuporaji wa mali ya wengine- wakati vita vya baada ya k utawazwa kuzuka, vatu walionekano kupora maduka ya

Kihindi, Kiarabu na hata ya Waafrika wenzao.

Katika jamii hii wanawake huavya mimba- Sauna alipachikwa mirnba na babake mlezi. Mamake mzazi alimsaidia kuavya kisha akamwonya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama wa babake.

Kuna baadhi yo wazazi wanaohusiana kimapenzi na watoto wao- Sauna afipachikwa mimba na babake mlezi. Mamake mzazi alimsaidio kuavya kisha akamwonya dhidiya kumwambja yeyote kuhusu unyoma wa babake.

Wanawake wengine katika jamii hii wanawaacha waume zoo no familia zao na kwenda kuyaishi maisha yao kwingineko mamake Umulkheri aliwaacha na kwenda kuishi mjini. Rejelea mhusika Naomi.

(Mwanafunzi aongeze hoja nyingine)

.

***3Fafanua namna mwandishi alivyotumia mbinu ya kisengere nyuma katika riwaya (alama 20)***

***' Jibu***

Mwandishi huyu amefaulu sana kutumia mbinu hii. Kisengere nyuypg imetumika katika mazingira yafuatayo

Ridhaa anakunibka n dinnaikratas1 VI ienezwakilfihm

Vikiwatahadharisha kuwa mna gharika baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya.

Kisa cha namna Mzee Kedi(jirani yao) alivyomsaidia Ridhaa kupata shamba lake na kuwa ameyadhamini masomo ya wapwaze wawili kimetolewa kwa urejeshi.

Mijadala baina ya Ridhaa na Tila imetolewa kwa njia ya urejeshi.

Kisa cha yule mwana wa mlowezi maarufu aliyemiliki mashamba ya Theluji Nyeusi katika Eneo la Kisiwa bora kimetolewa kwa urejeshi.

Kisa cha yule kiongozi wa Kiimla wa kike aliyekuwa akisimuliwa katika visakale cha majirani zao no narnna aivyowatumikisha wanaume kimetolewa kwa urejeshi.

Kaizari anasimuia yaliyojiri baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya aliyekuwa mwanamke kwa njia ya kurejelea.

Moyo wa Kaizari uipoanza kumsuta, alikumbuka kisa Cha wafuasi wa Musa ambao baada ya kukosa chakula jangwani wa!imshtumu kwa kuwatoa kule Misri.

Ridhaa ahpokuwa ameketi kwenye chumba cha mapokezi katika uwanja wa kimataifa wa ndege wa Rubia, alikumbuka namna walivyorudi nyumbani baada ya kuishi katika Msitu wa Mamba kwa miezi sita. Anakumbuka pia alivyokuwa akihisi.



Ridhaa anamkumbuka Tila bintiye aivyokuwa anapenda masuala yanayohusiana na sheria, haki na siasa.

Mwangeka alipolitazama tabasamu la babake, alihisi kuwa sasa amezingirwa na uzio imara. Akawa anakumbuka wimbo ambao mamake alizoea kumwimbia kila mara babake alipokuwa ameenda katika safari za kikazi.

Kisa cha namna Ami zake Kangata walivyokuwa wamekataa mwana wao aoewe na mtu wa ukoo mwingine kimetolewa kwa urejeshi.

Kisa namno Lunga aivyostaafishwa kwa kuwa na msimamo imara kuhusiar; a na sakata ya mahindi kimetolewa kwa urejeshi.

(mwanafunzi ashereheshee hoja hizi) zozote
10x2=20

**4.Fafanuo ufaofu wa anwani Chozi la Heri (alama 20)**

**Jibu**

Mwandishi anatueeza kuwa Ridhaa alipokwendo shuleni siku

YO kwanza alitengwa na wenzake kwani hawakuta ashiriki michezo yao. Kijana mmoja mchokozi alimwito 'mfuata mvua'

aliyekuja kuwashinda katika mitihani yote. Ridhaa alifululiza nyumboni na kujitupa rnchangani na kulio kwa kite na shake.

Mamake alimiwaza na kumhakikishia kumwona mwalimu keshoye. Tangu siku hii, huu ukowa ndio mwanzo wa maisha



ya heri kwa Ridhaa kwanibaada ya mwalimu Kuzungumza na wanafunzi umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano, Ridhaa alipea kwenye anga ya elimu hadi kufikia kilelecha Cha elimu na kuhitimu kama daktari.

Ridhaa alipotoka kwenye Msitu wa Mamba alijiona nafuu kwani wapwa zake- Lime na Mwanaheri walikuwa wamepata matibabu. Dadake Subira alitibiwa akapona. Mwamu wake Kaizari amepona donda lililosababishwa na kuwatazama mabin zake wakitendewa ukaini(kubakwa) na vijana wenzao. Ridhaa anajua kuwa Kaizari ni afadhali kwa sababu hakuna aliyemtenga na mmoja kati ya jamaa zake. Ridhaa anapomfikiria Kaizari anajiambia heri nusu shari kuliko shari kamili.

Ridhaa aliposikia sauti ya kike ikitangaza, tangazo lile lilimrudisha katika mandhari yake ya sasa. Aijaribu kuangaza macho yake aone anakoendo lakini macho yaijao uzito wa machozi ambayo alikuwa ameyaacha yamchome na kutiririka yatakavyo.

Wakati Ridhaa alimkazia macho Mwangeka-waka Mwangeka alikuwa akijiuliza iwapo babake amekuwa mwehu kwa kukosa kushirikiana na majirani kuchimba kaburi kuyazika majivumatone mazito ya machozi yalitunga machoni mwake Mwangeka. Akayaacha yamdondoke na kumcharaza yatakavyo. UvugU-

vugu uliotokana na mwanguko wa machozi haya uliulainisha moyo wake, ukampa amani kidogo. Moyo wake ukajaa utulivu sasa kwa kujua kuwa wino wwa Mungu haufutiki.



Vakatl Ridhaa_ alikuwa- akurismulia Mwangeka mrsiba ihyom-i wandama tangu siku alipoondoka kwenda kuweka amani Mashariki ya Katt Ridhaa alisita akajipagusa kijasho kilichoku- i wa kimetunga kipajini mwake kisha akatoa kitambaa mfukoni I no kuyafuta machozi yaliyokuwa yameanza kumpofusha. Uk 48 i Mwangeka alipokuwa ameketi mkabala no kidimbwi cha kuoge- lelea mawazo yoke yalikuwa kule mbali alikoanzia. Akawa ana- i kumbuka changamoto za ukauji wake. Akawakumbuka wanuna wake. Alipomkumbuka Annatila(Tila) mwili ulimzizima kidogo akatabasamu kisha tone moto la chozi likamdondoka. Katika Msitu wa Simba kulikuwa na maelfu watu waliogura makwao. Kati ya familia zilizoguria humu ni familia ya Bwana Kangata. Kwa Kangata na mkewe Ndarine, hapa palikuwa afad-hall kwani hawakuwa na pa kwenda kwa kuwa hata kule walikokuwa wakiishi awali hakukuwa kwao. Uk 57 Wakati Dick walikutana kisadfa na Umu katika uwanja wa ndege, walikumbatiana kwa furaha. Machozi yaliwadondoka wote wawili na wakawa wanalia kimyakimya. Walijua fika kuwa jaala ilikuwa imewakutanisha na kwamba hawatawahi kuten-gana ten°. Maisha sasa yalianza kuwa ya heri kwao. Baado ya miaka kumi ya kuuza dawa za kulevya, Dick alifaulu hatimaye kujinasua kutoka kwa kucha za mwajiri wake. Alianza biashara yoke mwenyewe ya kuuza vifaa vya umeme 189 :111 p

Sasa akaanza kujitegemea kwa kuwa amejiajiri. Alikuwo ameu_

fungua ukurasa mpya katika maisha yake. Maisha yake sasa ni ya heri.

Wakati Neema na Mwangemi walikabidhiwa mtoto wao wa kupanga na Mtawa Annastacia, Mwaliko alimkumbatia Neema na kumwita mama na kumwahidi kuwa ataenda naye. Neema alidondokwa na chozi la furaha na kumkumbatia Mwaliko kwa mapenzi ya mama mzazi. Hili lilikuwa ni chozi la heri kwa

Neema.

(mwanafunzi aongezee hoja) zozote IC)x2=20

5.***Ukabila ni tatizo sugu katika nchi nyingi za kiafrika. Tetea kauli hii ukirejelea chozi fa herj (aiama 20)***

Jibu

Ukabila ni matendo au fikira za mtu za kuthamini kabila lake mwenyewe tu na kuwabagua wa makabila mengine. Ukabila umejitokeza kama ifuatavyo katika Chozi la Heri.

Subira alitengwa na familia ya mume wake kwa kuwa wa kabila tofauti na lao. Mwanaheri anatueleza kuwa mama yake alikuwa ametoka kwenye jamii ya Mamwezi lakini babake alikuwa wa jamiii tofauti. Kila mara Subira aliitwa 'muki' au huyo wa kuja.

Kwa miaka mingi aliweza kuvumilia kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiwa kwa asiyoyatenda. Mwishowe alihiari kujiondokea na kwenda mjini alikojinywea kinywaji kikali, akafa.



ia alitengwa na watofs u em am ao awa um a a o iriki katika michezo yao. Kijana mmoja alimwita 'mfuata myua'

jambo lililomuumiza sana Ridhaa.

Mzee Kedi alimtendea udhalimu Ridhaa na kuiteketeza aila yoke licha ya wao kuwa majirani kwa miaka hamsini. Ridhag glifanyiwa hivi kwa kuwa alikuwa ametoka kwenye kabila tofautina

Kedi.

Ami zake Kangata walimsuta mno kwa kumwoza mwanawao kwa mtu wa jarnii tofauti na yao. Walishangaa ni vipi mwana woo ataozwo kwa mtu wa ukoo ambao huvaa nguo ndninje.

Waliamini kuwa ukoo huo huza majoka ambao hata kiporo cha juzi hayawezi kukupa.

Ndoa ya Selume iisambaratika baada ya Vitasvya kutawazwa kwa kiongozi mpya. Alibaki mwenye kilio baada ya wambea kumfikishia ujumbe kuwa mume wake amekwisha kuoa msichana wa kikwao.

Tulia alimsaidia Kaizari kufunganya na kumsindikiza had( njia panda. Alimkumbatia na kumwambia kuwa mwenyeZi mungu ndiye hupanga na nguvu na mamlaka pia hutoka kwake. Akamjuvya kuwa uongozi mpya umezua uhasama kati ya koo ambazo

Zimeishi kwa amani kwa karibu kame moja.

Sauna alishikwa na polisi "

**a. Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)**

Jibu

Maneno haya yalisemwa na Mwaliko. Alikuwa akiwaambia

Umulkheri na Dick. Tendo hili lilitukia katika mkahawa wa Majaliwa walipokutana kisadfa. Hii ni baada ya Mwaliko kumpeleka babake mlezi maeneo yale kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake.

**b. Fafanua sifa tatu za msemaji (alama 6)**

Jibu

Msemaji ni mwa!iko. Ana sif zifuotozo:

Mwenye maadii mema- Mwaiko alipoleewa na Mwangemi na

Neema aiinukia kuwa ghuamu mwenye nidhamu ya hali yajuu akiwaheshimu wazazi na majirani na kuwatii wazazi.

Mwenye shukrani- Mwaliko aliamua kumnunulia babake chakula Cha mchana siku yake ya kuzaliwa kwenye hoteli ya Majaliwa

Mwenye bidii- alifanya bidii masomoni hadi kufikia Chuo kikuu

Alijisajili kwa shahada ya uzamili katika taaluma ya mawasiliano na kuhitimu. Mwaiko anafanya kazi yake kwa bidii ya mchwa.

Zozote 3x2= 6

'Iamathali

(alama2)

moja ya ug yotu

Kuchanganya ndimi- Auntie d. Ni kwa nini Auntie Sauna alishikwa na polisi? Elezea kikamilifu (alama 8)

Jibu

Baada ya IJmu kupiga ripoti kwenye kituo cha polisi kuwmnduguze wanuna womepotea, Polisi walifanya uchunguzi WOO ng kujua kuwa walitekwo nyora. Aliyetekeleza kitendo hiki ni kijakazi Sauna. Sauna alikewa akimfanyia biashara Bi. Kangora. Polis walipojua mahGt; oikokuwa akijificha Bi. Kangara, walishika njia hadi nyumbani kwake ambako waliwaa mbaroni Bii Kangara na Sauna. Walifikishwo mahakamani na kushtakiwa kwa kosala ukiukaji wa haki za watoto hivyo basi wakafungwa miaka saba gerezani na kazingumu.

***7. Fafanua namna mbinu ya sadfa ilivyotumiwa atika***

***Riwaya (alama 20)***

Jibu sadfa ni matuki0 mawili ambayo hayakupangwa kutukia

Wakati mmoja. Sadfa imejitokeza katika mazingira yafuatayo.

KUkutano kwa IJmu na Dick kwenye uwanja wa ndege kulifg

nyikalisadfa -UrnThigEWci lakini cheti choke cha usafiri kikawa kimechelewa. Safari y ikawa leo na ndipo Umu na Dick wakakutana. Ni sadfa kuwa wakati Umu anampa Dick ushauri wakiwa kotikai safari, ndipo Dick alikuwa ameamua kuyabadilisha maisho ypkejl Ni sadfa kuwa Mwangeka ndiye mlezi wa Umu no Dick naye binamu yoke Mwangemi ndiye mlezi wa Mwaliko Ikumbukwe kuwa Umu, Dick no Mwaliko ni ndugu. Ni sadfa kuwa hoteli aliyoichagua Mwaliko kumpeleka babake ill amnunulie chakula cha mchana ndiko akina Umu walikuwal no wazazi wake. Kukutana kwa Mwaliko na ndugu zake wawili ilikuwa ni sadfa. Hakujua kuwa wangekutana kwenye Hotel ya Majaliwa. Ni sadfa kuwa siku yoke Umu yo kuzaliwa ilikuwa ndiyo siku ya kuzaliwa kwa Mwangemi. Ni sadfa kuwa siku aliyoitwo Ridhaa kwenda kumhudumia mgonjwa ndiyo siku Gila yoke iliangamizwa no kumponyoka. Mwanafunzi aongezee hoja

8. **Jadili maudhui ya kifo kama yanavyoangaziwa katika Riwaya (alama 20) Jibu Kifomauti ni hali ya kutokwa na uhai** 194

ama e aa a naga un ffdhaat um u a maneno marehemu mamake kuwa mwanamume hufumbika hlsia na kuwa machozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha.

Terry na wanawe walikumbana na janga hili Ia kifo baada ya kuchomwa wakiwa ndani ya nyumba yao.

Kangata na Ndarine waiiiaga dunia- mwandishi anatujuvya kuwa kwa sasa, miaka mitano imepita na Kangata na Ndarine wameipa dunia kisogo.

Kiriri alikumbona no mouti- mwandishi ametueleza kuwa Kiriri aliiaga dunia muda mfupi kutokana na kihoro cha kuflisikang ukiwa aliokuwa ameachiwo na mkewe Annette na wanawe. Subira alikumbana na mauti- baada ya Subira kuondoka nyumbani afienda mjini Kisuka na baada ya miezi kadha mumewe alimpata kwenye churnba chake akiwa amejifia, Nduguye Mwangeka alikumbana na mauti- Mwangeka anapomkumbuka Tila anatabasamu kisha tone moto la chozi linamdondoka. Kumbukumbu ya Annatila inavuta taswira ya mnuna wake mkembe aliyefariki dunia akiwa na umri wa miaka sita wakati Life Mwangeka akiwa na urnri wa miaka kumi na miwili tonna ile ilipowafika.

Baada ya Lunga kuachwa na mkewe aliiaga dunia- mwandi

shi dhu-jVykWTbFY7Sho wa mwaka alifariki na kuwaacha watoto wake na mikononi mwa wao.

Vijana waliofyatuliwa risasi waliiaga dunia- tumeelezwa walimiminiwa risasi vifuani mwao na wote wakaiaga dunia kifo cha kishujaa kwani walijitolea mhanga kupigania uhuru tatu. Kaizari alitokwa na machozi na kuwahurumia Vijana hawa waliokufa kifo walichoweza kukiepuka.

Lily Nyamvula na mwanawe Becky waliiaga dunia- Mwangeka ameketi mkabala mwa kidimbwi cha kuogelea nje ya jumbo lake

Ia kifahari ambalo yeye alitiona kama makavazi ya kumtonesho donda lililosababishwo no kifo cho mke wake Lily Nyamvula, Mgonjwa mmoja aliyejifia ni kijana anayesomea shahada ya uzamili, aiikuwa mwothiriwo wa pombe haramu.

Waschana waliokeketwa waliaga dunia- Mgonjwa kwa jina

Tuama alibahatika kwa kuwa hakuiaga dunia kama wenzake waliokuwa wamepashwa tohara kama yeye.

Tunaeezwa kuwa miezi mitatu baadaye gmi yakg Mwdngeka aliyeitwa Makaa alichomeka asibakie chochote alipokLjWa aakiwaokoa watu ambao walikuwa wakipora -mafuta kdtOka kwenye lori lililokuwa lignebingiria.

Mwanafunzi aongezee hoja. Zozote 10*2g2Qi

Mwongozo wa chozi la Heri

***9. Jadili maudhui ya 'asasi ya ndoa' kama yalivyuangaziwa riwayani (alamo 20)***

***Jibu***

Ndoa ni maofikiano rasmi baina ya mwanamume na mwanamke Hi waweze kuishi pamoja kama mke na mume.

Ridhaa alikuwa na mke kwa jina Terry. Walibarikiwa kuwa na watoto wafuatao: Mwangeka, Tila na marehemu Dede. Ndoa hii haikudumu kwani janga la moto iiliisambaratisha aila hii na ndipo Terry, Til a, Lily na Becky wakaiaga dunia. Ridhaa akabaki mjane. Mwangeka alikuta na Lily Nyamvula katika chuo kikuu na kumwoa. Walibarikiwa na mtoto mmoja kwa jina Becky. Ndoa hii haikudumu kwani Lily na Becky waliangamia kwenye janga la moto. Baada ya ndoa ya mwanzo kusambaratika, Mwangeka alimwoa

Apondi. Walibarikiwa na mwana wa kiume kwa jina Ridhaa.

Mwangemi alimwoa mwanamke kwa jina Neema. Hawakufaulu kupata mwana wao kindakindaki japo walipanga mwana wao kwa jina Mwaliko.

Kangata alikuwa na mke wake kwa jina Ndarine. Walibarikiwa na wana wafuatao. Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na Akelo Kiriri.

Lucia Kiriri -Kangata – alikuwa ameolewa katika ukoo wa

Waombwe ambao awali walikuwa maadui sugu wa ukoo wa



Mwongezo wa chozi la Hoi yamvua oa iFiFifi7fina u a mzima lakjni kutokana na Msimamo imara wa Kangata hg jlisimama. Watu wa ukoo wa kina Kangata walishangaapikwo nini mwana wao

akaozwa kwa watu ambao huvag nguo nje na pia huzaa majoka ya rndimu ambayo ni machovo kupjr dukia.

Kaizari alikuwa na mke kwa jina Subira. Waliborika no mabinti wawili, Lime na Mwanaheri.

Lunga alikuwa na mke kwa jina Naomi. Walikuwa wa watatu, Umu, Dick no Mwaliko. Ndoa hii haikudumu

Naomi alimwacha Lunga na kwenda mjini alikokuwa shangingi kwelikwe!i.

Pete na Fungo-tunaelezwa kuwa Pete alipoingia darasa la Sba alipashwa tohora nao wajombake wakapokea posa na baaye'

mahari kutoka kwa buda mmoja kwa jina Fungo aliyemuoa kama bibi wa nne. Ndoa hii haikudumu kwani Pete alihiarikumwacha baba huyu.

Mwanafunzi aongezee hoja. Zozote

**10. Jadili maudhui ya nafasl ya mwanamke katika jamii (alama**

**20)**

**Jibu**

Mwanamke amesawiriwa kwa namna mbalimbali:

Mwanamke ni Msomi-Tila alikuwa akimudu masuala ya sheria.

Hakuna aliyethubu kuuchangia mijadala kwani katika masuala ya sheria Tila alikuwa ameyamudu kweli kweli. Selume- Ridhaa alimfariji na kumwomba asilie kwani mwana wake yu hai tena ana kisomo na amehitimu kama mkunga, anaweza kujitegemea. Umulkheri pia alisoma na kuhitimu vizuri.

Mwanomke ni Mjinga- Tuama alikuwa amejipata katika hali mbaya kwa kukubai kupashwa tohara. Alibahatika kwa kuwa hakuiaga dunia kama wenzake. Tuama anaitetea mila hii ya upashaji tohara kwo wanawake eti haijapitwa na wakati kwani bila toharo mwanamke hubakia kuwa mtoto. Huu ni ujinga na upumbavu.

Mwanamke ni mwenye bidii- tunaelezwa kuwa Umulkheri alikuwa nyuma yake Dick akiwa amepiga foleni. Anasafiri ng'ambo kwa shahada yake ya uhandisi katika masuala ya kilimo. Umu, baada ya kuchukuliwa na Mwangeka na Apondi alifanya bidii masomoni na kufuzu vyema katika mitihani yake.

Mwanamke ni mwenye tamaa ya mali- Naomi hakuwekwa na mazingira haya mapya(Mlima wa Simba). Asubuhi moja

199

' alimtumia Lunga ujumbe na kumtaarifu kuwa ameohdoka7;

akatambe na ulimwengu na huenda akaambuia Cha kUmsaidia

Lunga kuikimu familia. Akawaacha Lunga na wanawe. Mwanamke ni mwenye huruma- Apondi na Neema walijitwikajukumu la kuwalea wana ambao si wao kwa upendo na imani.

Mwanamke ni katilimuuaji- Mamake Sauna aimsaidia Sauna kuavya mimba aliyokuwa amepachikwa na babake mlezi. Neema naye alikuwa ameavya mimba nyingi akiwa kwenye Chuo kikuu.

Mwanamke ni mwenye majuto- Neema aikuwa mwenye kujuta kwa kupoteza nafasi ya kupanga mtoto.

Mwanamke ni mwenye kujiheshimu- Zohai amewahi kupigana na majitu yaiiyokuwo yakitako kuuhujumu utu wake kwa kumnyanyasa kijinsia.

Mwanamke ni mcheshi- Terry amboye kawaida yake ni mcheshi hakunyamaza bali alimwambia Ridhaa kuwa kwake lazima kila jambo liwe na kiini.

Mwanafunzi aongezee hoja. Zozote 10*2=20

**11. Fafanua maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii (alama**

**20)**

r70...001.-yawn. Wana(jinsia zote) Ni wasomi- vijana kama Tila, Umu na Mwaliko walikuwa w, .cnye bidii masomont Walanguzi wa dawa za kulevya — Dick alikuwa akilangua za kuievya kwa muds wa miaka kurni. Wenye Umu no Dick walikuwa na bidii katika masomo yao-IF Wojingo- vijana wengine wa kike walikubali kukeketwcr 11 Wengine waliiaga dunia na wengine kulazwa zahanatini if Waraibu wa dam- Dick anasema kuwa alikuwa akitumia dowd: q1 hizi iii kujirahisishia kozi yoke ya kulangua. Wapenda fujo- vijana ndio waliotumiwa na wanasiaso kuute-1F keleza uovu wa mouaji no kuyaharibu mali ya wenzao. Katili- kung vijana waliowabaka mabinti zoke Kaizari no kumuumiza mke wake. I. Wasio no huruma- vijana wengine walikuwa wakiwaua wenzao bila huruma. Wasio na msimomo dhabiti- vijana wengine wakipotoshwa na wanasioso bila kuwaza na kuwazua 4,1911a funzi opngezee hoja.

Zozote 10 X7=29